**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 10 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maji kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN – K.n.y. MHE. GIDEON A. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:**

Maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 166

**Tatizo la Upungufu kwa Walimu Nchini**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilianzisha mradi wa kuziba pengo la upungufu wa walimu wa shule za msingi chini ya mpango wa MMEM unaoishia mwaka 2006 na kwa kuwa, mradi huo umekuwa wa manufaa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, mradi huo utakapomalizika upungufu wa walimu wa shule za msingi hautatokea tena?

(b) Je, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ualimu kwa mwaka mmoja au itarudia miaka miwili baada ya mradi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ulianza rasmi mwaka 2001/2002 kwa lengo la kuboresha Elimu ya Msingi na kuongeza uandikishaji wa watoto wenye umri wa kuanza shule ambao ni miaka 7. Aidha sambamba na uandikishaji huo, mitaala ya mafunzo ya Ualimu ilirekebishwa ili kozi ya ualimu ya Daraja 'A' iweze kutolewa kwa kipindi cha Mwaka mmoja Chuoni na mwaka mmoja kwa vitendo katika shule za msingi. Lengo lilikuwa ni kukidhi upungufu mkubwa wa walimu uliokuwepo. Kuanzia mwaka 2002 hadi mwezi Machi, 2006, jumla ya walimu 47,290 walihitimu mafunzo ya ualimu Daraja la 'A' chini ya mpango huo na wote wamepangiwa shule mbalimbali katika Mikoa yote Tanzania. Aidha, Awamu ya Kwanza MMEM inamalizika mwaka huu 2006 na Awamu ya Pili itaanza 2007 hadi 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa walimu wa shule za msingi utaendelea kuwepo kutokana na ufunguzi wa shule mpya za msingi, walimu kama watumishi wengine kufariki, kustaafu au kuachishwa kazi. Kwa hiyo, vyuo vya ualimu vilivyopo nchini vitaendelea na jukumu lake la kutoa mafunzo ya ualimu Daraja 'A' kila mwaka ili kukabiliana na upungufu utakaojitokeza.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya ualimu ya mwaka mmoja chuoni na mwaka mmoja kwa vitendo shuleni yaliyotolewa kwa lengo la kukidhi mahitaji makubwa ya walimu yaliyotokana na ongezeko kubwa la uandikishaji wa wanafunzi wa Darasa la Kwanza baada ya Mpango wa Elimu ya Msingi MMEM kuanzishwa. Kuanzia Julai, 2006 utaratibu huo hautatumika tena, badala yake wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na mafunzo ya ualimu Daraja la 'A' watapata mafunzo hayo kwa miaka miwili chuoni kama ilivyokuwa awali.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa miongoni mwa matatizo yanayosababisha upungufu wa walimu mashuleni ni pamoja na mazingira yasiyoridhisha kwenye shule za msingi, pamoja na ukosefu wa nyumba za walimu kuishi hasa pale shuleni na kwa kuwa hali hii inalikabili sana Jimbo la Muleba Kaskazini na Wilaya nzima ya Muleba.

Je, leseni itakuwa tayari katika mpango huu hasa mwaka huu wa fedha kuhakikisha kwamba inatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba madarasa yanaendelea kujengwa na nyumba za walimu zinakuwepo katika shule za msingi ili walimu waweze kupata mahali pa kuishi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuongezea kama ifuatavyo:-

Katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea vizuri kabisa kwamba Mpango wa MMEM utakuwepo. Awamu ya pili inaanzia mwaka 2007 mpaka 2011. Kila mwaka kutakuwa na mpango huo fedha zitakuwa zinatengwa kadri zinavyopatikana ili kusaidia nguvu za wananchi katika kujenga madaraja na pia katika kujenga nyumba za walimu. Serikali inafahamu wazi kabisa kwamba ukitaka walimu wafanye kazi vizuri hasa sehemu za vijijini lazima nyumba za walimu ziwepo na kwa msingi huo Serikali itaendelea kama nilivyosema kusaidia nguvu za wananchi ili nyumba za walimu zipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa kuongezea kwamba ni vizuri niiweke wazi kwa kutoa wito kwa wananchi wote kusaidia katika ujenzi wa nyumba za walimu. Walimu ni wengi kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba mwaka jana tulipata walimu 46,000. Sasa kupata nyumba za kutosha walimu 46,000 si rahisi kwa kweli kwa Serikali kubeba mzigo mkubwa huo. Naomba nitoe wito tena kwa wananchi kwamba wajitolee kwa hali na mali, halafu Serikali itaunga mkono ili tufikie azma ya kuwasaidia walimu kuwa na nyumba vijijini kama jambo muhimu sana la kuwawezesha kufanya kazi katika shule na hasa katika sehemu za vijijini. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kipindi kilichopita waliweza ku-*train* walimu 46,000 kwa nchi nzima na sasa hivi wamesema kwamba hawana nafasi tena ya kuweza kuwa-*train* hawa walimu wengine 46,000. Je, Serikali haijui kwamba ina shule ambazo zina wanafunzi 400, 500 ambazo zina walimu 2 tu na kuwa na upungufu mkubwa wa walimu na vyuo vya ualimu haviwezi kutosheleza kutoa walimu ambao wanaweza kufundisha shule zote katika nchi nzima? Naomba nijibiwe hilo swali. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu alilojibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, ni kwamba tulichoacha sasa hivi au ambacho tunategemea kwa kweli kukiacha ni ule utaratibu wa

kufundisha walimu kwa mwaka mmoja na baadaye wanapata mafunzo wakiwa kazini kwa mwaka mwingine wa pili. Akaelezea kwamba sasa tunarudi kwenye utaratibu wa zamani, kwa sababu mahitaji yaliyokuwepo wakati ule kutokana na ongezeko la shule nyingi kutokana na Mpango wa MMEM, sasa hivi angalau walimu wamefikia hatua fulani ya kutosheleza kwa kiasi kikubwa kwa hiyo, tunarudi kwenye utaratibu wa zamani wa kuwafundisha hawa walimu kwa miaka miwili, badala ya ule mtindo wa zamani.

Kwa hiyo, hatuwezi kuacha kufundisha walimu tutaendelea tu, kwa sababu shule zinaendelea kuwepo kama tulivyosema wengine wanastaafu, wengine bahati mbaya wanafariki. Kwa hiyo, kufundisha au mafunzo ya ualimu yataendelea tu. Ikitokea kwamba ongezeko limekuwa kubwa zaidi basi tutabuni mkakati mwingine wa kuongeza walimu kwa wingi halafu tunarudi tena kwenye utaratibu wa kawaida. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 167

***Ward Development Committee***

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa *Ward Development Committee* ni chombo kikubwa cha Maendeleo katika nchi yetu na kwa kuwa, chombo hicho kina jukumu la kupanga na kuratibu shughuli zote za Maendeleo katika Kata na kwamba, kwa mujibu wa Sheria Na. 7 na 8 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, wajumbe wa Kamati hiyo ni Mheshimiwa Diwani ambaye ni Mwenyekiti, pamoja na Wenyeviti wa Vijiji:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa, katika nchi yetu kuna *WDC* ambayo imeundwa na kijiji kimoja?

(b) Kwa kuwa, jukumu la *WDC* ni kupanga na kuratibu shughuli zote za Maendeleo katika Kata na iwapo zipo *WDC* zenye wajumbe wawili tu yaani Diwani na Mwenyekiti wa Kijiji kwa vile kata hiyo inaundwa na kijiji kimoja tu. Je, Serikali itakubali kuwa kwa kuweka maendeleo na hatma ya wananchi zaidi ya 3,000 mikononi mwa wajumbe wawili tu wenye kura ya uamuzi unawanyima wananchi hao mchango wa maamuzi sahihi ya vikao vikubwa vya *WDC* na Serikali inatoa kauli gani juu ya kutazama upya muundo huo?

(c) Ikiwa hali hiyo ni kweli na kwamba mfumo huo wa *WDC* hata kama unawashirikisha watalaam bado wajumbe wenye mamlaka ya kupiga kura ni wachache. Je, Serikali haioni kuwa inaleta kipingamizi na kikwazo kikubwa katika vita dhidi ya umaskini na hata utekelezaji wa *vision* 2025 na hivyo inatoa maelekezo gani ya haraka kuondoa hali hiyo wakati ufumbuzi wa kudumu unatafutwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo taarifa kuwa katika Wilaya ya Karatu, kuna Kata iliyoundwa na kijiji kimoja tu. Kata hiyo ni Oldeani yenye kilometa za mraba 105 na kijiji kilichopo kinaitwa Oldeani. Kata ya Oldeani ilikuwa na vijiji vinne ambavyo ni Oldeani, Mangola Juu, Makhoromba na Endashang'wet. Mwaka 1994 kata iligawanywa kuwa katika kata mbili, kata hizo ni Daa na Oldeani. Kata ya Daa hivi sasa ina Vijiji vya Mangola Juu, Makhoromba na Endashang'wet na Kata ya Oldeani ina Kijiji cha Oldeani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba jukumu la *Ward Development Committee* ni kupanga na kuratibu shughuli zote za maendeleo katika Kata. Kwa mujibu wa Sheria kila Kata inakuwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata yenye wajumbe wafuatao:-

(i) Diwani ambaye ni Mwenyekiti;
(ii) Wenyeviti wote wa vijiji katika Kata;
(iii) Diwani wa Viti Maalumu mkazi wa Kata husika;
(iv) Watu walioteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali au vikundi vya kiraia, kama vile wanawake, vijana, walemavu, n.k. lakini hawa hawaruhusiwi kupiga kura; na
(v) Afisa Mtendaji wa Kata ambaye ni Katibu wa *WDC*.

Hivyo Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Oldeani ina wajumbe wote niliowataja na sio wajumbe wawili kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema. Aidha mchango wa maamuzi sahihi unaotolewa na wajumbe watatu ni uwakilishi wa kutosha kwa wananchi zaidi 3,000 walioko katika kijiji hicho cha Oldeani na Kata ya Oldeani ambacho kimeundwa na kusajili kwa kufuata taratibu zote zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imewahi kujitokeza pia katika Halmashauri ya Mbeya, Kata ya Ikukwa mwaka 1999. Hata hivyo, kwa sasa Kata ya Ikukwa iliyoko Mbeya ina vijiji 3. Mazingira ya Mbeya yaliruhusu kuongeza vijiji kwa sababu kuna ardhi ya kutosha. Kwa kesi ya Karatu, Mazingira yake hayaruhusu kwa sababu ardhi inamilikiwa kwa mkataba. Kwa hiyo, ardhi ya kupanua katika kijiji hicho haipo. Kata hii inaundwa na mashamba 30 ya mkataba na Mji Mdogo wa Oldeani tangu mwaka 1994. Mashamba haya ya mkataba wa miaka 99 na yalianzishwa mwaka 1937.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa Kata ya Oldeani na kijiji kimoja cha Oldeani ni suala la kweli kama ambavyo nimekwisha sema. Aidha naomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, kwamba hali hii inaleta kipingamizi na kuwa kikwazo kikubwa katika vita dhidi ya umaskini. Hii ni kwa sababu wako watalaam katika Kamati hiyo ambao wanasaidia kutoa mawazo ya kitaalam kwa ajili ya maendeleo ya kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo suala la kuongeza kijiji lipo kwenye uwezo wa Halmashauri husika. Kama Halmashauri ya Karatu itatoa azimo la kugawa kijiji hicho

nashauri maombi yawasilishwe kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ili kuangalia uwezekano wa kutolea uamuzi.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili. Aidha namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake.

(a) Kwa kuwa Kijiji cha Oldeani alichokieleza kina mashamba 30 ya mkataba kama alivyosema na kwa kuwa mashamba haya tayari yana sura ya vitongoji kwa sababu hata Wenyeviti wa Vitongoji wapo, lakini mazingira hayo ni magumu kwa sababu hawaruhusu wale wenye vitongoji kuwa kijijini na suala hili lilishafikishwa kwa Waziri aliyetangulia. Je, sasa Serikali itakubali kuliangalia suala hili kama Waziri alivyowasilishiwa maana yake liko tayari ndani ya Ofisi ya Waziri?

(b) Kwa kuwa Kata ndiyo chemchem, msingi, nguzo ya mapambano ya vita dhidi ya umaskini na kwa kuwa watalaam hawa au Wenyeviti wetu na Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji na Madiwani ndiyo hasa majemedari wa mapambano. Je, Serikali iko tayari sasa kuwawezesha Wenyeviti wa Vijiji, wa Vitongoji na Madiwani kwa maana ya elimu na hasa kwa maana ya fedha kwa maana ya malipo ya mishahara ili waweze kuendesha vita hivi vizuri? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kata inapoanzishwa viko vigezo vinavyotazamwa. Lakini na vijiji vile vile vinapoanzishwa viko vigezo vyake vinavyotazamwa. Kwa upande wa Kata ya Oldeani naweza kusema tu ni kwamba mazingira yale ambayo ni *peculiar* kwa eneo hilo ndiyo hasa kikwazo kikubwa kwa upande mmoja. Lakini kwa pande mwingine nilitaka Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba kijiji kimoja ni kaya kama 250 ambayo ni wastani wa watu kati ya 2,500 mpaka 3,000 au maeneo mengine yanazidi kidogo.

Kwa hiyo, kwa upande wa kata hiyo ambayo ni kijiji hicho, vile vile kwa maana ya idadi ya watu, kinawiana na mahitaji halisi. Lakini niunganishe sasa na swali lake linalofuatia, ni kweli kwamba jambo hili liliwasilishwa ofisini wakati ule tulijaribu kulifanyia kazi, lakini kutokana na vikwazo hivi tulivyovionaa ikaonekana haitakuwa rahisi kwa sababu idadi ni ndogo ingawa mahitaji ya kiutawala ni makubwa.

Kwa hiyo, labda kama alivyosema watu tuliangalie tena upya lakini tutalazimika vile vile kuzungumza na wenye mashamba ili tuone kama tutakuwa radhi kuweza kuridhia masuala ya utawala yaweze kuenezwa katika eneo hilo.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo Oldeani kijiji kimoja kuwa ni kata na kama vile ilivyo Oldonyosambu katika Wilaya ya Ngorongoro.

Je, mahali inapotokea kwamba Halmashauri katika Kata fulani vipo vijiji vingi zaidi ya 11 kama ilivyo katika Kata za Namanyere kule Nkasi, Kate, Kilando, Chala, Kabwe kwamba watu wengi zaidi 20,000 kwenye kata moja na vijiji ni zaidi ya 10. Inapotokea hivyo kama Halmashauri imeomba vipewe kata kwa kugawanya, je, Serikali itakuwa tayari kama vile Nkasi tulivyoomba katika maeneo niliyoomba? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Nkasi mara ya mwisho walikuwa ni miongoni mwa Halmashauri walikuwa wamewasilisha maombi kwa ajili ya kugawa Kata kutokana na ukubwa vijiji. Tuliwahi kueleza hapa kwamba tulipata maombi 225 na kati ya 225 Kata zilizokubaliwa ni Kata 42. Kwa bahati mbaya ile ya Nkasi waliyokuwa wameomba haikukidhi vigezo na tuliwaambia wajitahidi kuvitazama tena upya ili tuweze kuona nini tunaweza tukafanya.

Lakini naomba niharakishe kwamba zoezi hilo kwa sasa tumelianza upya kujaribu kutatazama maombi yote tena na kama nilivyosema tumeagiza Halmashauri zile ambazo zilishindwa kutimiza vigezo kwa sababu mengi yalikuwa ni masuala ya kitaalam tu wakae tena upya wawasilishe maombi haya ili kabla ya mwaka huu tuone kama zoezi hili tunaweza tukawa tumelimaliza na tukaomba vibali ili baadhi ya Kata ziweze kugawanywa zaidi. (*Makofi*)

Na. 168

**Vijiwe vya Vijana Mijini.**

**MHE. MWADINI A. JECHA (K.n.y. MHE. BAKAR SHAMIS FAKI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeshauriwa kuvifanyia utafiti vijiwe vya vijana kwa lengo la kuvibadilisha kuwa vya uchumi.

(a) Je, ni vijiwe vingapi vimeshafanyiwa utafiti na kubadilishwa kuwa vya uchumi?

(b) Je, ni fedha kiasi gani zimetumika kwa shughuli hiyo kwa Mkoa wa Dar es Salaam hadi Desemba, 2005?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH SOLOMON SUMARI):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, napenda nitoe maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa vijiwe vya vijana ulianza katika mwaka wa fedha wa Serikali 2002/2003, kwenye iliyokuwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Tathmini hiyo ya kuainisha vijiwe vya vijana katika Mkoa wa wa Dar es Salaam, ilikuwa na lengo kuu la kuiwezesha Wizara kupata taarifa yenye uhakika kwa ajili ya kupanga mikakati mbalimbali ambayo itawezesha kuvigeuza vijiwe vya vijana kuwa sehemu ya uzalishaji mali na hivyo kuwapatia vijana kipato kwa njia ya Kujitegemea. Tathmini hii ilihusisha Maafisa toka Wizarani, Maafisa Vijana wa Manispaa tatu za Mkoa wa Dar es Salaam, Maafisa Watendaji na Viongozi wa Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa muhimu za vijiwe zilizokusanywa zilizingatia mambo yafuatayo: Jina la Kijiwe, Mahali kilipo, idadi ya washiriki, shughuli zinazofanywa na kijiwe, matarajio na mahitaji ya kijiwe. Aina ya vijiwe vilivyoainishwa katika utafiti huo ni pamoja na:-

- Vijiwe vya Biashara ndogondogo;
- Vijiwe vya Uzalishaji mali;
- Vijiwe vya Wapiga debe na *day woker;*
- Vijiwe vya porojo, maongezi ya Siasa na michezo;
- Vijiwe vya kupanga mikakati ya vitendo viovu;
- Vijiwe vya wavuta bangi na matumizi ya dawa ya kulevya;
- Vijiwe vya vibaka na waporaji;

Mheshimiwa Naibu Spika,baada ya maelezo hayo ya awali sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Babar Shamis Faki, Mbuange wa Ole, kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya vijiwe vilivyoainishwa katika Mkoa wa Dar es Salaam ni 509 na vina jumla vijana 8,967

(b) Kufikia Desemba 2005, kiasi cha fedha kilichotumika katika tathmini ya kuanisha vijiwe hivi katika Mkoa wa Dar es Salaam ni shilingi 1,000,000/= .Kwa kuzingatia umuhimu wa suala zima la ajira na maendeleo ya vijana, zoezi hili sasa litaendelea mwaka huu wa 2006/2007, siyo tu kwa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam

bali pia litajumuisha Majiji ya Mwanza, Tanga, Arusha na Mbeya, kigezo kwa miji hii ni kuwa inakua haraka. Kiasi cha shilingi 12,800,000/= kimetengwa kwa zoezi hilo.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa alieleza kwamba kati ya vijiwe viko vijiwe ambavyo shughuli zake ni za kupora na viko vijiwe ambavyo shughuli zake ni uvutaji wa bangi. Je, kabla ya kukamilisha shughuli hizo Serikali imechukua hatua ya kuweza kuwakaribisha vijana hawa ili waondokane na matatizo hayo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH SOLOMON SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kazi kubwa itakayofanya ni kuwapa elimu kwamba haya mambo kamwe hayakubaliki na kwamba ingekuwa vyema waingie sasa kwenye mipango ya Serikali kutokana na mikakati ambayo itatayarishwa ili walio kwenye hivi vijiwe waondoke ili waje kwenye vijiwe vya uzalishaji mali. Kwa hiyo, mkakati mkubwa ni kutoa elimu. (*Makofi*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Waziri alipokuwa anajibu amesema wamemaliza Dar es Salaam watakwenda Mwanza, Arusha na kama inavyofahamika vijana wako mahali popote hapa Tanzania, ukichukua hata miji midogo kama Iguguno, Ibaga. Sasa huu mkakati utakwenda kwa maeneo yote ambayo vijana wapo, wanataka kufanya kazi ila mitaji hawana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, kazi hii tulianza Dar es Salaam lakini kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti haikuwezekana kuendelea kwa kasi tuliyotegemea kwenye sehemu zingine za nchi. Mwaka huu wafedha 2006/2007 tumeomba shilingi milioni 12,800 na lengo ni kwenda sasa nje ya Dar es Salaam na miji tuliyosema minne, Mji wa Arusha, Mji wa Tanga, Mji wa Mwanza na Mji wa Mbeya ni miji ambayo imefahamika kwamba inakua kwa kasi zaidi ya sehemu zingine ya nchi.

Lakini lengo kuu ni kufikia vijana wote popote walipo nchini. Tunaelewa kwamba siyo tu vijiwe hivi havipo tu mijini lakini pia vipo na vijijini. Kwa hiyo, lengo ni kuanza kwenye zile sehemu ambazo zina vijana wengi, miji inakua kwa kasi zaidi. Halafu baadaye kwa jinsi bajeti itakavyoruhusu kuendelea sehemu zingine za nchi ikiwa ni pamoja na miji midogo ya nchi na vile vile sehemu za vijijini.

Na.169

**Hadhi ya Uwanja wa Ndege Mwanza.**

**MHE. ERNEST G. MABINA (K.n.y. MHE. ESTHER K. NYAWAZWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Mwanza ni Jiji, na kwa kuwa uwanja wa ndege wa Mwanza hauendani na sifa ya Jiji licha ya kwamba inategemewa sana na nchi za Afrika Mashariki na hata dunia nzima kwa usafirishaji wa madini, samaki, pamoja na maliasili na utalii:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya sasa ya kupanua haraka uwanja huu ili uendane na hali ya Jiji la Mwanza?

(b) Kama Serikali haina fedha, kwa nini mkataba usibadilishwe kwa kuyataka makampuni makubwa yanayofanya biashara ya samaki, madini maliasili na utalii yashiriki katika upanuzi na ujenzi wa uwanja huo?

(c) Je, Serikali inaweza kuwaeleza wananchi na wakazi wa Jiji la Mwanza ni lini ujenzi na upanuzi wa uwanja huu utafanyika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Esther Kabali Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kiwanja cha ndege cha Mwanza tayari kina uwezo wa kuchukua ndege kubwa kama vile *Boeng 737,* na kinatumiwa na ndege kubwa za mizigo kwenda bara la Ulaya kupeleka minofu ya samaki toka Ziwa Victoria. Njia ya kurukia na kutua Ndege ni nzima na ina uwezo wa kuhimili ndege kubwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni kukosekana kwa maegesho ya kutosha ya ndege za abiria za ukubwa huo (B373) hasa inapotokea ndege mbili kutua kwa wakati mmoja. Tatizo lingine ni hali mbaya ya maegesho ya ndege za mizigo pamoja na viungio vyake vinavyohitaji ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine kunahitajika kuwa na jengo kubwa la kisasa la abiria, jengo kwa ajili ya matengenezo ya ndege (*Hangar*) na jengo la mizigo.

Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Miundombinu kwa kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege tayari imekamilisha upembuzi yakinifu na kuandaa *Master Plan*, pia imekamilisha usanifu wa miundombinu ya majengo yote muhimu ya kiwanja.

- Kazi ya usanifu wa maegesho na viungio imefanywa kwa gharama ya shilingi milioni 22.8.
- Kazi ya usanifu wa majengo ya kisasa ya jengo la abiria, jengo la mizigo na hanga kwa ajili ya matengenezo ya ndege imefanywa kwa gharama za shilingi milioni 185. *(Makofi)*

- Gharama za ujenzi wa majengo ya abiria, mizigo na miundombinu ya maegesho na viungio yanakadiriwa kuwa dola za Kimarekani milioni 31.0.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoahidi wakati tukijibu hoja mbalimbali wakati wa Bajeti yetu, tunategemea kujenga uwanja huu kwa fedha za *BADEA*, ingawaje *World Bank* pia wameonyesha nia. Wataalam wa *BADEA*, tayari wamewasili nchini na leo hii wanategemewa kwenda Mwanza kwa ajili ya *appraisal* ya uwanja huo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mpango wa ushirikishwaji sekta binafsi kuwekeza katika kiwanja hiki, makampuni kadhaa yameonyesha nia ya kuwekeza katika jengo la mizigo, Hanga, Mfumo wa mafuta ya ndege na Hoteli.

(c) Wizara inategemea kuwa ufumbuzi wa ujenzi wa uwanja huu utapatikana na utekelezaji wa mradi huu kuanza mara tu baada ya kukamilika kwa *appraisal mission* ambayo inaanza leo ya *BADEA* na kukamilika kwa makubaliano na mikataba husika.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyengeza. Kwa kuwa uwanja huu unaonekana kwamba utajengwa kwa fedha tegemezi badala ya fedha za Serikali. Na katika Bajeti inaonyesha kwamba uwanja huu umetengewa shilingi milioni 100 pamoja na uwanja wa Kigoma. Je, Serikali ipo makini kweli kuuendeleza uwanja huu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa najibu hoja yangu kwamba uwanja huu ni kweli unategemea *BADEA,* na wameonyesha nia ya kusaidia katika uwanja huu. Milioni 50 tulizotenga ni kwa ajili ya kuimarisha uzio kama nilivyokuwa ninajibu. Uzio wa uwanja huu lakini shughuli nyingi zote zitafanywa na *BADEA* na wameonyesha nia ya kutusaidia.

Na. 170

**Ukarabati wa Majosho na Mabwawa ya Mifugo**

**MHE. AHMED A. SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM imeweka lengo la kuwawezesha wafugaji ili kuwe na ufugaji wa kisasa utakaowasaidia wafugaji kuboresha maisha yao na kuchangia pato la Taifa, na kwa kuwa, Jimbo la Solwa lenye Kata 16 yapo majosho na mabwawa machache sana na mengine yamechakaa, hayatoi huduma za kukidhi mahitaji ya wafugaji wa maeneo hayo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha kuwa majosho na mabwawa hayo yanatengenezwa ili kukidhi mahitaji ya maji kwa mifugo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, Mkoani Shinyanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba yapo majosho na mabwawa machache katika Jimbo la Solwa na Halmashauri ya Shinyanga Vijijini kwa ujumla na mengine yamechakaa na hivyo kuhitaji ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi na ukarabati wa majosho na malambo na utekelezaji wa miradi mingine ya sekta ya kilimo katika Halmashauri unafanywa kupitia mkakati wa kuendeleza sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Strategy (ASDS)* ambao ulianza kutekelezwa kuanzia mwaka 2001/2002.

Ili kuutekeleza mkakati huo kwa ufanisi, Serikali ilibuni mipango ya maendeleo ya kilimo Wilayani *(District Agricultural Development Plans (DADPs)* ambayo inatekelezwa na Halmashauri zote nchini kuanzia mwaka 2004/2005. *(Makofi)*

Vile vile, mradi wa uwekezaji wa Kilimo Wilayani *(District Agricultural Investment Project (DASIP)* unaotekelezwa katika Mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga, Kagera na Kigoma ambao ulizinduliwa mwaka 2005/2006 nao umebuniwa ili kuwekeza katika Halmashauri na vijiji. Ili kutekeleza kwa ukamilifu mkakati wa *ASDS,* kinachotakiwa sasa ni vijiji na Halmashauri zote kuibua miradi itakayotatua matatizo yanayowakabili wafugaji kwa kuwashirikisha wafugaji wenyewe. Miradi itakayoibuliwa iwe ni pamoja na ukarabati na ujenzi wa majosho kwa ajili ya kuogesha mifugo na mabwawa na malambo yatakayokidhi mahitaji ya maji kwa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia utaratibu wa *DADPs* mwaka 2003/2004 Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini iliomba fedha kwa ajili ya kukarabati majosho mawili (2) kati ya 14 yaliyopo katika Jimbo la Solwa. Jumla ya shilingi milioni 10 zilitolewa na Serikali kwa ajili ya kazi hiyo. Kutokana na vipaumbele vingine, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 na 2005/2006, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini haikuomba fedha kwa ajili ya ukarabati wa majosho badala yake iliomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa malambo, ujenzi wa mabirika ya kunyweshea mifugo, kununulia

wanyamakazi na kuimarisha *SACCOs* za wakulima na wafugaji. Serikali ilitoa jumla ya shilingi 20,669,578 kupitia *DADPs* kwa kazi hizo.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu ya mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Jimbo la Solwa ina idadi ng'ombe zaidi ya 250 (laki mbili na nusu) na mabwawa yaliyopo ni ya zamani, idadi yake ni 15 na kati ya hayo 15 mabwawa matano yamechakaa na hayafanyi kazi. Na majosho yapo 14 na majosho 6 hayafanyi kazi kwa muda mrefu sana. Kata ya Tinde lipo bwawa lakini halifanyi kazi kwa muda zaidi ya miaka saba, katika Kata ya Uswile vile vile.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, uliza swali?

**MHE. AHMED A. SALUM:** Je, Wizara itakubaliana na mimi kwamba kwa sababu gharama hizi si kubwa sana, ifanye utafiti ili iingize kwenye Bajeti hii ya 2006/2007 ili mabwawa hayo yatengenezwe?

Swali la pili, ni mabwawa mangapi mapya na majosho yalitengenezwa katika Jimbo la Solwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi fedha za ukarabati za majosho na malambo ndiyo zitapatikana lakini kupitia kwenye mradi wa *DADPs* ambao katika ngazi ya Wilaya unatekelezwa kupitia *District Agricultural Development Plans.*

Pili, kuhusu suala la malambo na majosho. Halmashauri ya Shinyanga Vijijini na wafugaji wenyewe, kwa utaratibu wa *DASIP* waamue wenyewe wanahitaji majosho na malambo kwenye Kata zipi na mangapi kulingana na idadi ya mifugo. Wizara yangu itakuwa tayari kusaidia kwa utaalam wa Jimbo la Mheshimiwa Ahmed Salum. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mifugo inachangia pato la Taifa kwa asilimia 18 na kwa kuwa magonjwa ya kupe yanazuilika kwa kuogeza mifugo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba iwapo majosho yote nchini yatakuwa yamekarabatiwa na kuogesha mifugo, vifo vingi vya mifugo katika nchi hii vitapungua?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kabisa kwamba tukijitosheleza ndani ya majosho ambayo ni 3,700 tutakuwa na uwezo wa kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe. Hili ndiyo lengo la Wizara la kuhakikisha kuwa tunadhibiti magonjwa yaletwayo na kupe na tunao mkakati wa kuhakikisha kuwa mahitaji ya majosho tumejitosheleza kwa nchi mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wananchi kupitia miradi ya *DADPs* wao wenyewe watusaidie kwa kuamua ni yapi mahitaji yanahitajika sisi Wizara tutatoa utaalam tu.

Na. 171

**Tatizo la Maji nchini**

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Lindi Mjini na Wilaya ya Nachingwea ina matatizo ya maji kwa miaka mingi sasa, lakini sasa tatizo la maji limekuwa ni la nchi nzima na kwa kuwa, miradi ya maji nchini, ile ya wahisani na ile ya Serikali inasuasua:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kulishughulikia tatizo hilo ki-dharura kwa kuipa uwezo kifedha Wizara ya Maji ili iweze kulishughulikia tatizo la maji katika Wilaya ya Lindi na nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miradi ya maji hapa nchini hausuisui kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Utekelezaji wa miradi ya maji hupitia katika hatua mbalimbali ambazo ni uhamasishaji, uchunguzi, usanifu, ujenzi na uendeshaji. Hatua hizi zinachukua muda na utekelezaji wa miradi ya maji kwa kawaida ni wa gharama kubwa. Serikali inatambua kuwepo tatizo la maji katika Wilaya ya Lindi Mjini na Wilaya ya Nachingwea.

Kwa kutambua kuwepo kwa tatizo hilo Serikali inaendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika Vijiji 13 Wilayani Lindi na vijiji vitano Wilayani Nachingwea kwa msaada wa Serikali ya Japan. Aidha, Serikali inaendelea kuipa uwezo wa kifedha Wizara ya Maji ili kushughulikia matatizo ya maji hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza huduma za maji katika Wilaya ya Lindi Mjini na Wilaya ya Nachingwea, Halmashauri ya Lindi Mjini na Wilaya ya

Nachingwea, kila mmoja imeleta Wizarani kwangu miradi ya maji ya vijiji 10 kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Lindi Mjini ni Mkwera, Kitumbikwera, Ndorochini, Mtanda Juu, Migombani, Mituleni, Mitwero, Wailesi, Majengo na Makonde. Wilaya ya Nachingwea vijiji ni:- Mtunguru, Rwege, Kiparamtua, Kitandi, Mkonjela, *Litula, Farm Eight,* Mandai, Chiola, Nakalonji na Lipuyu. *(Makofi)*

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Lakini nilitaka niulize tu kwamba hawa wa Shirika la *JICA* waliahidi tangu mwaka 2000 kujenga visima katika Mkoa huu wa Lindi ikiwemo katika vijiji vya Chinongwe, Litama, Likwachu, Machanganja, Chibula, Lipingo, hadi sasa tangu mwaka 2000 hawajafika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa miradi hii kama nilivyosema awali inachukua muda kwa sababu taratibu nyingi ambazo zinapitiwa humo hadi kufikia mfadhili aanze kuchimba kisima. Lakini hata hivyo wafadhili wa Kijapan tayari wako Mkoa wa Lindi wakiendelea na kazi katika baadhi ya vijiji ambapo sasa hivi miradi tayari imeshazinduliwa na mimi nilikuwa mmoja wapo ambao tulishiriki katika kuzindua. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ya kwamba miradi hiyo yote ambayo nimeitaja na mingine ambayo hakuiongelea hapa bado *JICA* Kampuni ya Kijapan itaishughulikia punde.

**NAIBU SPIKA:** Hotuba ya Wizara ya Maji inakuja karibuni kwa hiyo naendelea na Wizara ya Elimu.

Na. 172

**Ukosefu wa shule na Uhaba wa Walimu**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa kuwa elimu ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania, hii ikiwa ni pamoja na watoto wa Jimbo la Nanyumbu ambapo maeneo kama Mbangala, Mbuyuni, Wanike, Chinyanyira, Nkoromwana, Nambunda na Ngonji hakuna shule na hivyo kuwanyima watoto wa maeneo hayo haki yao ya msingi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule na nyumba za walimu jimboni humo?

(b) Je, ni lini walimu wa kutosha watapatikana katika Wilaya ya Nanyumbu ambako kuna uhaba mkubwa wa walimu wa shule za msingi na sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya mpya ya Nanyumbu ina jumla ya shule za msingi 90 zikiwemo 13 za *Satellite.* Maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge ni Makutano ya Mto Ruvuma na Mbangala yanayokaliwa na Wavuvi na hifadhi ya Mbuga za wanyama *(Selous Game Reserve).*

Idadi ya wakazi wa maeneo hayo ni ndogo, hata hivyo maeneo haya yana shule za msingi na shule za *Satellite.* Eneo la Mbangala-Mbuyuni lina shule ya msingi Marumba na *Satellite* ya Mbangala-Mbuyuni, eneo la Wanike lina shule msingi Namaromba na *Satellite* na Wanike na Nambunda, eneo la Chinyanyira lina shule ya msingi Rukumbi na *Satellite* ya Chinyanyira na eneo la Nkoromwana lina shule ya msingi Kamundi na *Satellite* ya Ndoromwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule katika maeneo hayo ikiongezeka shule za *Satellite* zitakuwa na stahili ya kuwa shule za msingi. Kwa mfano shule ya *Satellite* ya Namijati ambayo shule mama ni shule ya msingi Njisa ipo katika hatua za mwisho kuwa Shule ya msingi. Aidha, katika Wilaya mpya Nanyumbu kuna shule za sekondari Mangaka, Michiga, Nanyumbu na Mikangaula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi na sekondari (MMEM na MMES) inaendelea kuchangia nguvu za wananchi katika ujenzi wa shule na nyumba za walimu katika Wilaya zote nchini ikiwemo Wilaya ya Nanyumbu.

Katika mwaka 2004-2005 Serikali ilipeleka ruzuku ya maendeleo katika jimbo la Nanyumbu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 2 na nyumba moja ya mwalimu katika shule za sekondari Mangaka, Nanyumbu na shule ya sekondari Michiga ilipata fedha kwa ajili ya darasa moja. Katika kipindi hicho hicho kupitia MMEM wilaya ya Nanyumbu ilipelekewa shilingi 55,800,000/= kwa ajili ya vyumba 18 vya madarasa na shilingi 68,400,000/= kwa ajili ya nyumba za walimu. Aidha, shilingi 11,834,000/= zilipelekwa kwa ajili ya vyoo na shilingi 22,050,000/= kwa ajili ya madawati.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuwapanga walimu katika Wilaya zote ikiwemo Wilaya ya Masasi kadri wanavyohitimu mafunzo ya Daraja A na Stashahada. Mwaka 2005 walimu 60 na mwaka 2006 walimu 62 wa Daraja A walipangwa katika Wilaya ya Masasi. Aidha mwezi huu wa Julai, 2006 walimu 8 wa Stashahada walipangwa katika shule za Mangaka (2) Michiga (2) na Nanyumbu (4). Tunaomba Halmashauri na wananchi kwa ujumla kuendelea kuweka mazingira mazuri hasa ujenzi wa nyumba na kujitahidi kuondoa kero za walimu katika maeneo yao ya kazi ili kuwawezesha walimu kufanya kazi zao kikamilifu.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa walimu wanaopangwa au wanaopelekwa wengi wao huwa hawaendi kwa sababu ya mazingira magumu. Je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuwalipa posho ya mazingira magumu walimu wanaopelekwa Wilayani Nanyumbu, Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Lindi kwa ujumla?

Swali la pili, je, Serikali inahakikishaje kwamba walimu wanaopelekwa kule wanafika na ni hatua gani kwa wale ambao hawafiki vituoni mwao wanachukuliwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba ni kweli baadhi ya walimu wanasuasua kwenda kwa ajili ya mazingira magumu. Na hilo tumeliona, Serikali inatambua, Serikali imeshaahidi kulifanyia kazi na pale itakapokuwa tayari posho ya aina hiyo au huduma yoyote kwa ajili ya watumishi wote ikiwa ni pamoja na walimu itatolewa kwa mujibu wa taratibu na kanuni zitakazokubalika. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, swali (b) namwomba Mheshimiwa Waziri wangu alijibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nijibu swali la pili. Walimu wanapopangwa kwenye maeneo yao ya kazi kwanza kabla hawajafika ni kwamba hata mkataba hatunao. Kwa hiyo, wasipofika kwenye maeneo yao ya kazi hata kuwachukulia hatua si rahisi kwa sababu wanapoanza kazi huwa tunajaza mkataba yaani tunafunga nao mkataba. Kwa hiyo, unaweza ukamchukulia hatua. Lakini hata kabla hajafika kazini si rahisi kumchukulia hatua.

Tunachoweza kukifanya ni kile tu ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia kwa kweli ni kujitahidi sisi wote kwa kushirikiana na Serikali kuweka mazingira mazuri kule ambako walimu wanafika na hasa nyumba za walimu ndiyo kitu kikubwa sana katika kuwawezesha kukaa katika sehemu za kazi. *(Makofi)*

Na sasa hivi tuseme ule ukweli. Sasa hivi wenzetu wadau wenzetu yaani shule ambazo si shule za Serikali zimekuwa nyingi sana. Kwa hiyo, pale anaposuasua kama alivyosema Naibu Waziri wanawachukua, wanawapa kazi.

Lakini mimi ningependa kutoa wito kwa hao hao walimu wanaosuasua ni vizuri wakafika hii ni nchi yao waijenge, wakafanye kazi wakati Serikali na wananchi kwa ujumla tunajitahidi kuwawekea mazingira mazuri. Na ningependa kurudia hata lile jibu la msingi ni kwamba ili hawa walimu wafike kule lakini kweli Serikali bado inafanyia kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi kuona ni jinsi gani ambavyo tutawasaidia walimu hao wanaokwenda kufanya kazi katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Lakini ni sisi tuliomo humu humu kwa kushirikiana na wananchi tunaweza tukajenga shule, tutajenga nyumba za walimu, tukawaweka kwenye mazingira mazuri. Na ningependa nimpongeze Mheshimiwa Mzindakaya sijui leo yumo humu. Alitutajia hapa kwamba wameweka mkakati wa jinsi ya kupokea walimu katika maeneo yao. Naomba tuwapongeze na wengine naomba tufanye hivyo hivyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 173

**Tatizo la Rushwa – *TRA***

**MHE. KILONTSI M.M. MPOROGOMYI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania inatekeleza mkakati wa kuzuia rushwa, na kwa kuwa Mamlaka hiyo inatekeleza mpango wake wa kuimarisha utawala bora pamoja na uwajibikaji wa viongozi katika maswala ya utendaji na uadilifu.

(a) Je, ni matatizo gani yanaizuia *TRA* kumaliza tatizo la rushwa katika shirika hilo?

(b) Je, ni wafanyakazi wangapi wamekwishapatikana na hatia ya rushwa na ni hatua gani zimechukuliwa dhidi yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo yanayokwamisha juhudi za mamlaka kutekeleza mkakati wa kuzuia rushwa kikamilifu. Tatizo la msingi ni kukosekana kwa taarifa kutoka kwa wadau mara tu wanapoombwa rushwa. Mara nyingi taarifa zinazopokelewa na mamlaka ni simulizi za yaliyopita ambapo kitendo chenyewe kinadaiwa kuwa kimeshatendeka.

Kama inavyoeleweka rushwa ni tendo linalofanyika kwa siri kati ya mtoaji na mpokeaji, wengi kati ya watoaji rushwa katika eneo la kodi ni wale wenye nia ya kukwepa kodi, hivyo kwa kiasi kikubwa nao hunufaika. Watu wa aina hii hawako tayari kushirikiana na Mamlaka na vyombo vingine vya dola kuwanasa watumishi husika. Hata wale wanaotoa taarifa za matatizo ya rushwa, hawatoi ushahidi wa kutosha kuwezesha kumtia hatiani mhusika.

Aidha, tungependa kuwaomba wadau wote washirikiane na Serikali kutokameza tatizo la rushwa ndani ya mamlaka kwa kutoa ushirikiano kwa mamlaka na vyombo vingine vya dola kama TAKURU na Polisi kwa kutoa taarifa mapema mara tu wanapoombwa rushwa na watumishi wa Mamlaka ili waweze kunaswa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo hayo mamlaka kwa kiasi kikubwa imefanikiwa kupunguza tatizo la malalamiko ya wadau dhidi ya watumishi wake yakiwemo yale ya rushwa.

Katika kipindi cha mwaka 2003 yalipolekewa malalamiko 79 kutoka kwa wadau ikilinganishwa na malalamiko 31 yaliyopokelewa mwaka 2005. Aidha tunaamini kwamba mkakati mpya mamlalaka wa kuzuia rushwa wa mwaka 2006 hadi mpaka 2010 ambao Serikali umeupitia na kuupitisha utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza rushwa na kuitokomeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile rushwa ni jambo la siri na upelelezi wake unahitaji utalaam wa hali ya juu, mamlaka imekuwa ikifanya uchuguzi wa awali na pale inapoonekana kuna viashiria vya rushwa, kesi hizo upelekwa TAKURU kwa uchunguzi wa kina, kuanzia mwaka 2003 mamlaka imepeleka TAKURU jumla ya kesi nane, kati ya hizo tatu nusu zilikamilika, na madai hayakuweza kuthibitishwa, na kesi tano zilizobakia bado uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati za Maadili za mamlaka zimekuwa zikiratibu upokeaji wa malalamiko dhidi ya watumishi wake na kupitia taarifa za uchunguzi na hatimaye hutoa ushauri kwa idara husika, juu ya hatua za kinidhamu zinazostahili kuchukuliwa dhidi ya watumishi husika.

Hadi hivi sasa hakuna mtumishi wa mamlaka aliyepatikana na hatia ya rushwa mahakamani, lakini wapo walionekana kuwa na uadilifu ulio na mashaka yaani *doubtful integrity* na hatua za kinidhamu zilichukuliwa dhidi yao. Katika kipindi cha mwaka 2003 hadi mwaka 2005, watumishi 71 wa Mamlaka walisimamishwa kazi na kati ya hao 18 walifukuzwa kazi kwa makosa mbalimbali ya kimaadili. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri labda niseme hivi kwamba ninayo maswali ya nyongeza na napenda niulize kama ifuatavyo:

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu aliyoyatoa anafikiri ufanisi tulionao ndani ya *TRA* unatosha? Na kama anafikiri unatosha na amekubali kwamba rushwa ipo, tufanye nini ili tuongeze ufanisi wa jambo hili? Kama jibu ni ndiyo, ufanisi haupo. Je, kodi inayokusanywa hivi sasa inatosha? Kama jibu ni hapana, anawaambia nini umma wa Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, Maswali yamekuwa matatu yanatosha. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, angalia Bajeti ya Serikali kuhusu mapato, kuanzia ukurasa 28 mpaka ukurasa 33 tumeeleza kwa ufanisi kabisa kwamba mikakati kamili juu ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hapo, tumeeleza kuwa tutafanya hili na hili, yako mambo saba pale. Angalia hapo Mheshimiwa Mporogomyi, Mheshimiwa Mbunge, utaona kwamba hayo uliyoyauliza yote yanajibiwa katika *Budget Speech* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongeza majibu kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo waliyonayo *TRA*, bado wanafanya kazi nzuri sana. Mapato ya mwezi uliopita yamefikia bilioni 226. Kwa niaba ya Serikali napenda kuwapongeza watumishi wa *TRA*, na kuwaambia kwamba waendelee na jitihada hizi maana wanafanya kazi nzuri tunazojithamini. *(Makofi)*

Na. 174

**Uvunaji Holela wa Misitu**

**MHE. MBARUKU K. MWANDORO (K.n.y. MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH)** aliuliza:-

Kwa kuwa, hofu ya kuwa Misitu yetu mingi imekatwa kiholela haibishaniwi, hii ikiwa inathibitishwa na hali ya usafirishaji wa magunia ya mkaa toka mikoani kuja Dar es Salaam na baadhi ya miji mikubwa ya mikoa yetu; na kwa kuwa, kwa tathimini ya haraka siyo kweli kwamba mkaa unatumiwa hapa nchini tu, kutokana na ukweli kwamba wananchi wengi hawana uwezo wa kununua gunia la mkaa kwa matumizi ya nyumbani.

(a) Je, Serikli itakubaliana na mimi kuwa mkaa wetu unasafirishwa kwenda nchi za nje kama Ulaya, Mashariki ya Kati na nchi jirani katika visiwa vya Bahari ya Hindi isipokuwa visiwa vya Zanzibar?

(b) Je, Serikali itapata faida na hasara gani kama ikipiga marufuku suala la uvunaji misitu kwa muda kadhaa ili kutoa nafasi ya upandaji na ukuaji wa miti?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, licha ya kutoa leseni za uvunaji kwa ajili ya wananchi kupata mazao ya misitu kama vile mkaa, mbao na nguzo, imepiga marufuku kusafirisha mkaa nje ya nchi. Hata hivyo zipo habari kuwa mkaa unasafirishwa nje ya nchi kwa njia za kutorosha, kwa jina jingine njia za panya. Kutokana na doria inayofanywa na Wizara yangu kwa kushirikiana na polisi baadhi ya majahazi yanayohusika huwa yanakamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawaje wizi huo unachangia kwa kiasi kikubwa katika ukataji holela wa miti nchini, Wizara yangu haijaamua kupiga marufuku kabisa uvunaji wa misitu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa wananchi wanaitegemea sana misitu katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Kwa mfano, asilimia 92 ya watanzania wanatumia nishati inayotokana na kuni au mkaa kwa shughuli zao za kila siku.

Badala ya kusimamisha kabisa ukataji miti Wizara yangu imeamua kudhibiti matumizi ya misitu yetu ili maliasili hii itumike kiendelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti zaidi uvunaji holela wa misitu Wizara yangu imeandaa Mwongozo kupitia tangazo namba 69 na 70 la mwezi Juni, 2006 wa kuvuna, kusafirisha na kufanya biashara ya mazao ya misitu. Kwa mfano sasa vibali vya uvunaji vitakuwa vinatolewa na Kamati za Wilaya ambazo zitawajumuisha wajumbe wa vijiji vilivyoko karibu na msitu unaovunwa. Pia wavunaji watatakiwa kupanda miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itapata faida zifuatazo kama itapiga marufuku suala la uvunaji wa misitu kwa muda kadhaa:-

- Kutoa nafasi kwa miti kukua na hali ya misitu kuwa bora zaidi.
- Kutoa nafasi ya kufanya tathmini ya kiasi cha mazao ya misitu yaani *Inventory*.
- Kutoa nafasi kwa Serikali na jamii kwa ujumla kuibua nishati mbadala na vifaa mbadala vya ujenzi na matengenezo ya samani
- Kubwa kuliko yote ni kuinusuru nchi yetu kugeuka kuwa jangwa.

Mheshimiwa Spika, hasara itakayopatikana kama Serikali itapiga marufuku suala la uvunaji misitu kwa muda kadhaa ni kama ifuatavyo:-

- Kupanda bei kwa malighafi zitokana na rasilimali za misitu.
- Serikali itakosa mapato ambayo ingetokana na miti iliyokomaa na ambayo ingevunwa wakati wa usitishaji wa uvunaji.

Pamoja na hasara nilizozieleza hatuwezi kuzilinganisha na faida nilizozitaja awali. *(Makofi)*

Na. 175

**Mapato Yatokanayo na Leseni za Uvuvi**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja ya njia za mapato ya Serikali kutoka Maliasili ni kutokana na kuuza leseni za uvuvi:-

(a) Je, kuna meli ngapi za uvuvi nchini hivi sasa ambazo zimepewa leseni rasmi na Serikali?

(b) Je, ni mapato kiasi gani yamepatikana kwa njia hiyo ya leseni kuanzia mwaka 2003 hadi 2005?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa Mbunge wa Gando, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa na HAZINA mwaka 1998, Serikali imeelekeza mamlaka zitakazohusika na utoaji wa leseni za uvuvi pamoja na kupokea ada za leseni zitakazotolewa. Kwa mujibu wa mwongozo huo leseni za uvuvi nchini hutolewa na mamlaka mbili zifuatazo:-

- Halmashauri za Wilaya hutoa leseni kwa vyombo vya uvuvi vyenye urefu usiozidi mita 11 na ushuru unaokusanywa ni mapato ya wilaya husika.
- Serikali Kuu hutoa leseni za meli zenye urefu unaozidi mita 11;

Katika kipindi cha mwaka 2006, hadi mwezi Juni, 2006 Serikali Kuu ilitoa leseni kumi na tatu (13) za uvuvi wa kamba ambao hufanyika katika Maji ya Ndani (*Territorial Waters*) na leseni 42 za uvuvi kwenye Ukanda wa uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone (EEZ).* Hata hivyo takwimu halisi za leseni zinazotolewa na Halmashauri za Wilaya zinatunzwa na wilaya husika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2003 hadi 2005 Serikali Kuu ilitoa leseni 80 za uvuvi wa kamba na leseni 208 za uvuvi wa samaki aina ya Jodari. Serikali ilikusanya shilingi 153,931,989.80 kutokana na ada za leseni 80 za vyombo vilivyovua katika maji ya ndani, na Dola za Kimarekani 3,202,100 kutokana na ada za leseni 208 za kuvua samaki aina ya Jodari kutoka bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye kipengele (a) hapo juu, takwimu za mapato yatokayo na leseni za uvuvi hutuzwa na Halmashauri husika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha, na muda wa maswali umeisha pia. Nina matangazo machache, kwanza kuhusu vikao, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM, anaomba niwatangazie Wabunge, Wabunge wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Wabunge wa CCM. Kwamba kutakuwa na kikao leo tarehe 10 Julai, 2006 saa sita mchana katika ukumbi Na. 118, kwa Mheshimiwa Spika, ghorofa ya kwanza. Mkutano wa Kamati ya Uongozi ya CCM, chumba Na. 118. *(Makofi)*

Kikao cha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala leo tarehe 10 Julai, 2006 wanaomba wajumbe wake wakusanyike kwenye ukumbi Na. 231 gorofa ya pili, jengo la utawala, saa nne na nusu, chumba 231 saa nne na nusu. Taarifa ya kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama, wao pia watakuwa na kikao leo chumba Na. 219 mara baada ya kipindi hiki cha mswali, na ndio hiyo mikutano mitano iliyotangazwa.

Pia naomba niwatangazie kwamba tunapoingia Kamati ya Matumizi, naomba tusikilizane hapo tunapoingia Kamati ya Matumizi. Kumekuwa na tabia ikifika tu Kamati ya Matumizi kifungu cha mshahara wa Waziri wote wanasimama kuhusu mshahara wa Waziri, Mshahara wa Waziri ni mahali pa kujadiliana *policy issues*, sio mambo ya *operations* ama utekelezaji tu, wote wanasimama hapo.

Sasa sisi tutakuwa tunakataa sasa, hiyo inaonyesha kwamba hatufanyi wajibu wetu, kama tungekuwa tunafanya wajibu wetu, tutafute *vote* 49 kwa mfano, kuna kifungu 1001 *Administration General* sasa yale ni mambo ya kiutawala, *policy* kiutawala, lakini ukitaka mambo ya *accounts* kuna kifungu kinachofuata, ukitaka kwenye utawala mambo ya *policy* na *planning* kuna kifungu kingine.

Ukitaka mambo ya *water resources and assessment and exploration* ipo kifungu, sasa anakuja *exploration* mshahara wa Waziri, sasa Waziri sio *explorer* yeye ukitaka *central stores* kipo kifungu hiyo nimezungumzia *supply vote*, ukitaka *water laboratory* ipo, ukitaka *urban water supply and sewages* ipo, ukitaka *rural water supply* ipo, ukitaka *water resources institute* ipo, ukitaka *drilling* ipo.

Hapo tunazungumzia *supply vote*, tukija kwenye *development* sasa, pia kuna vifungu ambavyo vinahusiana na *policy and planning* kwenye *development*, na mnafahamu maana ya *development* kwamba ni miradi mipya *supply vote* ni matumizi ya kawaida ya Wizara mwaka ule. Kuna kifungu kama hawa tutakaoingia sasa hivi kuna kifungu cha *Livestock Research and Training Institute* kuna kifungu hapo, kuna *water resources assessment and exploration* kuna *water laboratories* kwenye *development*. *(Makofi)*

Sasa nimeyasema haya kusudi wale watakaotaka kuzungumza kesho wakati wa Kamati ya Matumizi tuzingatie hayo, tusiwe *too general* inakuwa tena kama tunaanzisha kama *debate* nyingine halafu haiwi *relevant*. Hiyo tulikuwa tunatumia kwa kukiuka. Kwa hiyo naomba sana wale watakaopenda kuingia kwenye *Committee of Supplies*, waji *focus* kwenye vifungu vinavyohusika.

Kama utakuwa huko huko basi watakuambia kifungu hicho sio chenyewe, kwa hiyo sio mshahara wa Waziri, kila mtu mshahara wa Waziri kuna mambo ya mshahara wa Waziri. Waheshimiwa naomba muende mkasome kanuni halafu mkafuatilie vile vitabu vyetu vile vitakueleza vizuri, na ukiuliza kwenye kifungu kinachohusika *attention* yote itapewa pale. Kwa hiyo, naomba hiyo tumeieleza hivyo kwa sababu kumetokea kama tunazungumza kila kitu sehemu isiyohusika.

Waheshimiwa Wabunge, mtatambua kwamba tulikuwa na wageni wengi tu waliohudhuria kikao hiki, kwa mfano tuna mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mkoa wa Shinyanga, tuna madiwani wa kutoka wilaya ya Chunya na tuna wageni wengi sana. Kwa hiyo, karibuni wote.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia kifungu Na. 55 (3) naomba kupata mwongozo kidogo wa kiti chako.

**NAIBU SPIKA:** Kifungu 55 ngapi?

**MHE. HAROUB SAID MASOUD**: Ndiyo Kifungu 55(3) ukurasa namba 38.

**NAIBU SPIKA:** Naomba usome.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema hivyo ili tuweze kuweka *hansard* zetu sawa. Ulipokuwa unaita lijibiwe swali la Wizara ya Kazi, na ndivyo ilivyoandikwa, iliandikwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, nilimwona Mheshimiwa anayehusika na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo alikunja uso kidogo, kwa sababu michezo imetolewa katika Wizara yake.

Ili kuweka *hansard* sawa, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, na kama ni ndio sahihi hivyo naomba kumbukumbu hizo ziwekwe sawa ili mwenyewe Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, awe mpole sasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge ni kweli na hilo limetambulika, bahati tu hatukutangaza, lakini tulitambua kutokana na ushauri tuliopewa kutoka kwenye meza, hilo ni sahihi.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007
### Wizara ya Maji

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Maji, naomba kutoa Hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2006/2007

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ikiwa ni ya kwanza baada ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi na shukrani kama ifuatavyo:- Kwanza, nampongeza kwa dhati kabisa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhati kabisa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwa asilimia 80.28 kuwa Rais na Makamu wa Rais. Ushindi huo mkubwa ni ishara ya imani ya wananchi waliyonayo kwa Rais na kwa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Aidha, nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi huo mkubwa, siyo tu katika uchaguzi wa Rais, bali pia kwa uchaguzi wa Wabunge na Madiwani. Aidha, nampongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura karibu zote kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa aliyekuwa Waziri aliyesimamia sekta ya maji kabla yangu, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge hili kuwa Waziri Mkuu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Anthony Diallo, aliyekuwa Naibu Waziri aliyesimamia sekta ya maji, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Kuteuliwa kwa wenzetu hawa ni ushahidi kwamba walifanya kazi nzuri katika sekta hiyo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na hivyo Mheshimiwa Rais akawateua kwa imani iliyotokana na uchapaji kazi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uniruhusu pia nitoe pongezi kwa Wabunge wenzangu kwa ushindi wa kishindo katika majimbo yao. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Spika kwa kuchaguliwa kwenu kwa kura nyingi kuliongoza Bunge hili la Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila, nisipotoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo la Bunda, kwa kunipigia kura nyingi wakati wa uteuzi na kwa wananchi wa Jimbo la Bunda kwa kunichagua bila kupingwa kuwa Mbunge wao. Ingawa wananchi walishawahi kunichagua mara kadhaa huko nyuma, uamuzi wao wa kunichagua tena bila kupingwa ni deni kubwa kwangu, na ninawaahidi kuwatumikia kwa Ari Mpya, na Nguvu Mpya kadri ya uwezo wangu wote.

Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu kwa kuniteua kuwa Waziri wa Wizara hii nyeti ya Maji. Nitajitahidi kwa nguvu zangu zote kulitumikia Taifa letu kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia, kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Sekta ya Kilimo na Ardhi, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mbunge wa Jimbo la Ileje, kwa ushauri, maoni na mapendekezo yaliyowezesha kuboresha Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2006/2007. Tunaiahidi Kamati hiyo kwamba tutazingatia ushauri, maoni na mapendekezo waliyotoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo napenda pia kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri wote waliotangulia kuwasilisha hoja zao hususan, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mbunge wa Jimbo la Ulanga Magharibi, Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia Meghji, Mbunge wa Kuteuliwa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa Sera za jumla za uchumi, fedha na utendaji wa Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi na shukrani, sasa nizungumzie masuala yahusuyo Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji iliundwa ili kushughulikia maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kusimamia na kutekeleza Sera ya Maji ya Taifa ya Mwaka 2002 na ina majukumu yafuatayo:-

(a) Utunzaji na usimamizi wa raslimali za maji;
(b) Usimamizi na utoaji wa huduma ya maji vijijini;
(c) Usimamizi na utoaji wa huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka mjini; na
(d) Utoaji wa mafunzo katika sekta ya maji.

Aidha, vyombo vinavyosimamiwa na Wizara katika kutekeleza majukumu hayo ni vifuatavyo:

(a) Bodi za maji na ofisi za maji katika mabonde tisa (9) ya maji yaliyopo nchini;
(b) Mamlaka za maji katika miji mikuu ya Mikoa, Wilaya na miji midogo;
(c) Jumuiya za Watumiaji maji vijijini;
(d) Wakala wa uchimbaji visima na ujenzi wa mabwabwa *(DDCA);*
(e) Bohari Kuu ya maji;
(f) Chuo cha maji cha Rwegalulira;

(g) Maabara za maji;
(h) *DAWASA/DAWASCO;* na
(i) Mamlaka ya kusimamia utoaji wa huduma za maji, umeme na bidhaa zitokanazo na petroli *(EWURA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo na baada ya kuainisha majukumu ya Wizara yangu, hotuba yangu itazungumza maeneo makuu saba yafuatayo:-

(a) Uenezaji na Utekelezaji wa Sera ya Maji;
(b) Hali halisi ya Sekta ya Maji;
(c) Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu pamoja na Mipango ya Maendeleo iliyoidhinishwa katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 na Mipango, Majukumu na Malengo ya mwaka 2006/2007;
(d) Mafunzo katika Sekta ya Maji;
(e) Masuala ya Jumla ya Sekta ya Maji;
(f) Shukrani; na
(g) Maombi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uenezaji na Utekelezaji wa Sera ya Maji, mwanzoni mwa mwaka 2002, iliyokuwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifungo ilikamilisha maandalizi ya Sera mpya ya maji ya Taifa (*National Water Policy (NAWAPO*, 2002). Sera hiyo ambayo ilipitishwa rasmi na Serikali mwezi Julai, 2002 pamoja na mambo mengine ilizingatia sera, mikakati na programu zenye uhusiano na sekta ya maji kama ifuatavyo:-

(a) Sera na Programu nyingine za ki-sekta kama vile afya, nishati na kilimo;
(b) Sera na Programu za ki-Taifa (*Development Vision* 2025, MKUKUTA);
(c) Mikakati na programu za kikanda kama vile *SADC,* Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki; na
(d) Programu za kimataifa kama vile malengo ya milenia *MDGs*.

Katika jitihada za kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Maji ya Taifa ya Mwaka 2002, Wizara yangu inaendelea kusambaza Sera hiyo na kuelimisha wadau wa sekta ya maji kwa kutumia makala pamoja na kuendesha warsha, kongamano, semina, mikutano ya hadhara na kwa kupitia vipindi vya redio na luninga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002 inatekelezwa kikamilifu, Wizara yangu, ilianza mchakato wa kuandaa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Maji (*National Water Sector Development Strategy (NWSDS*) mwezi Desemba, 2003 kwa kuunda Kamati maalum iliyohusisha wajumbe kutoka Wizara ya Maji, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Mkakati huo ambao maandalizi yake yamekamilika na ambao unangoja kuidhinishwa na Serikali unalenga kutekeleza mambo makuu manne yafuatayo:-

(a) Kuainisha majukumu ya kila mdau, ikiwa ni pamoja na Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, jamaii na sekta binafsi na kurekebisha muundo wa kitaasisi ambao unakidhi mabadiliko ya kisera yaliyopo.

(b) Kurekebisha Sheria ili ikidhi malengo ya Sera.

(c) Kuanisha viwango vya uwekezaji unaohitajika kukidhi malengo ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu.

(d) Kuboresha utoaji wa huduma katika sekta ya maji nchini, kwa kuimarisha taasisi na vyombo vinavyotoa huduma katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na Serikali Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kuongeza viwango vya ujuzi na taaluma ya watendaji, na kwa kuongeza idadi ya watendaji, nyezo na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Sera ya Maji ya Taifa na Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Maji ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo itaainisha maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa raslimali za mji ili ziweze kuchangia kikamilifu katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Programu hiyo itakuwa ndiyo mwongozo utakaotumiwa na Serikali kwa ajili ya kutafuta fedha za utekelezaji kutoka vyanzo mbalimbali. Upatikanaji wa fedha za kutosha katika kutekeleza programu hiyo ni nyenzo muhimu itakayoharakisha kasi ya utekelezaji kulingana na malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 pamoja na yale ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002 unasimamiwa kikamilifu, Wizara yangu, imeipitia Sheria ya Maji yaani *Water Utilization* (*Control and Regulation*) *Act. No.* 42 *of* 1974 na Marekebisho yake. Mapitio hayo yamelenga katika kuoanisha Sheria ya Maji na Sheria za sekta nyingine zikiwemo za afya, kilimo, mazingira, maliasili na nishati ili kuondoa migongano wa kisheria iliyopo na inayoweza kutokea wakati wa utekelezaji. Kutokana na mapitio hayo, Wizara yangu, inakusudia kuwa na sheria mbili za maji, yaani Sheria ya Utoaji wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Act*, 2006) na Sheria ya Raslimali za Maji (*Water Resources Act*, 2006). Miswada ya Sheria hizo inatarajiwa kuwasilishwa Bungeni mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inakusudia kuanzisha Mfuko wa Maji wa Taifa (*The National Water Fund*), chini ya Sheria zinazokusudia kutungwa. Lengo la kuanzishwa na uendelezaji wa raslimali za maji na utoaji wa huduma za maji nchini na utaendeshwa kama ilivyo kwa Mfuko wa Taifa wa Barabara. Mfuko utatunishwa na fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(a) Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuanzisha mfuko huo;

(b) Ada na ushuru utakaotozwa na Mamlaka zilizopo kisheria za kusimamia utunzanji na matumizi ya raslimali za maji;

(c) Msaada au ruzuku kutoka Mashariki ya ndani na nje na Serikali zinazoshirikiana na Serikali yetu katika kuleta maendeleo; na

(d) Ushuru au ada nyingine zitakazolipwa kwenye Mfuko kutokana na utekelezaji wa Sheria nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali Halisi ya Sekta ya Maji, Raslimali za Maji, nchi yetu imebahatika kuwa na raslimali kubwa ya maji baridi ingawa haipatikani kwa uwiano ulio sawa katika maeneo yote. Hekta milioni 5.5 kati ya eneo lote la Tanzania la hekta milioni 94 zimefunikwa na maji yakiwemo maziwa makuu ya Victoria, Nyasa na Tanganyika. Aidha, Tanzania inayo mito mingi ikiwemo Rufiji, Kilombero, Ruvuma, Ruhuhu, Malagarasi, Pangani na Kagera. Pamoja na hali hiyo, yapo matatizo yanayochangia upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo. Matatizo ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Ukame unaotokana na mabadiliko ya hali ya hewa;
(b) Uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa vyanzo vya maji; na
(c) Uwezekaji mdogo katika uvunaji na usambazji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani, nchi yetu imeendelea kuwa na upungufu wa mvua kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2001 na hivyo kusababisha upungufu wa maji katika vyanzo mbalimbali. Japokuwa mwaka huu mvua za masika za kutosha zilinyesha katika ukanda wa pwani na Nyanda za juu Kaskazini Mashariki, maeneo mengine ya Nyanda za Juu Kusini na maeneo ya katikati ya nchi yetu mvua zilinyesha kidogo na hivyo kuathiri wingi wa maji kwenye vyanzo mbalimbali hususan, katika mabwawa ya kuzalisha umeme katika maeneo hayo.

Mathalan, kina cha maji katika bwawa la Mtera kiliendelea kupungua kutoka wastani wa mita 692.9 mwaka 2000 hadi kufikia kina cha mita 687.35 mwezi Februari mwaka 2006 ikiwa ni chini ya kina mita 690 kutoka usawa wa bahari, kinachoruhusiwa kuzalisha umeme. Kufuatia mvua zilizonyesha, kina cha maji kwenye bwawa la Mtera kiliongezeka hadi kufikia mita 689.09 mwezi Aprili, mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na matatizo yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo kwa kiwango kikubwa yanaathiri upatikanaji wa maji kwa matumizi ya kiuchumi na kijamii, Wizara yangu inatekeleza mipango ifuatayo:-

(a) Kuziongezea uwezo Ofisi na Bodi za Maji za Mabonde ili kusimamia na kuendeleza raslimali za maji;

(b) Kushirikisha wananchi na wadau wengine katika kuendeleza na kusimamia matumizi ya raslimali za maji;

(c) Kushirikiana na Serikali za Mitaa katika kulinda vyanzo vya maji kwa kutunga na kusimamia sheria ndogo;

(d) Kuhakiki vyanzo vya maji ili kutathmini kiwango cha uchafuzi; na

(e) Kujenga miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vikubwa na vya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Maji, upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa vijijini umeongezeka kutoka asilimia 53.5 mwaka 2004/2005 hadi asilimia 53.7, mwaka 2005/2006, sawa na ongezeko la asilimia 0.2. Aidha, upatikanaji wa huduma ya majisafi mijini katika Makao Makuu ya Mikoa, umeongezeka kutoka asilimia 73 mwaka 2004/2005 hadi kufikia asilimia 74 mwaka 2005/2006, sawa na ongezeko la asilimia 1. Ongezeko la huduma kwa viwango hivyo ni kidogo ikilinganishwa na malengo ya MKUKUTA na yale ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, ambapo ni kufikia asilimia 65 kwa maeneo ya vijijini na asilimia 90 mijini ifikapo mwaka 2010 kwa ongezeko la wastani wa asilimia 2 vijijini na asilimia 3.2 mijini kwa mwaka. Sababu kubwa za kutofikia malengo hayo ni pamoja na ukame uliosababisha kukauka au kupungua kwa vyanzo vya maji na uwekezaji mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mipango wa Mwaka 2005/2006 na Malengo ya Mwaka 2006/2007, baada ya kutoa maelezo mafupi ya hali halisi ya Sekta ya Maji, naomba sasa nitoe maelezo ya utekelezaji wa mwaka 2005/2006 na Mpango na Bajeti ya mwaka 2006/2007 ya Wizara yangu ambayo imezingatia malengo ya MKUKUTA pamoja na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya majumu ya msingi ya Wizara yangu ni kuchunguza na kutathimini wingi na ubora wa maji juu na chini ya ardhi ili kubaini na kufuatilia mwenendo wa raslimali hiyo kwa ajili ya maendeleo ya sekta mbalimbali. Takwimu na taarifa kutokana na uchunguzi na tathimini hiyo huchambuliwa ili kuiwezesha Serikali kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya majanga mbalimbali pamoja na kubuni na kusanifu miradi ya maji. Katika jitihada za kupata takwimu na taarifa sahihi za mwenendo wa raslimali za maji, Wizara yangu imeendelea kuboresha na kusimamia mtandao wa vituo vya kukusanyia takwimu za wingi wa maji kwenye mito, maziwa na mabwawa; vituo vya hali ya hewa; vituo vya kupimia kiasi cha sasa mtandao huo una jumla ya vituo vya 360 vya kupimia wingi wa maji kwenye mito, maziwa na mabwawa vito 98 vya hali ya hewa, 267 vya kupima kiasi cha mvua na 43 vya kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi. Wizara yangu katika mwaka 2005/2006 ilikarabatiwa vituo 59 vya kufuatilia mwenendo wa maji kwenye mito kaitika mabonde ya Rufiji (36), Wami/Ruvu (3), Rukwa (1) na Ziwa Nyasa (5). Vilevile, vituo vya hali ya hewa vilifanyiwa matengenezo katika mabonde ya Ziwa Tanganyika (1) na Ziwa Nyasa (1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mtandao wa vituo vya kukusanya takwimu na taarifa mbalimbali za raslimali za maji. Jumla ya shilingi milioni 640.145 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kiufundi ili kuimarisha na kupanua mtandao wa kufuatilia wingi na ubora wa raslimali za

mjia juu ya ardhi katika mabonde 6 ya maji ya Mto Ruvuma, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, na Bonde la Kati ambapo vituo 126 vya kupima wingi wa maji, 32 vya hali hewa na 87 vya kupima kiasi cha mvua vitakarabatiwa. Pia, vituo 18 vya kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi vitajengwa katika Mabonde ya Ziwa Victoria (8), na Mto Ruvuma (10). Aidha, Wizara yangu kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam imetenga shilingi milioni 750 kukarabati vituo 29 vya kufuatilia mwenendo wa maji juu ya viuo 6 vya hali ya hewa katika Bonde la Mto Wami/Ruvu. Inakadiriwa kuwa kiasi cha maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu na kinachopatikana kwa sasa hapa nchini ni kilomita za ujaza 89, sawa na mita za ujazo 2,700 kwa mtu kwa mwaka. Kufuatia ongezeko la watu nchini linalokadiriwa kufikia milioni 59.8 ifikapo mwaka 2025, kiasi hiki cha upatikanaji wa maji kwa mtu kwa mwaka kitapungua kwa asilimia 45 na kufikia mita za ujazo 1,500 chini ya mita za ujazo 1,700 ambacho ndicho wastani wa chini wa kiwango kinachohitajika. Hali hii inaashiria uhaba mkubwa wa maji katika siku zijazo. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara yangu, inaendelea na jitihada za kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia, kuendeleza na kugawa maji yaliyopo kulingana na mahitaji ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Wizara yangu katika mwaka 2005/2006, imeunda bodi za Maji za mabonde ya Ziwa Tanganyika na Mto Ruvuma na hivyo kukamilisha uundwaji wa Bodi za Mabonde yote tisa ya maji nchini. Bodi za mabonde ya maji zimepewa uwezo kisheria wa kutoa hati za kutumia maji ambapo kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 jumla ya hati 235 zimetolewa. Utoaji wa hati hizo ni sehemu ya juhudi za kudhibiti matumizi holela ya maji katika vyanzo mbalimbali kwa lengo la kutunza raslimali hiyo. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu, itaendelea kuziimarisha Ofisi za Mabonde kwa kuzipatia watalaam, vyenzo na vitendea kazi. Aidha, Wizara itajenga ofisi mpya ya Bonde la Ziwa Nyasa katika Mji wa Tukuyu na kukamilisha ukarabati wa Ofisi za Mabonde kwa kuzipatia watalaam, nyenzo na vitendea kazi. Aidha, Wizara itajenga Ofisi mpya ya bonde la Ziwa Nyasa katika Mji wa Tukuyu na kukamilisha ukarabati wa Ofisi ya Bonde la Mto Ruvuma katika mji wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafutaji wa maeneo ya kuchimba visima virefu, maji chini ya ardhi ni chanzo cha uhakika cha kuwapatia wananchi maji hususan, katika maeneo kame. Katika jitihada za kuboresha huduma za maji nchini, Wizara yangu katika mwaka 2005/2006 ilichunguza upatikanaji wa maji chini ya ardhi na jumla ya maeneo 1,384 yalionekana kuwa yanafaa kwa ajili ya kuchimba visima vya maji. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuchunguza upatikanaji wa maji chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ili kubaini maeneo 1,500 ya kuchimba visima virefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usimamizi katika kuendeleza maji chini ya ardhi. Chini ya sheria ya usimamizi wa matumizi bora ya maji namba 42 ya mwaka 1974, Wizara yangu, imeandaa utaratibu wa uchimbaji wa visima vya maji kwa lengo la kudhibiti uchimbaji holela ambao unaweza kusababisha athari za kiafya kwa watumiaji maji ya visima na uharibifu wa mazingira. Katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu iliendelea kusimamia na kuratibu kwa karibu uchimbaji wa visima vya maji nchini ili kuhakikisha kwamba taratibu za kitaalam zilizowekwa zinafuatwa. Jumla ya visima 653

vilichimbwa na kusajiliwa katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Lindi, Kilimanjaro, Mara, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Rukwa, Singida, Shinyanga, Sumbawanga, Tabora na Tanga. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuratibu uchimbaji wa visima vya maji kwa kuimarisha usimamizi na udhibiti kupitia Ofisi za Mabonde. Aidha, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika uchimbaji wa visima ikiwa ni pamoja na kuwa na hati ya kutumia maji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji – shiriki *(Trans-Boundary Waters*) asilimia 43.4 ya raslimali za maji katika nchi yetu ni maji tunayoshirikiana matumizi yake na nchi nyingine katika mabonde ya Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Mto Ruvuma, Mto Pangani na Bonde la Kati. Kila nchi kwa upande wake imekuwa na msukumo wa kutumia raslimali za maji shiriki ili kuinua maisha ya wananchi wake kwa kubuni na kutekeleza miradi mbalimbali ya kutumia maji hayo bila kujali maslahi ya nchi nyingine na uendelevu wake. Kwa kutambua tatizo hilo ni muhimu kushirikiana katika matumizi ya raslimali hizo ili kuhakikisha kwamba zinakuwa endelevu na zinatumika kwa manufaa ya wananchi wa nchi shiriki. Katika kufikia azma hiyo, imelazimu kuunda vyombo madhubuti vya pamoja kwa ajili ya kusimamia matumizi endelevu ya raslimali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, nchi shiriki katika matumizi ya maji ya Bonde la Mto Nile chini ya chombo cha mpito cha ushirikiano kijulikanacho kama *Nile Basin Initiative (NBI),* ziliendelea na usimamizi wa hifadhi ya mazingira, uzalishaji wa umeme, matumizi bora ya maji kwa ajili ya umwagiliaji na kujenga mazingira ya kuaminiana katika matumizi ya maji. Aidha, mchakato wa kuunda Kamisheni ya Bonde la Mto Nile itakayosimamia na kuratibu matumizi endelevu ya raslimali za maji shiriki katika nchi za Bonde la Mto Nile upo katika hatua za mwisho za kukamilishwa. Ili kunufaika na ushirikiano huo, nchi yetu kupitia Wizara yangu inatathmini mahitaji ya maji kwa ajili ya sekta mbalimbali kwa manufaa ya Taifa letu na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Agosti, 2003, Bunge lako tukufu liliridhia Itifaki inayohusu Maji Shiriki katika Nchi za *SADC*. Itifaki hiyo imetoa mwongozo kwa nchi wanachama kuunda vyombo vya ushirikiano katika matumizi endelevu ya raslimali za maji. Chini ya Itifaki hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika na maji katika nchi zilizopo katika Bonde la Mto Zambezi iliendelea na mchakato wa kuanzisha kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi itakayosimamia na kuratibu matumizi endelevu ya raslimali za maji katika Bonde la mto huo.

Aidha, nchi ya Msumbiji iliendelea na mchakato wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya maji itakayosimamia na kuratibu matumizi endelevu ya raslimali za maji katika Bonde la Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Tanzania kwa kushirikiana na Kenya na Uganda iliendelea kutekeleza Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria chini ya utaratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara yangu ikiwa mdau.

Mradi huu ni miongoni mwa miradi ya ushirikiano chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Madhumuni ya mradi huo yalikuwa ni kubaini kiwango cha uchafuzi wa maji ya Ziwa Victoria na vyanzo vinavyosababisha uchafuzi huo ili hatua za kurekebisha hali hiyo zichukuliwe kwa pamoja na nchi husika. Utafiti uliofanyika katika Awamu ya kwanza ya mradi umebaini yafuatayo:-

(a) Kumekuwa na ongezeko kubwa la virutubisho vya aina ya *Nitrogen* na *Phosphorus* ambapo karibu asilimia 80 ya virutubisho vinaingia ziwani kupitia angani. Hali hii inaendelea kuathiri ubora wa maji na ndiyo kiini cha kuenea kwa uoto uliokithiri kama vile magugumaji na vijimea *(Algae);*

(b) Kumekuwa na upungufu mkubwa wa hewa ya Oksijeni kwenye kina kinachozidi mita 20 kwa kipindi kinachokadiriwa kuwa miezi 9 katika mwaka, hali ambayo inaathiri kwa kiwango kikubwa uhai wa viumbe hususan samaki; na

(c) Uchambuzi wa maji ya kina kifupi katika maeneo ya mwambao wa ziwa hasa kwenye miji mikubwa ya mwanza, Musoma na Bukoba.

Awamu ya pili ya mradi huo, ambayo itazihusisha pia nchi za Rwanda na Burundi, itatekelezwa chini ya uratibu wa Wizara yangu, kwa kuzingatia matokeo ya tafiti ya Awamu ya kwanza ya Mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kudumisha ushirikiano na nchi zilizopo kwenye Bonde la Mto Nile, Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC,* katika utekelezaji wa itifaki, programu na miradi mbalimbali, yenye lengo la kuweka utaratibu mzuri wa kuhifdhi, kuendeleza na kutumia maji shiriki kwa faida ya wananchi wa nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vingi vya maji nchini, vimechafuliwa kutokana na uharibifu wa mazingira, unaotokana na shughuli mbalimbali za binadamu karibu au kwenye vyanzo vya maji. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya vyanzo vya maji, kwa kukagua vyanzo vya maji 493 katika mabonde ya mito ya Rufiji (256) na Ruvuma (35), Ziwa Victoria (25), Ziwa Nyasa (62), Ziwa Rukwa (2), Ziwa Tanganyika (32) na Bonde la Kati (81). Aidha, migodi mikubwa minane na viwanda 57, vilikaguliwa na hatua kuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam wa kurekebisha miundombinu ya kusafishia majitaka na/au kuchukua hatua za kisheria ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji. Pia, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, wananchi walihamasishwa kuhusu hifadhi ya vyanzo vya maji na matumizi bora ya maji na jinsi zitakavyodhibiti uchafuzi katika ngazi za Wilaya na vijiji, kwa kutunga na kusimamia sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, niwashukuru Wakuu wa Mikoa na Wilaya, kwa hatua na jitihada wanazochukua kwenye maeneo yao za kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji. Utunzaji wa vyanzo vya maji ni jukumu letu sote hususan, katika kipindi hiki ambapo maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali, yanaendelea

kupungua siku hadi siku. Hatua zinazochukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwaondoa wafugaji na wakulima waliovamia vyanzo vya maji ni muhimu kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri za Wilaya, itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira na Vyanzo vya Maji, ili kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa vyanzo hivyo. Aidha, naziomba Halmashauri za Wilaya, ziorodheshe vyanzo vyote vya maji katika maeneo yao na kutunga sheria ndogo za kulinda vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilihakiki ubora wa maji kwa kuchunguza viwango vya kemikali na uwepo wa vijidudu katika sampuli za maji 2,800 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Matokeo ya uchunguzi huo yalibaini kuwa, asilimia 80 ya vyanzo hivyo, maji yake yalikuwa katika viwango vinavyokubalika Kitaifa. Katika kuhakikisha majitaka yanayorudishwa kwenye vyanzo vya maji baada ya kusafishwa yanafikia viwango vinavyokubalika Kitaifa, Wizara yangu, iliendelea kuhakiki ubora wake katika mifumo ya majitaka ya Manispaa za Dodoma na Morogoro na Majiji ya Mwanza na Dar es Salaam. Matokeo yamebaini kuwa, usafishaji wa majitaka hayo haujafikia viwango vinavyokubalika hivyo, juhudi zinaendelea kuchukuliwa na Wizara yangu ili kurekebisha hali hiyo. Aidha, Wizara yangu iliendelea kuhakikisha kuwa, maji yanayotumiwa na wananchi, yanasafishwa na kutibiwa kufikia viwango vinavyokubalika Kitaifa, ikiwa ni pamoja na kukagua ubora wa madawa yanayoingizwa nchini, kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji. Wizara yangu pia, iliendelea kuimarisha maabara za maji, kwa kuzipatia vifaa na madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuziimarisha maabara za maji nchini, kwa kuzipatia usafiri, vifaa na madawa ili ukaguzi wa vyanzo vya maji ufanyike kwa ufanisi zaidi na pia, kupata takwimu sahihi na za kutosha za kutolea maamuzi. Aidha, taratibu za kisheria za utoaji wa hati za utapaji wa majitaka zitakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa vijijini, umeongezeka kwa asilimia 0.2 kutoka asilimia 53.5 mwaka 2004/2005, hadi asilimia 53.7 mwaka 2005/2006. Kama nilivyokwisha eleza hapo awali, kiwango hiki ni kidogo ikilinganishwa na Malengo ya MKUKUTA na yale ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, ambapo ongezeko la ukuaji linatakiwa kufikia asilimia mbili kwa mwaka. Kutofikiwa kwa kiwango hicho, kulitokana na ukame uliosababisha kukauka au kupungua maji kwenye vyanzo na hivyo kuathiri utoaji wa huduma za maji na pia, kuwa na uwekezaji mdogo kwenye sekta ya maji. Hali hiyo ni changamoto kwa Wizara yangu. Katika mwaka 2006/2007, tumekusudia kutekeleza mikakati ya kuhakikisha huduma ya maji vijijini inaongezeka kwa kiwango cha kuridhisha, kwa kushirikisha wadau katika ngazi zote za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zitakazochukuliwa na Wizara yangu ili kuhakikisha huduma ya maji vijijini inaongezeka, ni pamoja na kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji vijijini, kuchimba visima virefu na vifupi, kujenga mabwawa hususan, katika Wilaya karne na kuendeleza teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, kupitia Shirika lake la Maendeleo *(JICA)*, imekamilisha uchunguzi wa maji katika vijiji 22 katika Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam. Vile vile, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, ilianza upembuzi yakinifu wa miradi ya maji vijijini katika Wilaya zote za Mikoa ya Mwanza na Mara. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini, imekamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya kukarabati na kujenga miradi ya maji katika vijiji 122. Wizara yangu pia, iliendelea na hatua za kumpata Mhandisi Mshauri, atakayesanifu awamu ya pili ya mradi wa maji wa Chalinze, ambao utahudumia vijiji 42, Wilaya ya Bagamoyo vijiji 38 na Kibaha vijiji vinne. Mradi huo utatekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kusanifu miradi ya maji kwa ajili ya Miji ya Muleba, Urambo, Chunya, Ruangwa na Kijiji cha Nyakagomba (Geita) na awamu ya pili ya mradi wa maji wa Chalinze. Aidha, Wizara yangu inatambua tatizo la maji linaloikabili Miji ya Masasi, Nachingwea na Tarime. Kutokana na ufinyu wa bajeti na kiasi kikubwa cha fedha kinachohitajika kukamilisha uchunguzi na hatimaye kujenga miradi ya maji ya chemchemi ya Mbwinji kwa ajili ya miji ya Masasi na Nachingwea; matumizi ya maji ya Ziwa Victoria kwa ajili ya Mji wa Geita na mradi wa maji wa Mji wa Tarime; Wizara yangu katika mwaka 2006/2007, itaendelea kuwasiliana na wahisani mbalimbali ili kutafuta fedha za kutosha kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, iliendelea kuboresha huduma za maji vijijini, kwa kukarabati miradi 20 ya maji ya Kayenze, Sikonge, Kitomanga, Iwindi, Chato, Nyang’hanga/Kabila, Same, Njombe Vijijini, Usangi,Chunya Vijijini, Manyoni, Maswa, Magu Mjini, Nderemo – Handeni, Lesingita, Kiponzelo, Mugango/Kiabakari, Makonde, Muleba na Rombo Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, itaendelea na ukarabati wa miradi ya maji ya Same, Gonja Maore, Kilulu, Kiponzero/Kihanga, Mugango/Kiabakari, Gabimori, Hedaru, Makonde, Maswa, Lushoto, Rombo Vijijini, Njombe-Wakichi Kibena, Karagwe, Muheza – Ubembe/Kwemhosi, Bariadi, Mwanza Vijijini, Mbinga Vijijini na Iringa Vijijini. Miradi mingine ni ya Kayenze – Ilemela, Nassa, Sikonge, Kotomanga, Iwindi, Chato, Tunduma, Makete, Dindimo, Nyang’hanga/Kabila, Masonga, Singa-Kibosho, Elerai/Longido, Kwanyange-Mwanga, Sumve/Mantare, Korogwe Mjini na Njombe Vijijini. Miradi mingine itakayokarabatiwa ni ya Usangi, Nzega Vijijini, Mgwashi - Handeni, Kamachumu, Ileje Vijijini, Rondo, Litumbakuhama/Kingirikiti-Mbinga, Njombe Mjini, Maswa, Mwanga Mjini, Kongwa, Galula/Mbuyuni/Mbagala/Songwe, Magu, Ngudu, Igunga, Nderema - Handeni, Same Mjini, Namanyere, Tukuyu, Magubike, Biharamulo, Kilwa Masoko na Sengerema.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani, kupitia Benki yake ya Maendeleo *(KfW),* pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini, itaanza kukarabati miradi 30 ya maji katika awamu ya kwanza ya utekelezaji, ambayo itachukua muda wa miaka minne na utakapokamilika, utawanufaisha wananchi wanaokadiriwa kufikia 65,400.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Hai na Serikali ya Ujerumani, iliendelea na utekelezaji wa awamu ya nne ya mradi wa maji wa Wilaya hiyo, utakaohudumia vijiji 17 vya Kifuni, Mkomongo, Umbweonana, Kombo, Umbwesinde, Manushi Ndoo, Manushisinde, Kindi na Sambarai. Maeneo mengine ni Kilanya, Lyamungo Kati, Lyamungo Sinde, Mlama, Orori, Ussari, Tella na Kimashuku. Katika mwaka 2006/2007, awamu ya nne ya mradi huo, itaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2005/2006, iliendelea kushirikiana na Serikali ya Uholanzi katika kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, inayozihusisha Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga. Jumla ya visima virefu 15 na vifupi 52 vilichimbwa, ukarabati na ujenzi wa miradi mitatu ya bomba na ujenzi wa mabwawa mawili. Aidha, ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji katika Mji wa Maswa umekamilika. Katika mwaka 2006/2007, kuanzia mwezi Januari, 2007, programu hii itajumuishwa katika utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, inayoanza kutekelezwa mwezi Julai, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* iliendelea na utekelezaji wa miradi sita ya maji ya mtiririko katika vijiji vya Barabarani, Migombani, Majengo, Losirwa, Alarash na Orkejuloongishu. Pia, iliendelea kujenga mabwawa madogo matatu ya kuhudumia maeneo ya Meserani, Makyuni, Skarda na Ngoswak; Uchimbaji wa visima virefu vinane katika maeneo ya Makuyuni - Lemiyoni (1), Ngaramtoni (1), Namanga (2), Lesoit - Mariani (1), Eworendeke (1), Sinonok (1) na Ngoswak (1). Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu, itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli na Benki ya Maendeleo ya Afrika, katika utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Serikali ya Japan, kupitia Shirika lake la Maendeleo la *JICA*, kutekeleza na kukamilisha ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 37 vya Mikoa ya Lindi na Mtwara. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na *JICA* itaendelea na utekelezaji wa mradi huo utakaohudumia vijiji 27 zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, katika juhudi za kueneza teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua, ilitoa mafunzo ya ujenzi wa matangi kwa mafundi binafsi 24 katika Wilaya ya Chunya. Aidha, katika kuendeleza matumizi ya teknolojia hiyo, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaziwezesha Halmashauri za Wilaya za Lindi

Vijijini na Babati, kujenga matangi ya mifano ya kuvuna maji ya mvua kwenye mapaa ya nyumba katika taasisi za umma, ikiwa ni pamoja na shule na vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, itapanua miradi ya maji ya Madibira, Chiuwe, Pangani, Ilula, Igombe, Malya, Kilwa Masoko, Mwisanga/Ntomoko, Mundarara, Mji wa Bunda na Nyamuswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini katika Wilaya tatu za awali za Rufiji, Kilosa na Mpwapwa, kwa kutumia fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Kazi zilizotekelezwa na kukamilika ni uchimbaji visima vifupi 94 na ufungaji wa pampu za mikono katika visima hivyo; uchimbaji na ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji wa visima virefu 25 na ufungaji wa pampu katika visima virefu 17; na ujenzi wa miradi mitano ya maji ya mtiririko katika Wilaya hizo. Katika mwaka 2006/2007, utekelezaji wa mradi utaendelea kwa kufunga pampu za kusukuma maji kwenye vijiji vya Kimbuga, Mtawanya, Jaribu Mpakani, Ngarambe, Ruaruke na Muhoro katika Wilaya ya Rufiji, Msowero, Kitange II na Mtumbatu katika Wilaya ya Kilosa. Kazi hiyo itakapokamilika, vijiji 44 katika Wilaya hizo tatu za Rufiji, Kilosa na Mpwapwa, vitapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa mradi huo katika Wilaya nyingine 11 za Morogoro vijijini, Mvomero, Kongwa, Kondoa, Manyoni, Singida Vijijini, Iramba, Igunga, Kiteto, Kilindi na Handeni. Utekelezaji wa mradi huo umeanza katika Wilaya hizo na ujenzi upo katika hatua mbalimbali. Mradi utakapokamilika mwezi Juni, 2007 vijiji 90 katika Wilaya hizo vitakuwa vimepatiwa huduma ya maji. Katika mwaka wa 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, itaendelea na ujenzi wa miradi katika miji midogo ya Igunga, Kiomboi, Kondoa na Kongwa. Tathmini ya zabuni kwa ajili ya kuwapata wachimbaji wa visima na ujenzi wa miradi kwa miji ya Kondoa na Kiomboi, imekamilika na uchimbaji wa visima na ujenzi wa miradi, utaanza mara baada ya kusaini Mkataba na Halmashauri za Wilaya husika. Taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kujenga mradi wa maji kwa mji mdogo wa Igunga zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, kwenye Wilaya 14 nilizozitaja hapo awali, hususan katika kuwashirikisha wananchi, sekta binafsi na wadau wengine, Wizara yangu kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007, itaanza kutekeleza programu ya Taifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, ambayo itatekelezwa katika Halmashauri zote nchini kwa fedha ya mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).* Aidha, nchi za Ujerumani na Uholanzi, zimeonyesha nia ya kuchangia katika kugharamia utekelezaji wa programu hiyo. Utekelezaji wake utaanza kwa kila Halmashauri ya Wilaya kuchagua vijiji 10, kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo la maji katika Wilaya husika, hivyo jumla ya vijiji 1,075 vitahusika.

Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, usanifu wa miradi ya kusambaza maji katika maeneo hayo, utaanza kwa kuwashirikisha Wahandisi Washauri. Kwa hivi sasa Wilaya hizo zipo kwenye hatua za kuchagua Wahandisi Washauri hao. Programu hiyo inayohusu ujenzi na upanuzi wa miradi ya maji na uboreshaji wa usafi wa mazingira nchini kote, ni kubwa na ya kipekee kutekelezwa hapa nchini tangu tupate uhuru. Utekelezaji wake utaharakisha kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi vijijini kutoka asilimia 53.7 ya sasa hadi kufikia asilimia 65, kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na katika MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu itatekelezwa katika ngazi ya Wilaya kwa kusimamiwa na Wizara yangu, kwa kuzingatia Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002. Utekelezaji wa programu hiyo utahusu yafuatayo:-

(a) Ujenzi wa miundombinu ya miradi ya maji na usafi wa mazingira na uhamasishaji wa wananchi kuhusu elimu ya afya na usafi wa mazingira;

(b) Kuongeza uwezo wa kila Halmashauri wa kusimamia utekelezaji wa programu hiyo;

(c) Kuboresha mawasiliano na mgawanyo wa majukumu kwa lengo la kuongeza uwezo wa kila mdau ikiwemo sekta binafsi katika uboreshaji wa huduma ya maji vijijini;

(d) Kuongeza uwezo wa Wizara kwa kuimarisha ushirikiano na taasisi nyingine zikiwemo Wizara ya Afya na TAMISEMI; na

(e) Kuboresha mfumo wa kupokea na kutoa taarifa ili kuweza kuratibu na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa programu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha malengo ya programu hiyo, ni muhimu kwa Wilaya zote kuwa na wahandisi wa maji na vitendea kazi vya kutosha. Tathmini iliyofanywa na Wizara yangu, imeonyesha kuwa, kuna upungufu wa wataalam na vitendea kazi katika ngazi ya Wilaya. Ili kukabiliana na tatizo hilo, ni muhimu kwa Halmashauri za Wilaya, kuajiri Wahandisi wanaotakiwa na kuwa na vitendea kazi vinavyofaa, kwa ajili ya kutekeleza kikamilifu programu hiyo. Jumla ya wahandisi 52 wanahitajika, kwa ajili ya Wilaya ambazo hazina Wahandisi wa Maji. Ni vyema suala hili likapewa kipaumbele na Halmashauri husika, kwani itakuwa siyo busara, kuidhinisha fedha kwa Halmashauri ambayo ni dhahiri kuwa, haina uwezo wa kutekeleza majukumu ya programu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, inatambua ukubwa wa tatizo la upungufu wa Wahandisi wa maji katika ngazi ya Wilaya hivyo, kwa kushirikiana na TAMISEMI, itaongeza watalaam wa maji na mahusiano katika ngazi za Mikoa ili kuweza kutoa ushauri wa kitaalam *(Technical Backstopping)* katika kutekeleza programu hiyo, kwenye ngazi za Wilaya kwa ufanisi zaidi. Nachukua nafasi hii, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, nao wawe wasimamizi katika utekelezaji wa programu hiyo ili

kupunguza au kuondoa kabisa kero ya maji kwa wananchi katika maeneo itakakotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kuhamasisha uundaji na uimarishaji wa vyombo vya watumiaji maji *(Water User Associations),* katika miji mikuu ya Wilaya, miji midogo na vijiji vilivyoundwa kisheria kwa lengo la kutoa huduma ya maji iliyo endelevu. Utekelezaji wa taratibu hizo, umeleta mafanikio yafuatayo:-

(a) Ongezeko la mwamko wa wananchi kumiliki na kugharamia uendeshaji wa miradi ya maji vijijini;

(b) Idadi ya Kamati za Maji imeongezeka kutoka 8,363 mwaka 2004/2005 na kufikia Kamati 10,701 mwaka 2005/2006;

(c) Fedha zilizopo kwenye akaunti za Mifuko ya Maji zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 1.3 mwaka 2004/2005 hadi shilingi bilioni 1.386 mwaka 2005/2006;

(d) Bodi za maji katika ngazi ya Wilaya zimeongezeka kutoka 39 mwaka 2004/2005 na kufikia 67 mwaka 2005/2006;

(e) Vyombo vya watumiaji maji vilivyoanzishwa kisheria vimeongezeka kutoka 75 mwaka 2004/2005 hadi kufikia vikundi kutoka 1,709 mwaka 2004/2005 na kufikia vikundi 7,239 mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka 2005 kwamba, katika jitihada za kuboresha huduma za maji vijijini, Serikali ilianza kutumia utaratibu wa kupeleka fedha za Sekta ya Maji moja kwa moja kwenye Halmashauri za Wilaya, kwa kutumia kigezo cha idadi ya watu ambao bado hawajapata huduma za maji. Katika mwaka huu wa fedha. Jumla ya shilingi bilioni 9.6 zimetengwa kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za maji kupitia utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuimarisha skimu kubwa sita za maji katika vijiji vya Maswa, Mugango/Kiabakari/Butiama, Chalinze, Makonde, *Handeni Trunk Main (HTM)* na Wanging'ombe, kwa kutoa fedha za ukarabati na kulipia gharama za uendeshaji. Sababu kubwa za kuendelea kuimarisha skimu hizo ni pamoja na ukubwa wake, gharama kubwa za uendeshaji, baadhi ya skimu kuhudumia zaidi ya Wilaya moja na uhaba wa Wahandisi katika ngazi ya Wilaya. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.9, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.3 zitatumika katika kuchangia gharama za uendeshaji kwa kulipia umeme na madawa ya kusafisha na kutibu maji na shilingi bilioni 1.6 zitatumika kukarabati skimu hizo. Fedha hizo ni nyongeza ya fedha ambazo Wilaya husika zitapata kutokana na mgao kama nilivyoelezea katika aya iliyotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuwapatia wananchi wengi vijijini huduma ya maji, kwa matumizi ya watu na mifugo, Wizara yangu inaweka kipaumbele

katika ujenzi wa mabwawa na malambo. Mabwawa na malambo haya yakijengwa na kutunzwa vizuri, ni chanzo muhimu cha maji kwa wananchi na pia kwa mifugo. Kwa mfano, katika Wilaya ya Igunga, ambayo ni kame, imetekeleza mpango kama huo kwa kujenga mabwawa 32 na hivyo, kupunguza tatizo la maji. Hiki ni kielelezo kwamba, mpango kama huo, unaweza kufanikiwa mahali pengine penye mazingira kama ya Igunga.

Njia nyingine itakayozingatiwa na Wizara yangu katika jitihada za kuwapatia wananchi wengi zaidi huduma ya maji vijijini ni uchimbaji wa visima virefu. Hivi ni vyanzo ambavyo vinaweza kustahimili ukame, kwa kuwa maji yake yapo chini ya ardhi, ingawa hupungua wakati maeneo ya vyanzo yanapoharibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 15 Juni, 2006, Wizara yangu kupitia Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa, ilichimba visima virefu 437, vilivyogharamiwa na Wizara, Taasisi za Kiserikali, Taasisi za Dini, Wafadhili, Halmshauri za Wilaya na watu binafsi. Vile vile, Wakala ulichunguza kwa kina, maeneo 318 na mabwawa madogo manne, yalijengwa kwa kusimamiwa na Wakala katika maeneo ya Tarawanda na Kigongoni Mkoani Pwani, Misungwi Mkoani Mwanza na Sale-Ngorongoro Mkoani Arusha. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itakamilisha ujenzi wa Bwawa la Mugumu katika Wilaya ya Serengeti, ambapo shilingi bilioni 2.5 zimetengwa kwa ajili hiyo. Pia, Wizara imetenga shilingi bilioni 6.5, kwa ajili ya kujenga mabwawa 20 ya ukubwa wa kati na shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya kuchimba visima virefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika kipindi cha mwaka 2006/2007, imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.5 ili kuimarisha Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa, kwa lengo la kuiwezesha kutoa huduma kwa wateja kwa gharama nafuu. Fedha hizo zitatumika kukarabati mitambo chakavu, kununua mitambo mipya miwili na kununua vifaa vya kisasa vya kutafiti maji chini ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa mijini katika Makao Makuu ya mikoa 19, umeongezeka kwa asilimia 1.0 kutoka asilimia 73 mwaka 2004/2005 hadi asilimia 74 mwaka 2005/2006. Kama nilivyokwisha eleza hapo awali, kiwango hiki ni kidogo ikilinganishwa na malengo ya MKUKUTA na yale ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, ambapo ongezeko la ukuaji linatakiwa kufikia asilimia 3.2 kwa mwaka. Kutofikiwa kwa kiwango hicho ni kutokana na ukame uliosababisha kukauka au kupungua kwa vyanzo vya maji na hivyo kuathiri utoaji wa huduma za maji. Miji iliyoathirika zaidi na ukame huu, uliosababisha upungufu katika uzalishaji maji ni pamoja na Musoma kwa asilimia 46, Sumbawanga asilimia 43, Arusha asilimia 22, Songea asilimia 36, Lindi asilimia 17 na Mwanza asilimia 15. Aidha, kina cha maji kwenye bwawa la Mindu Mjini Morogoro, kilishuka kutoka mita 5.07 hadi mita mbili, wakati Bwawa la Igombe Mjini Tabora, kina kilishuka kutoka mita tano hadi mita moja. Hali hiyo ni changamoto kwa Wizara yangu na katika mwaka huu wa fedha, Wizara imekusudia kutekeleza mikakati ya kuhakikisha kuwa, huduma ya maji mijini inakua kwa

kiwango cha kuridhisha, kwa kuhifadhi vyanzo vya maji na kuboresha huduma katika Mamlaka za Maji Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa maji katika miji mikuu 19 ya mikoa, umeongezeka kutoka lita bilioni 101 kwa mwaka 2004/2005, hadi lita bilioni 102 mwaka 2005/2006. Makusanyo ya maduhuli katika miji hiyo, yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 17.4 mwaka 2004/2005 hadi kufikia shilingi bilioni 20.8 mwaka 2005/2006. Mamlaka nane kati ya 19, zimeendelea kujitegemea kimapato, kwa kulipia gharama zote za uendeshaji bila ya msaada kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Marekebisho ya Muundo wa Madaraja ya Mamlaka, ambayo yamefanyika kulingana na Tangazo la Serikali Na. 282/2005 la mwezi Novemba, 2005, Mamlaka za Maji za Miji ya Musoma, Shinyanga, Singida na Sumbwanga, zitaingia kwenye Daraja B kutoka C na zitaanza kuwalipa watumishi wake wote mishahara, kuanzia mwezi Julai 2006 na Serikali itaendelea kuchangia sehemu ya gharama za umeme wa kuendesha mitambo ya uwekezaji. Aidha, kuanzia mwezi Julai, 2006, Mamlaka ya Maji ya Mjini Mtwara, ilipandishwa Daraja kutoka C kuingia A na hivyo kuanza kujitegemea. Kutokana na mafanikio hayo, kwa sasa ni Mamlaka za Maji za Miji ya Babati na Lindi, zimebakia katika daraja C, ambapo Serikali itaendelea kugharamia mishahara ya watumishi, umeme wa kuendeshea mitambo na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu imeandaa mpango mahsusi wa kuboresha huduma ya majisafi na majitaka katika miji 19 ya mikoa ya Tanzania Bara. Mpango huo utatumika kama dira ya uwekezaji katika miji hiyo hadi mwaka 2020. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, itagharamia kazi za dharura, ambazo ni ukarabati wa mifumo ya majisafi katika Miji ya Babati, Lindi, Mtwara na Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia, kwa kushirikiana na Jumuiya ya nchi za Ulaya *(EU)*, kupitia Mfuko wa *ACP – EU Water Facility* na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)*, itagharamia uchunguzi, usanifu na maandalizi ya makabrasha ya zabuni ya mpango wa muda mrefu wa kukarabati na kupanua mifumo ya majisafi na ujenzi wa mifumo ya uondoaji wa majitaka (*Urban Upgrading Program*) katika miji saba ya Babati, Lindi, Mtwara, Sumbawanga, Bukoba, Musoma na Kigoma, kwa gharama ya shilingi bilioni 3.8. Aidha, katika mwaka 2006/2007, upembuzi yakinifu wa mfumo wa majitaka katika Mji wa Kigoma, utaanza chini ya Mpango wa *Lake Tanganyika Regional Development Programme (PRODAP),* unaogharamiwa na Mfuko wa Maendeleo wa nchi za Nordic na kuratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa, kupitia Shirika la Maendeleo la *AFD*, ilikamilisha upembuzi yakinifu wa miradi ya majisafi na majitaka katika Miji ya Bukoba, Musoma na Misungwi na kubaini kuwa gharama za kutekeleza miradi hiyo ni shilingi bilioni 95.5 katika mgawanyo ufuatao: Bukoba shilingi bilioni 31.7; Musoma shilingi bilioni 48.8 na Misungwi shilingi bilioni 15.0. Katika mwaka 2006/2007, Serikali ya Ufaransa kupitia *AFD*, imekubali kuchangia kiasi cha shilingi bilioni 9.6, kwa ajili ya kutekeleza kazi za dharura katika

Miji ya Bukoba na Musoma. Aidha, mazungumzo kati ya Serikali na Shirika la Misaada la Marekani la *Millenium Challenge Corporation (MCC)*, yameanza na Shirika hilo limeonyesha nia ya kusaidia miradi mbalimbali ya maji ikiwa ni pamoja na Mradi wa Maji wa Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Makazi la Umoja wa Mataifa *(UN – Habitat),* chini ya Mpango wa *Lake Victoria Regional Water and Sanitation Initiative*, itagharamia uboreshaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Bukoba kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kukarabati chanzo cha maji na matangi matatu ya kuhifadhi maji katika maeneo ya Kashura, Magoti na Rwamishenye;

(b) Kununua pampu mpya nne kwa ajili ya kufunga kwenye kituo cha kusukuma maji kutoka ziwani; na

(c) Kujenga vioski vya maji 25 kwenye maeneo mbalimbali katika Mji wa Bukoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilishirikiana na Serikali ya Uswisi, kuandaa programu ya kuboresha huduma za maji katika Miji ya Tabora na Dodoma, kwa kukarabati na kupanua mifumo ya majisafi. Programu hiyo itatekelezwa kwa mfumo wa utatu, ambapo Serikali ya Tanzania, Serikali ya Uswisi kupitia Shirika la *SECO* na Mamlaka za Maji za Miji ya Dodoma na Tabora, zitachangia gharama. Programu hiyo itatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu, kuanzia mwaka 2006/2007, kwa gharama ya shilingi bilioni 24. Katika utaratibu huo, *SECO* itachangia shilingi bilioni 17.8; Serikali ya Tanzania itachangia shilingi milioni 792 na Mamlaka husika, zitachangia shilingi bilioni 5.5. Mkataba wa makubaliano ya kutekeleza programu hiyo, utasainiwa mwanzoni mwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na *OPEC,* iliendelea na uchunguzi wa kutafuta maeneo ya kuchimba visima virefu, ikiwa ni vyanzo vya maji mbadala kwa ajili ya Mji wa Singida, baada ya chanzo cha awali cha Bwawa la Itamka, kuonekana kuwa maji yake hayafai kwa matumizi ya binadamu. Uchunguzi wa maji chini ya ardhi, kwa lengo la kupata maeneo manne ya kuchimba visima vya majaribio, unaendelea ambapo mkandarasi tayari amewasilisha taarifa ya awali ya uchunguzi huo. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itagharamia uchimbaji na kuendeleza visima virefu vinne, kukarabati na kupanua mfumo wa maji uliopo kwa gharama ya shilingi bilioni 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kuboresha huduma za maji mijini, kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali, kwa kukarabati mifumo ya majisafi na majitaka mijini. Wizara yangu kwa kushirikiana na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU)* na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW),* iliendelea

kuimarisha huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Mwanza na Mbeya na Manispaa ya Iringa, kwa gharama ya shilingi bilioni 13. Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa vyanzo vya maji, ukarabati wa mitambo ya kusafisha maji, ujenzi wa matangi ya kuhifadhi maji na ukarabati wa mifumo ya usambazaji wa majisafi.

Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea na uboreshaji wa huduma za maji katika Majiji ya Mwanza na Mbeya na Manispaa ya Iringa. Aidha, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la fedha la *KfW,* iliendelea kutekeleza awamu ya pili ya mradi wa kupanua mfumo wa majisafi na ujenzi wa mfumo wa majitaka katika Mji wa Songea, baada ya kusainiwa Mkataba mwezi Desemba, 2005. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kutekeleza awamu ya pili ya mradi huo kwa gharama yashilingi bilioni 5.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kutumia fedha za ndani, iliendelea kuboresha huduma za majisafi katika Miji ya Kigoma, Musoma, Sumbawanga na Lindi, kwa gharama ya shilingi milioni 338. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itakarabati miradi ya majisafi kwenye Miji ya Sumbawanga, Lindi, Mtwara, Kigoma, Musoma na Tabora, kwa gharama ya shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kupanua mifumo ya usambazaji majisafi na uondoaji wa majitaka mijini, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutoa huduma hizo ili kukabiliana na kukua kwa miji na ongezeko la watu. Katika mwaka 2005/2006, upanuzi wa ujenzi wa miundombinu ya majisafi ulitekelezwa katika Mji wa Singida na Babati. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wahisani mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Serikali ya Ujerumani, Umoja wa Nchi za Ulaya, Serikali ya Uswisi na *BADEA*, itatumia shilingi milioni 8.73 kupanua mifumo ya majisafi katika Miji ya Iringa, Mwanza, Dodoma, Singida na Bukoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea na ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria, kwenda Miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji 54 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Kama ilivyokwisha elezwa hapo awali, mradi huo utakapokamilika, utaleta manufaa yafuatayo:-

(a) Upatikanaji wa majisafi, salama na ya kutosha kwa wananchi wapatao milioni moja na mifugo yao ifikapo mwaka 2010 katika vijiji 54 vilivyopo katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga, ikiwemo Manispaa ya Shinyanga na Mji wa Kahama.

(b) Kupungua kwa magonjwa ya kuambukiza yatokanayo na uhaba wa maji na matumizi ya maji yasiyo salama na hivyo wananchi watakuwa na afya nzuri za kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kijamii ili kuwawezesha kuchangia katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato chao.

(c) Kuvutia wawekezaji katika nyanja za viwanda, migodi na biashara.

(d) Kutoa ajira kwa wananchi wakati wa ujenzi na uendeshaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa mradi huo, Wizara yangu inatumia kandarasi nne ili kuharakisha ujenzi. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2005, Wizara yangu ilikuwa tayari imesaini mikataba minne ya ujenzi na makandarasi na hadi kufikia mwezi Juni, 2006, utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 65. Gharama za utekelezaji wa kandarasi zote nne ni shilingi bilioni 193.57. Kazi ambazo tayari zimetekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Ulazaji wa bomba kuu la urefu wa kilomita 233 lenye vipenyo kati ya milimita 1,200 na 300. Hadi sasa kazi imekamilika kwa kulaza mabomba hayo umbali wa kilomita 108, sawa na asilimia 46.

(b) Ujenzi wa matangi 47 yenye ukubwa wa mita za ujazo 35,000 hadi 45. Kazi ya ujenzi wa Matanki hayo umekamilika kwa asilimia 65.

(c) Ujenzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 625 katika Miji ya Shinyanga na Kahama. Hadi sasa ujenzi wa mtandao huo umefikia kilomita 167, sawa na asilimia 27.

(d) Ujenzi wa kituo cha kusafirishia maji katika Kijiji cha Ihelele umekamilika kwa asilimia 85.

(e) Ujenzi wa vituo vya kuvuta maji kutoka ziwani na kile cha kusukuma maji safi kutoka mtambo wa kusafishia maji kwenda tangi kuu katika Mlima Mabale umekamilika kwa asilimia 75.

Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kusimamia ujenzi wa Mradi huo na inatarajiwa kuwa kazi za kandarasi zote nne zitakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji na taratibu za kutoa huduma za maji mijini. Kulingana na Sheria ya Maji Namba 8 ya mwaka 1997, huduma za maji mijini zinatolewa na Mamlaka za Maji chini ya usimamizi wa Bodi za Wakurugenzi zenye wawakilishi wa makundi mbalimbali ya jamii katika miji husika. Katika mwaka 2005/2006, Wiazara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kiufundi la Ujerumani *(GTZ)*, ilikamilisha maandalizi ya kuweka mtandao wa kisasa wa takwimu za kiufundi na mahesabu katika kuboresha utunzaji wa takwimu na taarifa mbalimbali za Mamlaka hizo. Mtandao huo utaanza kutumika rasmi mwezi Julai, 2006 na utakuwa na uwezo wa kupokea, kutunza na kusambaza takwimu kwa haraka na kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuwa, bei za maji mijini ni kubwa na zinapangwa kiholela bila kuzingatia matumizi halisi. Katika jitihada za kupunguza malalamiko hayo, Wizara yangu inashirikiana na Mamlaka za Maji Mijini, kufunga dira za maji ili wateja wote walipe kulingana na matumizi halisi. Kwa sasa tayari wateja wote walipe kulingana na matumizi halisi. Kwa sasa tayari asilimia 82 ya wateja wote wa maji mijini wamefungiwa dira za maji. Hatua hiyo ilisaidia kupunguza upotevu wa maji kutoka asilimia 50 mwaka

2004/2005 hadi asilimia 45 mwaka 2005/2006. Lengo ni kuwafungia dira za maji wateja wote wa maji mijini ifikapo 2010. Hivi sasa baadhi ya Mamlaka za Maji Mijini, zimefunga kompyuta zenye uwezo wa kuweka na kutunza kumbukumbu za dira za maji ili kutoa Ankara zilizo sahihi. Aidha, kila Mamlaka ya Maji Mijini, imeanzisha Kitengo cha Huduma kwa Wateja, yaani *Customer Care* na kuanzisha Ofisi za Kanda ili kushughulikia kwa haraka malalamiko ya wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka huu wa fedha, mapendekezo ya bei za maji ambazo bodi za mamlaka za maji zilizoanzishwa kisheria zitapendekeza, yatawasilishwa kwenye chombo kilicho chini ya Wizara ya Maji cha kusimamia utoaji wa huduma za maji, umeme na mazao yatokanayo na petroli, yaani *Energy and Water Utility Regulatory Authority – EWURA.* Chombo hicho ambacho kimeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 11 ya Mwaka 2001, kitasimamia utoaji wa huduma za maji katika mamlaka hizo, ikiwa ni pamoja na kujadili kwa mapana bei za maji kwa kuhusisha makundi yote ya watumiaji na watoa huduma. Lengo ni kuwa na viwango vya bei ya maji, vyenye kuzingatia maslahi ya pande zote mbili. Utendaji wa chombo hicho, unatarajiwa kwa kiwango kikubwa, kupunguza malalamiko ya wateja juu ya kupanda kiholela bei za maji na pia kuwezesha mamlaka hizo kutoa huduma endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Raslimali ya Ulaya, iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Huduma za Majisafi na Majitaka kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Kazi zilizotekelezwa ni ukarabati wa mitambo ya kuzalisha maji katika vyanzo vya Ruvu Juu na Ruvu Chini, ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40. Ulazaji wa mabomba makuu mapya umefikia asilimia 30, na mabomba ya usambazaji maji yenye vipenyo kati ya milimita 150 na 600 ya urefu wa mita 26,340 yamelazwa. Lengo ni kulaza mabomba ya urefu wa mita 85,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuboresha huduma za uondoaji wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam, Wizara yangu iliendelea na ukarabati wa bomba linalomwaga majitaka baharini. Hadi sasa ulazaji wa bomba jipya umefikia mita 970 kati ya mita 1,036 sawa na asilimia 94. Aidha, mabomba ya kukusanyia majitaka ya urefu wa kilomita 10.3, yamelazwa katika lengo la kulaza mabomba ya urefu wa kilomita 14.6. Pia, ukarabati wa mabwawa ya kusafisha majitaka katika maeneo ya Buguruni, Vingunguti, Kurasini, *Air – Wing* Ukonga, Mikocheni, Mabibo na Lugalo, upo katika hatua za mwanzo za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji katika Mto Ruvu ambao ni chanzo kikuu cha maji kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, kwa muda mrefu sasa yamekuwa yakipungua sana wakati wa kiangazi mara baada ya msimu wa mvua kumalizika na hivyo kutotosheleza uzalishaji wa maji katika mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Hali hii imejitokeza zaidi katika kipindi cha mwaka 1997 – 2005, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa hapa nchini, ambapo mvua zinaendelea kupungua na au kunyesha kwa kipindi kifupi. Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hilo, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kutafuta vyanzo vipya na utafiti wa awali ulifanyika

na kupendekeza ujenzi wa bwawa katika eneo la Kidunda Mkoani Morogoro, ambalo linakadiriwa kugharimu shilingi 70.0 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira hususan, katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam na maeneo yanayokaliwa na makundi ya watu wa kipato cha chini. Wizara yangu chini ya usimamizi wa *DAWASA* inatekeleza Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa gharama ya shilingi bilioni tatu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Miradi hiyo inatekelezwa kwa kushirikisha makundi mbalimbali ya kijamii. Aidha, katika utekelezaji wa miadi hiyo, Wizara yangu pia, inashirikiana na Serikali ya Ubelgiji.

Katika mwaka 2005/2006, maandalizi ya miradi hiyo yalikamilika katika maeneo 16 ya Manispaa zote za Jiji la Dar es Salaam yenye matatizo ya maji. Chini ya ushirikiano huo, jumla ya shilingi bilioni 2.63 zitatumika, ambapo Serikali ya Ubelgiji itachangia shilingi bilioni 2.2, Manispaa ya wananchi husika watachangia shilingi bilioni 430. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaanza utekelezaji kwa kuchimba visima 16 katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Serikali kusitisha Mkataba na Kampuni ya *City Water Limited* wa kutoa huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, Serikali iliunda Kampuni ya *DAWASCO* na kuanza mara moja kutoa huduma katika maeneo husika. Wananchi waliendelea kupata huduma kama kawaida na hali ya huduma hizo iliboreshwa baada ya pampu mpya mbili kufungwa katika mtambo wa kusafishia maji ya Ruvu Juu. Kwa ujumla tangu kuanzishwa kwa *DAWASCO*, mafaniko yafuatayo yamepatikana:-

(a) Kuongeza kwa makusanyo ya maduhuli kutoka shilingi milioni 950 kwa mwezi kabla ya kuundwa kwake na kufikia wastani wa shilingi bilioni 1.5 kwa mwezi.

(b) Kupungua kwa kiwango cha uvujaji wa maji kutoka maeneo 3,500 yaliyokuwa yanavujisha maji hadi maeneo 200 kwa mwezi.

(c) Kuongezeka kwa muda wa upatikanaji wa maji.

(d) Kufungwa kwa kompyuta mpya zenye uwezo wa kuweka na kutunza kumbukumbu na kutoa ankara zilizo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafaniko hayo, bado huduma ya maji kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam siyo ya kuridhisha. Katika jitihada za kukabiliana zaidi na tatizo hilo la huduma za maji katika Jiji hilo, utafiti uliofanywa na Wizara yangu kwa kutumia wataalam wa ndani, umebaini kuwa kuna uwezekano wa kuongeza kiasi cha maji kinachozalishwa kwenye mtambo wa Ruvu Chini kutoka galoni milioni 40 kwa siku kwa sasa hadi kufikia galoni milioni 60. Ili kufanikisha lengo hilo, italazimu kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kupanua kituo cha kuzalisha na kusukuma maji cha Ruvu Chini pamoja na kufunga pampu mpya tatu.

(b) Kulaza bomba jipya la kipenyo cha inchi 54 la umbali wa kilomita 15 kutoka kituo hicho sambamba na sehemu ya bomba kuu lililopo lenye msukumo mkubwa wa maji. Bomba hilo litasaidiana na lililopo kuhimili msukumo mkubwa wa maji.

Gharama za kutekeleza upanuzi huo inakadiriwa kufikia shilingi bilioni 37.5. Aidha, utekelezaji wa kazi hizo utaanza mara baada ya fedha kupatikana na utachukua miezi 15 hadi kukamilika. Maeneo yatakayonufaika na upanuzi huo ni pamoja na Msasani, *Bahari Beach,* Masaki, Mikocheni, Mwenge, Sinza, Kijitonyama, Temeke, Mbagala, Mtoni, Kurasini na maneo ya viwanda yaliyopo Barabara ya Nyerere. Wizara yangu inaendelea na jitihada za kutafuta fedha hizo ili utekelezaji wa kazi hizo uanze mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Chuo cha Maji kilikuwa na wanafunzi 102 wa Cheti cha Ufundi Sanifu. Kati ya hao wanafunzi 41, walihitimu mafunzo mwezi Mei, 2006 katika fani za uhandisi wa mifumo ya usambazaji wa maji, utafutaji wa maji ardhini na uchimaji visima vya maji, sayansi ya maji *(Hydrology)* na teknolojia ya maabara za uchunguzi wa maji. Aidha, mwezi Desemba, 2005, mafundi sanifu 86 walihitimu mafunzo katika fani za ufundi bomba, uunganishaji wa vyuma, ufundi magari na ufundi umeme wa magari na majumba. Wizara yangu pia iliendelea kukiboresha Chuo cha Maji, kwa kukarabati majengo na kukipatia vifaa na nyenzo muhimu kwa ajili ya kuendeshea mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, katika jitihada za kukipa Chuo cha Maji hadhi ya Kitaifa na Kimataifa na pia kuboresha utoaji mafunzo kulingana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na mahitaji ya soko la ajira, katika mwaka 2005/2006, chuo kilianzisha mtaala mpya wa kutoa tuzo za Kitaifa za elimu ya ufundi *(National Technical Awards – NTA),* kuchukua nafasi ya mtaala wa mafunzo ya ufundi sanifu. Mtaala huo unalenga kutoa tuzo za Kitaifa za elimu ya ufundi kuanzia ngazi ya nne *(NTA 4),* yaani Cheti cha Awali cha Elimu ya Ufundi, mpaka ngazi ya sita *(NTA 6),* ambayo itatoa cheti cha Stashahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara yangu kupitia Chuo cha Maji, itaendelea kutoa mafunzo kwa mafundi sanifu wa sekta ya maji. Aidha, Chuo kimelenga kuongeza idadi ya wanafunzi wapya kutoka 50 wa mwaka 2005/2006, hadi kufikia 70 mwaka 2006/2007. Vile vile, chuo kitatoa mafunzo kwa mafundi sanifu wapatao 200 katika daraja la kwanza, la pili na la tatu, katika fani za ufundi bomba, uunganishaji wa vyuma, ufundi magari na ufundi umeme wa magari na majumba. Aidha, katika utaratibu wa mtaala mpya, wanafunzi 49 wa cheti cha awali cha ufundi sanifu *(NTA 4),* katika fani za Uhandisi wa Mifumo ya Usambazaji wa Maji na Uondoaji majitaka, utafutaji wa maji ardhini na uchimbaji visima vya maji, sayansi ya maji na teknolojia na maabara za uchunguzi wa maji, watahitimu mafunzo yao mwezi Agosti, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina jumla ya watumishi 1,774 ikilinganishwa na mahitaji yake ambayo ni watumishi 1,965. Katika mwaka 2005/2006, jumla ya watumishi 41 walipandishwa vyeo, 20 walibadilishwa vyeo na wanane walithibitishwa kazini. Aidha, katika jitihada za kuendeleza watumishi na kuboresha utendaji wa kazi, watumishi 12 waliajiriwa na 199 walipata mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi.

Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2006/2007, imepata kibali cha kuajiri watumishi 191 wa fani na kada mbalimbali. Aidha, watumishi wenye sifa, watapandishwa vyeo kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira ya Utumishi wa Umma. Watumishi 335 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu, ndani na nje ya nchi. Pia, Wizara itaendelea na zoezi la kuwathibitisha kazini, watumishi wanaomaliza muda wao wa majaribio kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na TAMISEMI, Halmashauri za Wilaya, Taasisi ya Takwimu ya Taifa na Wizara nyingine, ikiwa ni pamoja na Afya na Ustawi wa Jamii, Nishati na Madini, Maendeleo ya Mifugo, Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Fedha katika kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza takwimu na taarifa kwa watumiaji kulingana na mahitaji. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, iliendelea kutoa takwimu na viashiria vinavyohusu hali ya umaskini kwa ajili ya usambazaji kupitia tovuti ya Serikali, inayohusu taarifa za kiuchumi na kijamii. Takwimu hizo zinatumika kutathmini maendeleo ya sekta ya maji katika suala zima la kupambana na umaskini. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusu sekta ya maji. Pia, itaendelea kuiboresha tovuti ya Wizara kwa lengo la kupokea na kutoa taarifa sahihi za sekta ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya jumla yaliyowekwa na Serikali katika mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania (MKUKUTA), yataweza kufikiwa kwa sekta mbalimbali kutekeleza wajibu na majukumu yao, ambayo yanahusiana na sekta nyingine. Utekelezaji wa Sera, Mikakati na usimamizi wa sheria za sekta mbalimbali, unalazimu kufanyika kwa majadiliano na kufikia makubaliano kati ya sekta moja na nyingine katika maeneo yale ambayo yanahusiana.

Wizara yangu katika mwaka 2006/2007, itaimarisha majadiliano na ushirikiano wa kiutendaji na sekta nyingine ambazo tunahusiana nazo ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Aidha, mwezi Septemba, 2006 Wizara yangu, itafanya mapitio ya sekta ya maji kwa pamoja na wahisani wote, kwa lengo la kutathmini hali ya sekta ilivyo kwa sasa katika nyanja za utoaji huduma, uwekezaji na maeneo ya ushirikiano na sekta nyingine. Pia, katika kuimarisha mawasiliano kati ya Wizara na watendaji wa sekta ya maji katika Halmashauri za Wilaya, Wizara itaweka mfumo wa kupashana habari katika Wilaya zote kwa kutumia mtandao wa kompyuta *(Management Information System – MIS)*. Mfumo huo wa mawasiliano utarahisisha ufuatiliaji na upatikanaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maji katika ngazi za Wilaya ili hatua zinazostahili zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, itaendelea kushirikiana na Wizara za Maliasili na Utalii, Kilimo, Chakula na Ushirika na

TAMISEMI, katika kutekeleza mkakati wa kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji ulioandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimimwa Naibu Spika, Wizara yangu inawajibika kutoa huduma za maji kwa makundi mbalimbali ya jamii katika kutimiza azma ya Serikali ya kupunguza umaskini. Aidha, Wizara inatambua mchango wa wanawake katika utunzaji wa rasilimali za maji na uboreshaji wa huduma za maji. Wanawake na watoto ndio wanaoathirika zaidi kutokana na kukosekana kwa huduma za maji, kwa kutembea umbali mrefu na kutumia muda mwingi katika kutafuta maji. Pamoja na mchango wanaotoa na adha wanayopata, kundi hilo halina sauti katika kufikia maamuzi ya kupanga, kutekeleza na kuendesha huduma za maji.

Katika jitihada za kupunguza kero za uhaba wa maji na kuongeza ushiriki wa wanawake katika maamuzi ya kupanga, kutekeleza na kuendesha huduma za maji, Wizara imeimarisha Dawati la Jinsia Wizarani, kwa kumteua Mratibu, kuandaa mkakati wa jinsia wa sekta ya maji na kuunda Kamati ya kuratibu masuala ya jinsia. Vile vile, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, watumishi 195 walipatiwa mafunzo ya uhamasishaji wa masuala ya jinsia katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza mkakati wa jinsia sambamba na mpango wa kuongeza ushiriki wa wanawake katika maamuzi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kujenga uwezo wa dawati la jinsia;

(b) Kutoa mafunzo ya kijinsia kwa viongozi na wafanyakazi;

(c) Kuelimisha na kuhamasisha watumishi wanawake kujua haki zao na sheria mbalimbali za nchi;

(d) Kuandaa vigezo vyenye mtazamo wa kijinsia kwa sekta ya maji ili kuwawezesha wataalam na wadau wa sekta ya maji kupanga na kutekeleza Sera na Mipango yenye mtazamo wa kijinsia;

(e) Kuimarisha ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu na taarifa zenye kuainisha masuala ya jinsia; na

(f) Kuandaa mpango maalum wa kuwaendeleza wanawake wataalam ikiwa ni pamoja na kuunda umoja wa wanawake wataalam wa sekta ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Bunge lako Tukufu lilivyoelezwa mwaka 2005, Wizara yangu iliandaa na kuanza kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti UKIMWI kwa watumishi wa Sekta ya Maji. Suala la UKIMWI limepewa kipaumbele na litakuwa ni moja ya *agenda* wakati wa utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kisekta, ikiwa ni

pamoja na ujenzi wa miradi ya maji, maadhimisho ya Wiki ya Maji na Mkutano wa mwaka wa wataalam wa sekta ya maji.

Wizara pia, inawajibika katika kutoa msaada wa hali na mali, kwa watumishi waathirika watakaojitokeza. Aidha, kutokana na Kanuni na Haki za Binadamu, mwathirika wa UKIMWI, anapaswa kujitokeza na kutoa taarifa kwa mwajiri wake, kwa ridhaa yake bila kushinikizwa. Katika kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti UKIMWI, kwa mwaka 2006/2007, yafuatayo yatatekelezwa:-

(a) Kutathmini hali halisi ya UKIMWI pamoja na madhara yake katika Wizara;

(b) Kuendesha mafunzo ya waelimishaji rika pamoja na semina zitakazoelimisha watumishi namna ya kuepuka maambukizi ya UKIMWI;

(c) Kusambaza kondomu kama kinga dhidi ya UKIMWI; na

(d) Kusambaza vipeperushi, mabango, pamoja na vitabu vyenye ujumbe wa kujikinga na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuzuia Rushwa, kwa kuziba mianya ya rushwa katika Sekta ya Maji. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Kitengo cha Utawala Bora, pamoja na Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU), ilitoa miongozo na makala mbalimbali kwa watumishi wake, yanayohusu mbinu za kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuziba mianya ya rushwa na kuboresha huduma kwa wateja ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Taifa wa Kuzuia Rushwa na mpango uliowekwa kutekelezwa kisekta. Aidha, Wizara itaimarisha kitengo cha Sheria cha Wizara, ambacho kitakuwa mhimili wa kutoa na kufafanua mambo mbalimbali ya kisheria na pia itaendelea kusimamia kikamilifu, Sheria ya Manunuzi Na. 4 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Maji kwa mwaka 2005/2006 ni matokeo ya ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam, kutoka kwa nchi wahisani, taasisi zisizokuwa za Kiserikali, Mashirika ya Kidini, Mashirika ya Misaada na Taasisi za Kifedha za Kimataifa. Aidha, katika mwaka huu wa fedha, tutaendelea kushirikiana na nchi na mashirika hayo ya kihisani katika jitihada za kuendeleza na kusimamia Sekta ya Maji na kutatua matatizo ya maji hapa nchini. Napenda kuzishukuru Serikali za nchi ya Ujerumani, Japan, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi, Uswisi, Ireland, Ubelgiji, Marekani na Uingereza, kwa misaada yao. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa taasisi za fedha za Kimataifa, yaani Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA),* Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB),* Umoja wa Nchi zinazouza Mafuta Duniani *(OPEC),* Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU),* Mashirika ya Umoja wa

Mataifa ya *UNDP* na *UNICEF* na Shirika la Kimataifa Nguvu za Atomiki *(IAEA)*, kwa misaada na michango yao ya utaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Aidha, nayashukuru Mashirika ya Kidini ya *World Islamic League,* Shirika la *Al Munadhanat Al Dawa Al Islamia,* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa la Kilutheri la Ujerumani na Kanisa Katoliki Tanzania *(TEC),* pamoja na Taasisi nyingine za hiari za *Water Aid, Millenium Challenge Corporation (MCC),* Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili *(IUCN), World Wildlife Fund (WWF)* na wale wote ambao kwa njia moja au nyingine, wameendelea kuisaidia Wizara yangu katika kutoa huduma kwa wananchi. Naomba, kwa dhati kabisa, kupitia kwako Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Shamsa Selengia Mwangunga, Mbunge wa Viti Maalum, kwa msaada na ushirikiano wake. Aidha, napenda pia, nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu, Bwana Patrick Rutabanzibwa, Wakuu wa Idara, Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu, pamoja na wataalam wote, kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.170,302,291,900 kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2006/2007. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni Sh.22,962,164,000, ambapo Sh.6,170,564,000 ni mishahara ya watumishi *(PE)* na Sh.16,791,600,000 ni fedha za matumizi mengine *(OC)*. Bajeti ya Maendeleo ni Sh.147,340,127,900, ambapo kati ya hizo Sh.77,864,995,000 ni fedha za ndani na Sh.69,475,132,900 ni fedha za nje.

Naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza. Hotuba yangu pia, inapatikana katika tovuti ya Wizara yangu kwa anwani *www.maji.go.tz*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN (k.n.y. MHE. GIDEON A. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kutumia nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kuhusu utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara ya

Maji, kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutekeleza masharti ya kanuni ya 81(1), Toleo la mwaka 2004, naomba kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Pia nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza sana wewe binafsi, pamoja na Wenyeviti wa Bunge, kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili Tukufu, kwa kipindi cha miaka mitano. Sisi sote tu mashahidi wa viwango na kasi nzuri katika uongozi wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Edward N. Lowassa, kwa kuteuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa, Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri, kwa kuteuliwa katika nyadhifa zao. Mwisho, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa na wananchi, pamoja na wale walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge. Tunawapa hongera nyingi sana na kuwatakia kazi njema katika uwakilishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati hii, kwa ushirikiano wao mkubwa wakati wa kuchambua na kupitia bajeti ya Fungu 49, Wizara ya Maji. Natumia nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo: Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa Salehe, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Kheri Khatibu Ameir, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu; Mheshimiwa Manju S.O. Msambya; Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye; Mheshimiwa Said J. Nkumba; Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Shally J. Raymond; Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Fred M. Tungu, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda; Mheshimiwa Martha J. Umbulla na Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, ilikutana Dar es Salaam, tarehe 30 Mei, 2006 ili kuchambua, kutoa maoni na kushauri juu ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara ya Maji, kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2006/2007. Ili kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilizingatia utaratibu ufuatao: Kupitia utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka uliopita; kuchambua utekelezaji wa malengo ya

bajeti kwa mwaka 2005/2006; na kuchambua na kupitia kazi zilizopangwa kufanyika mwaka wa fedha 2006/2007 na maombi ya fedha kwa kazi hizo.

Kamati iliridhika na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa ushauri wa Kamati ulioutoa wakati inachambua bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha uliopita. Aidha, Kamati ilitoa ushauri mbalimbali ili kuleta ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za maji na utoaji wa huduma za maji safi na maji taka mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifahamishwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana wakati wa kutekeleza bajeti ya mwaka uliopita, baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mpango wa kutekeleza mkakati wa kuendeleza sekta ya maji umekamilishwa na programu ya uendelezaji na usimamizi wa rasilimali ya maji pamoja na programu ya uendelezaji wa huduma za maji mijini na vijijini zimeandaliwa.

(b) Katika jitihada za kutafuta vyanzo vipya vya maji, Wizara imechunguza jumla ya maeneo 1384 ili kuona kama yanafaa kuchimba visima virefu. Kati ya maeneo hayo, visima 653 vimechimbwa lengo lilikuwa ni kuchimba visima 600.

(c) Wizara kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika na masuala ya maji na mazingira katika nchi za Kenya na Uganda, iliendelea kutekeleza mradi wa hifadhi ya mazingira ya Ziwa Victoria ambapo takwimu zinazohusu ubora wa maji zilikusanywa kwa ajili ya kuzichambua na taarifa inaonyesha hali ya usafi na ubora wa maji wa Ziwa Victoria umekamilika.

(d) Idadi ya Kamati ya Maji imeongezeka kutoka 8,363 Desemba, 2004 na kufikia Kamati 10,701 Desemba, 2005. Fedha zilizoko kwenye akaunti za mifuko ya maji zimeongezeka kutoka Sh.1,300,000,000 Desemba, 2004 hadi Sh.1,386,054,646 Desemba, 2005.

(e) Wizara imeunda ofisi za maji za mabonde ya Ziwa Tanganyika na Bonde la Mto Ruvuma. Aidha, hati 235 za haki ya kutumia maji zimetolewa kwa watumiaji. Mapato katika ofisi za maji za mabonde hayo yameongezeka kutoka Sh.440,453,099 mwaka 2004/2005 hadi Sh.522,499,325 mwaka 2005/2006.

(f) Wizara iliendelea na ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda kwenye Miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji 54 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Mradi huu ukikamilika, utawezesha upatikanaji wa maji safi na salama ya kutosha kwa wananchi wapatao milioni moja pamoja na mifugo yao ifikapo mwaka 2010.

(g) Wizara iliendelea na ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda kwenye Miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji 54 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Mradi huu ukikamilika, utawezesha upatikanaji wa maji safi na salama ya

kutosha kwa wananchi wapatao milioni moja pamoja na mifugo yao ifikapo mwaka 2010.

(h) Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, imeendelea kuboresha huduma za maji vijijini kwa kukarabati miradi ya maji ya Kilosa, Kitomanga, Maswa, Kayenze, Iwindi, Same, Kiponzelo, Muleba, Rombo, Arumeru, Makonde, Handeni, Sikonge, Chato, Monduli, Magu Mjini, Nyakahanga Kabila, Usangi Chini, Manyoni, Serengeti, Geita, Mzenga na Gabimori.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati yangu ilibaini changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo uliathirika kutokana na kutopatikana kwa fedha za ndani na nje kwa wakati unaotakiwa.

(b) Upungufu wa wataalam wenye sifa zinazohitajika umepunguza kasi ya kutekeleza miradi ya maji katika ngazi ya Wilaya.

(c) Uvamizi wa maeneo ya vyanzo maji kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii umeleta uharibifu wa mazingira na hivyo kuathiri upatikanaji wa maji.

(d) Mabadiliko ya hali ya hewa yalisababisha ukame wa muda mrefu katika maeneo mengi nchini na hivyo kuathiri vyanzo vya maji na utoaji wa huduma ya maji.

(e) Viwango vikubwa vya gharama ya umeme unaotumika katika kuendeshea mitambo ya kuzalisha maji vinaongeza gharama za uendeshaji na kusababisha ankara za maji kuwa kubwa kwa watumiaji wa maji mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha uliopita na kutoa ushauri mbalimbali kwa Wizara kama ifuatavyo:-

Tatizo la uhaba wa wataalam wa fani ya maji. Uhaba wa wataalam wa sekta ya maji unakwamisha kwa kiasi kikubwa, juhudi za Serikali kuwapatia wananchi maji safi na salama mijini na vijijini. Aidha, wataalam wachache waliopo hususan katika ngazi za Halmashauri, hawana sifa zinazostahili, hali hii husababisha utekelezaji wa miradi mingi ya maji kuchelewa kukamilika kwa kukosa uratibu na usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua tatizo hili, Kamati inaishauri Serikali, kukipandisha hadhi Chuo cha Maji cha Rwegarulila kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ili kitoe taaluma ya Uhandisi wa Maji. Aidha, juhudi zifanywe kukipanua Chuo hicho, pamoja na kupitia upya mitaala yake ili iende sambamba na ukuaji, mabadiliko na maendeleo ya Sekta ya Maji. Kadhalika, utoaji wa ajira katika Sekta ya Maji ufuate utaratibu ambao unatumiwa hivi sasa na sekta za elimu, afya na kadhalika, ambapo menejimenti ya utumishi wa umma, huhusishwa ili kudhibiti ubora wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la utoaji wa ankara za maji zisizokuwa sahihi, limekuwa sugu na ni kero kubwa kwa watumiaji wa maji. Kamati inapendekeza kuwa, utatuzi wa tatizo hili upewe kipaumbele kwa mamlaka zote za maji. Aidha, mamlaka za maji zitumie mfumo wa *computer* katika utoaji wa ankara za maji ili kukabiliana na tatizo hili. Wizara pia iweke utaratibu wa kuzikutanisha mamlaka za maji ili kubadilishana uzoefu, kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Sekta za Maji, maana hivi sasa mamlaka hizo zinazidiana sana, kiutaalam na kiufanisi, katika utoaji huduma na usimamizi wa sekta ya maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika Kamati yangu inashauri kuwa, hatua thabiti zichukuliwe ili kuhakikisha kuwa, wadeni sugu hususan Wizara na Taasisi za Serikali, wanalipa madeni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inaipongeza Wizara, kwa kukamilisha uanzishaji wa ofisi zote tisa za mabonde ya maji nchini. Ofisi hizi ni ofisi za Mto Pangani, Bonde la Mto Rufiji, Bonde la Ziwa Victoria, Bonde la Ziwa Tanganyika, Bonde la Ziwa Nyasa, Bonde la Ziwa Rukwa, Bonde la Mto Ruvuma, Mbwenkulu na Pwani ya Mashariki, Bonde la Kati lenye Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Shinyanga na Bonde la Mto Wami Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa, ofisi hizi zinatekeleza kwa ufanisi shughuli zake, Kamati inashauri Wizara kuzipatia ofisi hizi wataalam na nyenzo za kutosha na kuboresha maslahi ya Maafisa wa Maji wa mabonde hayo. Aidha Ofisi hizo zifanye kazi kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya ambazo ni walengwa wakuu wa ofisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa Mfuko wa Maji Kitaifa, tofauti na Sekta nyingine kama madini na utalii, uwekezaji wa Sekta ya Maji umekuwa mgumu kwani hauwavutii wawekezaji wengi kutokana na mtaji mkubwa. Aidha, sekta binafsi, bado haijahamasishwa kushiriki kikamilifu katika Sekta ya Maji. Hali hii inaifanya Serikali kuwa mwekezaji mkubwa pekee katika Sekta ya Maji. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uanzishaji wa Mfuko wa Maji Kitaifa kama njia endelevu wa kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za kila siku za binadamu, unatishia uhai na upatikanaji wa rasilimali muhimu za maji kwa vizazi vilivyopo na vijavyo. Aidha, sehemu ya uharibifu huo unatokana na upandaji wa miti kwa mfano jamii ya mikaratusi, *ekalptus, grandisi, salgina, kamalgundesi* na *sitrodiodora,* inayokausha maji. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri Wizara ihamasishe wananchi, waepuke upandaji wa miti inayokausha vyanzo vya maji. Aidha, kampeni maalum ifanywe ili miti ya aina hiyo, iondolewe kwenye vyanzo vya maji na kupanda miti mingine inayohifadhi maji nchini kote. Pamoja na hilo, Serikali pia ihakiki mara kwa mara, vyanzo vya maji na kuwaelimisha wananchi, wasijenge kwenye maeneo hayo. Kadhalika wale waliojenga kwenye maeneo ya vyanzo vya maji, waondolewe.

Aidha, wananchi waishio katika vijiji vilivyo karibu na vyanzo vya maji, wapewe kipaumbele katika kupatiwa maji ili washiriki ipasavyo kulinda vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara, kwa hatua ilizochukua kuhamasisha wananchi kuvuna maji ya mvua na kujenga mabwawa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Ili juhudi hizo ziweze kuleta mafanikio, Kamati inaishauri Serikali, wananchi na wadau mbalimbali, kuvuna maji ya mvua na kujenga mabwawa katika ngazi ya kaya kwa maeneo kame. Aidha, juhudi zifanywe, kuhamasisha uvunaji wa maji mashuleni, kwenye zahanati na kadhalika. Yajengwe mahodhi, malambo na mabwawa kwa ajili ya kuhifadhia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakala wa uchimbaji visima ni chombo muhimu katika kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali ya maji. Aidha, kutokana na sera za soko huria, makampuni na wananchi mbalimbali, wamekuwa wakichimba visima hususan katika Jiji la Dar es Salaam ili kujikwamua na tatizo la upatikanaji wa maji. Hata hivyo, visima vingi vinavyochimbwa na makampuni ya watu binafsi, havina viwango na ubora unaotakiwa. Hali hii husababisha mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza hususan kipindupindu. Ili kuhakikisha ubora wa visima vinavyochimbwa na makampuni na watu binafsi, Kamati inaishauri Serikali kuupa nguvu wakala wa uchimbaji visima ili uweze kusimamia uchimbaji na Wizara iimarishe huduma ya uhakiki wa ubora wa maji ya visima hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo hafifu ya maji taka hususan mijini, ndicho chanzo kikubwa cha milipuko ya magonjwa mbalimbali hasa kipindupindu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, katika baadhi ya maeneo, watu wasio waaminifu wameunganisha mifumo ya majisafi, pamoja na ile ya majitaka, kama tulivyoshuhudia hivi karibuni, Buruguruni Jijini Dar es Salaam. Aidha, katika maeneo mengi, mifereji ya maji ya mvua, imeunganishwa na majitaka. Ili kutatua tatizo hili, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa, ramani za ujenzi wa nyumba mpya, ziwe zinaonyesha mfumo wa usafirishaji wa maji taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za sasa zinaonyesha kuwa ni asilimia 20 tu ya wananchi, ndiyo wameunganishwa kwenye mifumo ya majitaka. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Wizara, itoe elimu na kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kuunganishwa kwenye mifumo ya majitaka na athari zitokanazo na mifumo hafifu ya majitaka. Sambamba na hilo, Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Halmashauri za Miji, ianzishe mradi wa kutokomeza kipindupindu, kama ilivyokwisha fanyika kwa magonjwa mengine. Katika harakati hizo, Wizara ihakikishe kuwa, sehemu kubwa ya wakazi wa mijini wanaunganishwa kwenye mifumo ya majitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka nchini, bado zinaendelea na mifumo ya kusafirisha na kutupa majitaka baharini bila kuyasafisha. Hali hii inatishia uhai wa viumbe wa baharini na binadamu kwa ujumla. Ili kuepukana na athari zitokanazo na maji hayo, Kamati inaishauri Serikali, ishirikiane na Mamlaka hizo kutumia mifumo na teknolojia ya kisasa ya kusafisha majitaka. Aidha, Serikali pia

iangalie uwezekano wa ku- *recycle* maji hayo ili yaweze kutumika kukidhi mahitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeipongeza Wizara ya Maji, kwa juhudi inayofanya, kuhakikisha upatikanaji wa Maji Safi na Salama Mijini na Vijijini, pamoja na fedha kidogo inazotengewa. Mfano mzuri wa miradi hiyo ni Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria, unaoendelea hivi sasa na Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira katika Wizara zote. Kadhalika, Wizara imeanza kuratibu na kujenga bwawa la kuhifadhia maji kwenye Mto Ruvu, kwenye eneo la Kidunda Mkoani Morogoro, ili kuongeza upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamaoyo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara, ikamilishe miradi mbalimbali ya Maji iliyoanzishwa siku za nyuma ili wananchi waondokane na adha ya kutopata maji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Maji kama zilivyo Sekta nyingine nchini, imeathirika na inakabiliwa na changamoto kubwa ya ugonjwa wa UKIMWI na athari zake kwa rasilimali watu. Kamati inaishauri Wizara, kuwasaidia waathirika wa Ugonjwa wa UKIMWI, kwa kuwapatia mafunzo hususan lishe bora na dawa, virutubisho vya kurefusha maisha *(ARVs),* badala ya kujikita kwenye warsha, semina na makongamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maombi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2006/2007, Sekta ya Maji kutengewa kiasi kidogo cha Fedha za Maendeleo. Katika hotuba yake ya kwanza Bungeni tarehe 30 Desemba, 2005, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alibaini kuwa kero ya maji ndiyo kero nambari moja vijijini na mijini. Kwa kuzingatia kauli ya Rais, Kamati inaishauri Serikali, kuitengea Sekta ya Maji fedha za kutosha kwa ajili ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, kwa kukamilisha miradi ya maji ya zamani na kuibua miradi mipya, hivyo kuwaondolea wananchi kero hiyo sugu.

Katika mwaka huu wa fedha, Wizara imetengewa kiasi cha shilingi 147,340,127,900/= tu, fedha za maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi 77,864,995,000/=. Kiasi hicho cha fedha ni kidogo ukilinganisha na majukumu makubwa iliyonayo Wizara hii. Kamati inaishauri Serikali, kuzingatia na kuboresha bajeti ya Wizara hii katika bajeti zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha taarifa hii, kwa kumshukuru kwa namna ya pekee, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira na Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Selengia Mwangunga, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipa Kamati hii, kila tunapokutana na Wizara. Kadhalika, kutoka katika sakafu ya moyo wangu, natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake, kwa kutushirikisha katika shughuli za Wizara ndani na nje ya nchi. Kamati yangu ina imani kubwa kuwa, ushirikiano huu utadumishwa. Aidha, nawapongeza Watendaji wa Wizara, wakiongozwa na Katibu, Ndugu yangu Patric Rutabanzibwa, kwa umahiri, umakini na ushirikiano waliouonyesha wakati Kamati inachambua bajeti ya Fungu 49 - Wizara ya Maji.

Nawashukuru kwa mara nyingine tena, waheshimiwa Wabunge, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa ushirikiano, umakini na ustahimilivu wao, ambao umefanikisha kazi hii muhimu.

Mwisho, namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Daniel Eliufoo, Ndugu Frank Mbumi wakisaidiwa na Bi Maria Mwakasege, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu, ilipitia vifungu mbalimbali vya matumizi ya kawaida ya Wizara ya Maji, ambayo ni shilingi 22,962,164,000 na bajeti ya maendeleo ambayo ni shilingi 147,340,127,900, jumla ya fedha zote ni shilingi 170,302,291,900.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii, kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza. Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa kupata fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu 43(5)(b) na (c) na 81(1), Toleo la 2004, kuhusiana na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Wabunge wenzangu, kukupongeza pamoja na Mheshimiwa Spika mwenyewe na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili katika kipindi cha uhai wa Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa pongezi kwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Naibu wake, Mheshimiwa Shamsa Selengia Mwangunga, pamoja na timu nzima ya utendaji ya Wizara hiyo, kwa majukumu makubwa na mazito waliyonayo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati, kwa wananchi wa Jimbo langu la Tarime, kwa kusimama imara kuitetea Demokrasia ya kweli katika nchi hii, bila kujali vitisho, majeraha na mauaji, wakanichagua mimi mnyonge mwenzao na kuikataa takrima ili niwe sauti ya wasiokuwa na sauti hapa Bungeni. Waliopoteza maisha yao, Mungu awarehemu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wangwe, naomba ukae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 50(8). Ni marufuku kwa Mbunge

yeyote kusema mambo ambayo hayana ushahidi. Mheshimiwa Chacha Wangwe, katika maelezo yake ameeleza hapa kwamba, wapiga kura wake walimchagua, pamoja na mauaji yaliyofanyika, sasa tunamtaka athibitishe kauli yake na kama hana uwezo wa kuthibitisha, basi aiondoe hiyo kauli. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kifungu unachozungumzia siyo cha 50(8), ni kifungu cha 50(1) ambacho kinasema hivi: "Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni, kwa sababu hiyo Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni, atawajibika kuwa na hakika kwamba, maelezo anayoyatoa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu na Spika au Mbunge mwingine yeyote, aweza kumdai Mbunge huyo, atoe uthibitisho wa usemi wake. Mbunge aliyetakiwa kufanya hivyo, atawajibika kutoa uthitibisho huo katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili hiyo."

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, yale uliyoyasema kwamba, kulikuwa na mauaji na pia walikataa takrima zao, wakakuchagua wewe; una ushahidi wowote ule?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama Mbunge, ambaye nimekula kiapo katika Bunge hili kwamba, nitasema ukweli daima, hayo ninayoyasema, nina uhakika nayo na nina ushahidi nayo na mengi ni ambayo nimeshamwandikia Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, anayo na mkitaka ushahidi zaidi, mtaupata kwa muda utakaonipa wewe mwenyewe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakupa wiki moja uwe na ushahidi wa kuleta.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitauleta.

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu maneno haya tunaposema una ushahidi, siyo maneno ya kutaniana Bungeni, naomba ukae kidogo. Siyo maneno ya utani, ni suala zito sana, katika huo muda wa siku saba, unaweza kutoa ushahidi wa mauaji yaliyotokea, kwa sababu ya kukunyima wewe kura na kwamba, yalikuwa yanakuhusu wewe. Kwa hiyo, ni vitu ambavyo kwetu ni *quite serious,* basi kama unao ushahidi tutafurahi. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi nitauleta ndani ya huo muda ulionipa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI:** Nikiendelea ni kwamba, hao waliopoteza maisha yao, Mwenyezi Mungu awarehemu na tuliobaki, tutasonga mbele mpaka demokrasia itoke kwenye vyombo vya habari, wananchi wawe huru kulingana na matakwa ya utawala wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakosa adabu kama sitakishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa kunipatia nafasi ya kuwawakilisha wananchi wa Tarime kwa tiketi yake. Namshukuru sana Mwenyekiti wa CHADEMA, Mheshimiwa Freeman Mbowe na watendaji wote wa Makao Makuu ya CHADEMA, kwa kunifanyia kampeni nzuri sana na yenye ubunifu mkubwa ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii, kuwapongeza wanaharakati wote wa Vyama vya Upinzani na wale wasiokuwa na vyama, kwa kuunga mkono Mageuzi ili mabadiliko ya kweli na Uhuru wa Kweli, yaje nchini mwetu. Tupate maendeleo ya kweli na demokrasia pana zaidi, inayojali Utawala Bora na Haki za Binadamu. Katika Uchaguzi Mkuu uliopita, harakati hizo zilifanyika katika mazingira magumu sana.

Mwisho, namshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa kuniona nafaa kumsaidia katika nafasi hii ya Msemaji Mkuu wa Kambi yetu katika Wizara nyeti ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa uchumi katika sekta zote za uzalishaji, unatakiwa uende sambamba na ukuaji wa sekta ya maji. Hivyo basi, maji ni kichocheo, yaani *catalyst* muhimu sana katika sekta zote za uzalishaji kama vile viwanda, uzalishaji umeme, kilimo cha kisasa, ufugaji na bila kusahau matumizi ya majumbani. Kwa hiyo, ningependa Serikali iangalie tena vipaumbele ambavyo imeviweka, kama vile ilivyosema kwamba, ni Elimu halafu Kilimo. Sisi wa Kambi ya Upinzani, tunaona pengine wangeangalia kwamba, Maji ndiyo kipaumbele cha kwanza kikifuatiwa na Afya halafu Kilimo

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa maji hapa Tanzania, unachangiwa kwa kiasi kikubwa na ushindani mkubwa uliopo miongoni mwa watumiaji katika sekta mbalimbali za uchumi, vile vile uharibifu unaofanywa katika vyanzo vya maji katika maeneo mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuwa na angalizo madhubuti kuhusu kuendeleza hazina ya maji iliyopo chini ya ardhi, yaani *ground water resources* na hili linasababisha upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo, japokuwa chini ya ardhi maji yapo mengi sana.

Mheshimiwaa Naibu Spika, MKUKUTA ni sehemu ya mpango wa Tanzania unaotokana na Mpango wa Umoja wa Mataifa wa kuondoa umaskini duniani, yaani *Millenium Development Goals (MDGs),* kwa lengo la kuzinusuru nchi zilizo maskini zaidi duniani, Tanzania ikiwa mojawapo. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani, inapenda kumpongeza mwakilishi wa Umoja wa Mataifa hapa nchini, aliyemaliza muda wake, Bwana John Hendra, kwa kusimamia vizuri mchakato mzima wa kuanzishwa kwa MKUKUTA, kwa kushirikiana na Serikali, Vyama vya Siasa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, yaani *NGOs*. Kwa mantiki hiyo, MKUKUTA si Sera ya chama Fulani, bali ni Mkakati wa Kitaifa wa Kuinua Uchumi wetu. MKUKUTA ni wetu sote na kamwe chama fulani cha siasa, kisihodhi Mkakati huu na kujifanya ni wake. Jambo la muhimu ni kuwa sote kwa pamoja, tushiriki kuhakikisha malengo ya MKUKUTA yanafikiwa.

Kila Halmashauri ya Wilaya na Mji, ihakikishe kuwa, imejiwekea malengo ya kila mwaka kufikia malengo makuu ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wakati wa kufanya kazi na kwa kweli tusilale mpaka malengo ya MKUKUTA katika Sekta ya Maji yafikiwe. Tujipime kila mwaka kuwa tumefikia wapi na Waziri wa Maji kila mwezi wa Juni au Julai, atoe taarifa Bungeni, kufanikiwa au kutofanikiwa katika kufikia malengo ya MKUKUTA katika mwaka uliokwisha. Hakuna kulala mpaka kieleweke, kueleweka ni Wananchi wote kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujikumbushe malengo ya MKUKUTA ili sote twende kwa pamoja katika mjadala huu wa Sekta nyeti ya Maji. Lengo kubwa la MKUKUTA ni kuhakikisha kuwa, ifikapo mwaka 2009/2010 zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania, waishio vijijini wanapata maji safi na salama ndani ya dakika thelathini kutoka makazi yao. Hii maana yake ni kwamba, akina mama 65 kati ya 100, waweze kutumia dakika thelathini tu kupata maji ifikapo mwaka 2010. Hali ya sasa ni mbaya sana huko Vijijini, kwani kuna Wanawake wanatumia zaidi ya saa mbili kupata maji. Lengo hili la MKUKUTA liliwekwa mwaka 2003. Je hali ya sasa ikoje; Serikali inatekeleza wajibu wake?

Taarifa ya Umaskini Tanzania *(Poverty and Human Development Report 2005)*, ambayo ni Taarifa ya Serikali na sina uhakika kama Mawaziri wetu wanasoma taarifa hizi. Katika ukurasa wa (xv), inatueleza kuwa, zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania wa Vijijini hawana uhakika wa maji safi na salama. Ripoti inaendelea kusema kuwa, katika Wilaya saba nchini, zaidi ya asilimia 90 ya wananchi hawana huduma ya maji safi na salama, kwa viwango vya MKUKUTA. Hii ni hatari, maana katika Wilaya hizi, watu 90 kati ya 100 hawana maji ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tu ya Bunge lako Tukufu, naomba nitaje Wilaya tatu ambazo zaidi ya asilimia 90 ya wananchi, hawana uhakika wa maji safi na salama, kwa mujibu wa Ripoti ya Umaskini, *percentage of households with access to water.* Wilaya hizi ni Sikonge watu saba tu kati ya 100 ndiyo wanaopata maji; Mkuranga watu tisa tu kati ya 100 wanapata maji; na Igunga watu tisa tu kati ya 100 wanapata maji. Hii ni taarifa ya mwaka 2005, *very recent.* Wilaya zote hizi toka mfumo wa Vyama Vingi umeanza, zinaongozwa na chama kinachotawala. Nawapa pole watu wa Igunga, Mkuranga na Sikonge, tuache siasa, hali hii inatisha. Ni lazima Serikali itoe maelezo hapa Bungeni, ni kwa nini hali ipo hivi katika Wilaya hizi na kuna mipango gani ya kuhakikisha kuwa, wananchi wa Wilaya hizi nao pia wanajiona ni Watanzania kwa kuwapatia maji.

Sote tunafahamu kwamba, miradi ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, kwa kutumia malori makubwa na *canters*, imeshamiri na inasemekana kwamba, mingi ya miradi husika, inamilikiwa na baadhi ya matajiri wachache. Hali ya utatuaji wa tatizo la maji kutokutengemaa, ni kweli kwamba, kutokana na matatizo ya maji, magari hayo yanasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza kero. Hata hivyo, gharama za ununuzi wa maji kwa ndoo/galoni ni kubwa mno kulingana na hali ya kipato cha Watanzania wengi.

Kambi ya Upinzani, ingependa kupata tamko la Serikali, kuhusiana na biashara husika, ambazo zinazidi kushika kasi na vilevile Serikali ituambie ni kiasi gani cha kodi, ambacho Serikali inapata kutokana na biashara hiyo, ambayo kwa safari moja tu inaingiza zaidi ya shilingi 45,000/= za Kitanzania. Kambi ya upinzani pia ingependa Serikali ituambie ni kwa kiasi gani maji hayo yanayouzwa ni salama kwa matumizi ya wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anajua kuwa maji ni uhai. Asilimia 79 ya mwili wa mwanadamu ni maji. Sayari yetu dunia asilimia 75 imezungukwa na maji. Mwenyezi Mungu, ametujalia nchi yetu Tanzania, maji mengi kuliko nchi nyingi za Bara la Afrika. Tumezungukwa na maji yaliyotuama katika maziwa makubwa kila upande. Kaskazini Ziwa Victoria, Magharibi Ziwa Tanganyika, Kusini Ziwa Nyasa. Kuna maziwa madogo madogo ndani ya nchi kama vile Ziwa Manyara, Ziwa Natron, Ziwa Eyasi na Ziwa Rukwa, pia kuna idadi lukuki ya mabwawa madogo madogo na makubwa.

Mito midogo ni mingi sana inayojaza mito mikubwa, inayokatiza nchi yetu kila upande kama vile Kagera, Malagarasi, Mara, Pangani, Wami, Ruvu, Rufiji, Ruaha, Ruhuhu na Ruvuma. Mito hiyo yote inatiririsha lita nyingi sana za maji kwenda baharini. Hiki ndicho kiwango cha Rasilimali Maji tulichonacho nchini na pia ni hasara kupoteza maji mengi namna hiyo, ambayo pia yangeweza kufanyiwa *recycling* badala ya kulalamika kwamba, maji yamepungua Bwawa la Mtera, basi maji hayo yawe yanakuwa *recycled* ili kuongeza umeme. Kwa hiyo, tutumie rasilimali hii kuhakikisha kuwa, watoto wetu wanapata uhakika wa maji miaka inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inatambua kuwepo kwa Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002. Kambi ya Upinzani, imeridhishwa na kauli ya Sera hiyo kwamba, Sera ya Maji ya mwaka 1991, ilikuwa haitekelezeki. Serikali hii, yenye watu wale wale, ilitunga Sera mwaka 1991 na kuweka malengo. Miaka 10 baadae, Serikali ile ile, ya watu wale wale, inasema hawawezi kutekeleza! Sera mpya nzuri sana kama mlivyomsikia Mheshimiwa Waziri, alipokuwa akiieleza na imetungwa vizuri, sasa tusije kuambiwa mwaka 2010 kwamba, hiyo nayo pia haitekelezeki. Watanzania wa mwaka 1991 si wa leo. Serikali itekeleze majukumu yake na itekeleze Sera zake mpaka nukta ya mwisho. Ikishindwa, njia nyepesi ni kutupisha sisi Wapinzani ili tuweze kutekeleza wajibu inavyotakiwa. Huo ndio uungwana, lakini si kujibadili kama kinyonga kila mwaka na kazi haifanyiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizingatia kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Maji, ina jukumu la kusimamia menejimenti ya matumizi yote ya maji na hivyo ni wajibu wake kutoa msukumo kwa wadau mbalimbali, kuona na wao wanashiriki ipasavyo katika matumizi endelevu ya maji. Kambi ya Upinzani tayari imeanza kuona mushkeli katika utekelezaji wa Sera ya Maji. Kwa mfano, Sera ya Maji, kifungu 4(1)(i), inahimiza wananchi kuanzisha mamlaka zao za maji *(Water Users Entities)*. Jambo hili ni muhimu sana, kwani linawafanya wananchi wenyewe kumiliki vyanzo vya maji na pia ugavi wa maji. Lakini Serikali hiyo hiyo tayari inaingilia maamuzi ya wananchi na kuleta siasa. Kwa mfano, Wilayani Karatu, Wilaya ambayo inaongozwa na CHADEMA kwa miaka kumi sasa, wananchi walianzisha mamlaka yao kwa jina la KAVIWASU. Baadhi ya

Viongozi wa Serikali, wakaingilia kati na kutaka kuzuia juhudi za wananchi. Sasa wananchi wanatekeleza Sera ya Taifa, Serikali ambayo ndio mtunzi wa sera hiyo inazuia! Tunaamini jambo kama hili, halitatokea katika Serikali ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete wa Awamu ya Nne wa Tanzania. Tuache kuingiza siasa katika masuala ya maendeleo. Kama Mpinzani akihakikisha maji yanapatikana, wanachama wa chama kinachotawala hawatakunywa? Tuondokane na mawazo mgando ya Chama Tawala, kuhodhi fikra na ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kutekeleza Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria ni nzuri sana. Hata hivyo, haina mantiki yoyote, kuvuta maji ya Ziwa Victoria hadi Shinyanga na Kahama, bila kuandaa miundombinu ya umwagiliaji katika vijiji ambavyo mabomba yanapita. Maji ya Ziwa Victoria, yatumike pia kwa umwagiliaji. Tunafuatilia kwa karibu sana mradi huu, kwani isije kuwa tunapeleka maji kwenye migodi tu na kuacha wananchi bila maji ya matumizi ya nyumbani na kilimo. Maana mfano wa umeme wa Gesi ya Songosongo, ambapo wananchi wa Kusini wameachwa solemba, usijirudie kwa maji ya Ziwa Victoria. Tunafuatilia kila hatua ya Mradi na tutawaeleza Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ianze kuandaa miundombinu ya kutumia maji ya Ziwa Victoria kwa Vijiji vyote, ambavyo maji hayo yatapita ili tuondokane na adha hii ya kuwa omba omba wa chakula. Naishukuru Wizara ya Maji, kwa mwaka huu kwa kuweka kipaumbele katika kutimiza ahadi ya Rais aliyetangulia, ya kuleta maji mjini Tarime. Tunashukuru kwa sababu watu 30,000 watapata maji, lakini watu laki tano wa vijiji 154, basi nadhani Serikali itaona hiyo ni *plan* ya pili ya kufikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Wizara ya Maji, ina chuo chake cha maji, yaani Chuo cha Maji Rwegalulila, huu ni muda muafaka kutumia wahitimu hao katika miradi kama hii ambayo inatakiwa iwe ni kwa nchi nzima, kutokana na ukweli kwamba, Tanzania imezungukwa na maji, ila tatizo letu ni jinsi ya kuelewa matumizi endelevu. Kwa hiyo, ni vizuri ku-*review strategic plan* ya maji katika nchi nzima. Chuo cha Maji kiimarishwe ili kitoe wahandisi makini wa kutosheleza mahitaji ya maji Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia ya umwagiliaji kwa ajili ya kilimo ni ya kale mno kihistoria, kwa nini sisi itushinde? Hata nchi jirani ya Misri ni mfano bora wa kujifunzia. Teknolojia ya mifereji ya umwagiliaji *(canals)*, ilianza yapata miaka 4,000 iliyopita. Historia inaonyesha kuwa, umwagiliaji ndio ulikuwa kitovu cha ustawi wa dola staarabu za kale kama Misri ya Kale, kandokando ya Mto Nile, Kaldayo kandokando ya mito Tigris na Euphrates. Mifano mingine ni tamaduni zenye uchumi mzito zilizojengwa kandokando ya Mto Ganges (India), Mto Yang-Ze-Kiang (China) na hivi karibuni Mto Mississippi (Marekani). Maendeleo ya Viwanda Ujerumani (*Ruhr Industrial Base*), kandokando ya Mto Rhine, ustawi wa kilimo, viwanda na miji kandokando ya Mto Thames (Uingereza).

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ndiyo yalikuwa nyenzo kuu ya Mapinduzi ya Viwanda Ulaya *(Industrial Revolution),* kati ya mwaka 1750 – 1850. Vile vile

Maendeleo ya Viwanda Marekani, yaani Kusini wakiwa wanazingatia kilimo na Kaskazini viwanda, vivyo hivyo Urusi na Uchina. Hii ndio sababu kubwa inayotulazimisha kusema kuwa, wananchi wanao uwezo wa kuchimba mifereji yao ya umwagiliaji mashamba *(canals),* kinachotakiwa ni mwongozo, yaani *guidance* toka kwa wataalam tu na huu ndio mchango wao na kuona kuwa wao ni sehemu ya umiliki huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maji ni sekta mtambuka, kwa hiyo, ni jukumu la kila Mtanzania kusaidiana na Wizara ya Maji ili kutimiza malengo yafuatayo:-

(a) Kuzuia na kudhibiti uharibifu wa mazingira hususan vyanzo vya maji;

(b) Kuhakikisha maji safi yanapatikana ili kupunguza magonjwa;

(c) Kutoa huduma ya maji karibu na makazi ya wananchi ili kupunguza muda unaotumiwa hasa na akina mama na watoto kufuata maji na hivyo kutoa nafasi zaidi ya kufanya kazi nyingine za kiuchumi na kijamii na kuongeza mahudhurio ya wanafunzi shuleni;

(d) Kuhakikisha kuwa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii zinapata maji kulingana na mahitaji. Hizo ni pamoja na uzalishaji wa nishati ya umeme, matumizi ya viwandani na kadhalika; na

(e) Kutoa hakimiliki ya ardhi kwa wadau mbalimbali ikiwemo wafugaji na wakulima ili kuendeleza maeneo yao ili yaweze kuzalisha kulingana na uchumi wa soko. Kwa hiyo, Serikali ni vema iangalie kwamba, uharibifu wa vyanzo vya maji unaofanywa na wakulima na wafugaji, basi umetokana na Serikali kutoangalia, ila wao washirikishwe vile vile kama wadau wa sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti ya Serikali, kuna mambo kadhaa ambayo yamepelekea kutofikia malengo ya Wizara ya Maji, ikiwa ni pamoja na udhibiti mbovu na ubadhirifu wa fedha zilizotolewa kwa ajili ya kuendesha miradi mbalimbali, hasa ile inayopelekwa Wilayani. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri, anaweza kujiuliza swali, ni kiasi gani cha fedha zimeshatolewa kuanzia mwaka 1961, kutekeleza miradi ya maji Tarime? Je, ni miradi mingapi imeshatekelezwa mpaka sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hali ikoje katika Wilaya nyingine? Katika vijiji 154 vilivyopo Wilaya ya Tarime, hakuna hata kimoja kinachopata maji safi!

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari, 2005 na Januari, 2006, jumla ya shilingi 131,230,000/=, ziliibiwa na watumishi wa umma katika Idara ya Maji Wilaya ya Tarime. Taarifa za wizi huu, zipo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, ana taarifa ya ubadhirifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ubadhirifu wa fedha hizo, taarifa inaonyesha kuwa, katika vipindi vyote vya huko nyuma, hali imekuwa ni hiyo hiyo. Taarifa za ubadhirifu huo zipo na zinafahamika, lakini wakati wananchi laki tano wa

Wilaya ya Tarime wanaendelea kupata taabu kwa kukosa huduma ya maji safi kwa miaka mingi, watumishi waliofanya ufisadi huo, bado wanaendelea kuneemeka. Tunataka tupate ufafanuzi kuhusu hii tabia ya ubadhirifu wa mali ya umma na wahusika kutochukuliwa hatua, wakati ushahidi upo wazi na hii ni sekta moja ya maji; je, sekta nyingine zikoje katika Tanzania nzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inapenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwa kuitembelea Wilaya ya Tarime mwisho mwa mwezi Mei, 2006. Nafikiri aliona hali halisi na jinsi ambavyo Taifa linapata aibu kwa watu wanaopakana na nchi jirani ya Kenya, wanavyovuka mpaka kwenda kufuata maji kwa majirani zao, kwa mfano, Vijiji vya Sirari, Masanga, Kegonga, Kogaja na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvunaji wa maji ya mvua, ni ukweli usiopingika kuwa, Tanzania katika Mikoa yote, ina kipindi kimoja au viwili vya mvua kulingana na jiografia ya Mkoa husika. Sehemu za kati ya nchi maji hayo ya mvua kiasi kikubwa hupotea bila ya kuvunwa kwa matumizi ya baadae. Kwa hiyo, imekuwa ni kawaida kwa Serikali pamoja na wananchi kushangaa ni kwa nini hili daraja limebebwa na maji lakini hakuna anayeshangaa kwamba, hayo maji yamekwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Serikali, inasema teknolojia hiyo ya uvunaji maji ya mvua itaendelezwa kwa Wilaya kama 33 ifikapo mwaka 2009. Hilo ni jambo zuri. Kwa hali ya kawaida, maji yanayotiririka *(run off water),* hayahitaji teknolojia ngumu, kikubwa ni kuchimba mashimo makubwa kwa ajili ya uhifadhi tu na hii inahitaji kuelimisha wananchi, hivyo sio suala la mpaka mwaka 2009, vinginevyo utakuwa ni ukiritimba usio wa lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuvunjwa kwa Mkataba na *City Water*. Moja ya maeneo ya kipaumbele katika Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2006/2007, pamoja na mambo mengine ni kulipa gharama za kesi kati ya Serikali na Kampuni ya *City Water Limited,* iliyokuwa ikitoa huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam na Kampuni mama ya *Biwater* ya Uingereza, kutokana na kusitishwa kwa Mkataba wa kutoa huduma za maji Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, wananchi hawajaelezwa gharama hizi ni kiasi gani katika Mahakama Kuu ya Uingereza? Je, Serikali haikujua athari hii wakati inachukua maamuzi? Gharama hizi za kesi ni sawa na miradi mingapi ya maji, kwa mfano, katika Wilaya ya Monduli? Tunataka kujua, tuna haki ya kujua na Watanzania lazima wajue jinsi ambavyo kodi zao zinatumika kulipia maamuzi mabovu ya Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji wa huduma za maji nchini ni moja ya suala lililo lalamikiwa sana na wananchi pia na wanaharakati. Serikali ilikuwa mtetezi mkubwa wa ubinafsishaji wa maji Jijini Dar es Salaam. Watanzania wanakumbuka jinsi ambavyo Serikali ilipotetea ubinafsishaji huu kupitia kwa Waziri wa Maji wa wakati huo, Mheshimiwa Edward Lowassa. Tulielezwa kuwa ubinafsishaji huu ni kwa faida ya nchi yetu. Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Maji wakati

Fulani, alinukuliwa na gazeti moja la Uingereza akisema yafuatayo: "Miundombinu ya maji ya miaka ya sabini ni mibovu, kuna upotevu mkubwa wa maji na *DAWASA* imeshindwa kukusanya maduhuli ya maji, hivyo, ni lazima ibinafsishwe kwa faida ya nchi." Hilo ni Gazeti la *The Guardian* la Juni, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, miezi miwili baadaye, *DAWASA* ikabinafsishwa kwa *City Water* kwa Mkataba wa miaka kumi. Miaka miwili baadae, *City Water* ikafukuzwa kwa kushindwa kazi na kazi hiyo kupewa Watanzania wanaoitwa Wazalendo mara moja. Je, Wazalendo hawa, hawakuwepo kabla ya kubinafsishwa kwa *DAWASA?* Uzalendo ni neno linalotumika kuficha maovu, kufuatia maamuzi mabaya ya Serikali? Maana hata katika ubinafsishaji wa Kampuni ya Ndege *(ATC),* tuliambiwa ni Uzalendo? Serikali ya CCM ina tafsiri mpya ya neno Uzalendo? Uzalendo umekuwa ni kuuza mali ya umma bila mpango, iliyopatikana kwa jasho la Watanzania kisha kuirudisha Serikalini baada ya hasara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la *City Water*, tunaitaka Serikali iwaeleze Watanzania yafuatayo:-

(a) Tarehe 1 Juni, 2003 *African Development Bank,* ilitoa taarifa kuwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, aliweka saini makubaliano na Benki hiyo ya mkopo wa dola za Marekani 47 milioni kwa ajili ya *City Water*. Nini hatma ya mkopo huu kipindi hiki ambapo Mkataba umevunjwa? *(Makofi)*

(b) Benki ya Dunia, Benki ya Rasilimali ya Ulaya *(European Investment Bank)* na Wakala wa Maendeleo wa Ufaransa *(Agence Française de Développement),* iliikopa Tanzania dola za Marekani milioni 98 kwa ajili ya ubinafsishaji wa *DAWASA*. Nini hatma ya mkopo huu? *(Makofi)*

(c) Serikali itoe tamko kuhusiana na fedha jumla ya Pauni 273,000 ambazo Idara ya Maendeleo ya Uingereza *(DFID),* ilitoa kwa kampuni ya Uingereza iitwayo *Adam Smith International* ili kutengeneza vipeperushi, nyimbo na matangazo ya *TV* ya kueneza sifa za ubinafsishaji *(Public relations materials including a pro-privatisation, pop video and song, to persuade a sceptical Tanzanian Public of the merits of privatisation)*. Fedha hizi ni mkopo au msaada na je, tumefikia mahali ambapo wageni wanatulipia kushawishi wananchi, masikini na wanyonge wa Tanzania, kukubali ubinafshaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika kwa Watanzania na zaidi viongozi wetu, kujifunza umakini wa kutambua maslahi ya Mtanzania, wakati wa kutoa na kusimamia maamuzi mbalimbali ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *City Water* ni moja ya mifano hai ya hasara za maamuzi ya kimahiri, yanayokosa umakini. Wakati Serikali yetu ilipokuwa ikijaribu kuutetea mradi huo wa kubinafsisha menejimenti ya mamlaka za maji nchini, viongozi wetu kwa umahiri mkubwa, walitetea maamuzi yao kwa kujiamini sana. Sasa hivi

Watanzania, wanabeba mzigo wa hasara za maamuzi yasiyo na maslahi kwa wananchi, yaliyofanywa na viongozi wao katika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanaomba kupata maelezo ya kina na ya kweli, yasiyo na chembe ya ubabaishaji, kuhusu masuala yafuatayo:-

(a) Ni akina nani waliohusika kuandaa, kusimamia na kuingia Mkataba huo kwa niaba ya Serikali na wananchi kwa ujumla na wanahusishwaje katika kupata ufumbuzi wa tatizo lilijitokeza baada ya Mkataba huo kuvunjwa? *(Makofi)*

(b) Ni masuala gani ya kiutendaji ambayo yamepelekea kuvunjwa kwa Mkataba huo na ni vipi yalikuwa na athari kwa Mtanzania?

(c) Serikali inawahakikishia vipi kwamba, uamuzi wa kuvunja Mkataba huo haukufanyika kwa kuangalia maslahi binafsi ya kisiasa ya mhusika mkuu wa suala hilo, yaani Waziri wa Maji wa wakati huo?

(d) Ni kiasi gani cha fedha, ambacho Serikali imekwishatoa ama inapaswa kutoa, kama gharama zinazohusiana na kuvunjwa kwa Mkataba huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanataka maelezo ya kina kuhusu njia zilizotumika kuhalalisha na kusimamia mabadiliko ya kiutendaji kutoka kwa *City Water* kwenda kwa Kampuni ya *DAWASCO*. Kuhusiana na hili, Watanzania wanataka kujua yafuatayo:-

(a) Je, ni sheria ipi imetumika kuanza rasmi kwa majukumu ya kusimamia menejimenti ya mamlaka ya maji safi na maji taka katika Jiji la Dar es Salaam kutoka kwa *City Water* kwenda kwa *DAWASCO?*

(b) Ni lini Serikali ilileta Muswada Bungeni kuunda *DAWASCO* kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya Umma; na kama *DAWASCO* imeanzishwa kupitia Sheria ya Makampuni *(Cap. 212),* ni kina nani wanachama (*subscribers*)? Tujibiwe haya ili kuepuka mambo ya Simu 2000, ambayo umiliki wake una utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kuendelea na suala hili la Bodi za Maendeleo ya Mabonde, ni wazo zuri lakini kinachohitajika ni utekelezaji, tukizingatia kwamba, mto kama Mto Rufiji ni *strategic* na hiyo bodi ilipoanzishwa mwaka 1991 haijafanya kazi inayotakiwa kufanywa mpaka leo. Kwa hiyo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania, faida ambayo mpaka sasa imeshapatikana kutokana na Bodi hizo au zimekuwa zikitumia fedha za walipa kodi bila kuwaonyesha Watanzania nini kinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa, hii ni bajeti ya kwanza ya Serikali ya Rais wa Awamu ya Nne. Kwa kuzingatia msemo wa wahenga kwamba, "mwanzo mgumu," Kambi yetu ilishauriana na kuamua kwa kauli moja kwamba, tutaiunga mkono Bajeti hii ya mwaka 2006/2007, kama tulivyothibitisha kwa

kura zetu hapa Bungeni. Aidha, tunafahamu kwamba, Serikali ya Rais wa Nne, imerithi mzigo mkubwa wa matatizo na kero zilizotokana na Awamu Tatu zilizotangulia. Kwa kipindi hiki tunadhani Awamu hii, itarekebisha udhaifu na makosa iliyorithi ili ifikapo kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2007/2008, kuwepo na mabadiliko makubwa ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu kama tunavyowashauri. *(Makofi)*

Ushauri mwingine wa mwisho, Serikali ibadilishe jina la Wizara ya Maji iwe ni *Ministry of Water and Sanitation,* yaani Maji na Uboreshaji wa Mazingira ya Maji, kwa sababu hilo linaenda sambamba ili iweze kusaidiana na Wizara ya Mazingira katika kuboresha vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kwanza kabisa, Kamati Ndogo ya Chama cha Wabunge Wanawake, inayohusika na kuandaa *Strategic Plan,* wanatakiwa wakutane bila kukosa saa saba katika Ofisi za *TWPG,* Mwenyekiti wao Suzan Lyimo ndiye anayetangaza.

Baada ya kusema hivyo, nina wachangiaji wengi sana. Kwa hiyo, tunakwenda kwanza kwa wale ambao hawakuchangia kabisa, halafu tutakwenda kwenye *list* ya wale waliochangia mara moja, kama nafasi itakuwepo tutakwenda kwa wale waliochangia zaidi ya mara mbili. Kwa hiyo, ambao hawakuchangia kabisa mpaka sasa ni Mheshimiwa Capt. George Mkuchika na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula. Halafu waliochangia mara moja ni Mheshimiwa Benedict Losurutia. Kwa hiyo, naanza na Mheshimiwa Capt. George Mkuchika.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kuwa mchangiaji wa kwanza katika Hotuba hii ya Wizara ya Maji. Pili, nilipojadili Hotuba ya Rais, niliwapongeza Viongozi Wakuu wa Serikali; Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika na Naibu Spika.

Leo naomba nichukue nafasi hii, kuwapongeza Viongozi wa Chama changu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Chama. Nampongeza Komredi Yusuf Makamba kuwa Katibu Mkuu wa CCM na pia nawapongeza Wajumbe walioingia katika sekretarieti bila kumsahau rafiki yangu wa karibu, Capt. Jaka Mwambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii, kukupongeza Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Maji na Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa kuchaguliwa kuongoza Wizara hii. Wananchi wa Newala, wameniomba nikufikishie salamu. Mheshimiwa Wasira, katika muda mfupi tu baada ya yeye kuteuliwa kuwa Waziri wa Maji, mimi na mwenzangu wa Tandahimba tulimwalika na hata kabla hajamaliza miezi miwili katika Kiti cha Uwaziri, alitembelea Newala. Ndio maana haya ninayoyasema leo, tutakwenda pamoja sana mimi na yeye, lakini angekuwa hajakwenda pengine ingekuwa vigumu kuelewa. Kwa hiyo, nampongeza sana, lakini nisije nikanogewa nikasahau zaidi nishukuru yale aliyoyaahidi. Tumeona hapa ahadi ya

kukarabati Mradi wa Maji wa Makonde, jinsi ambavyo upatikanaji wa maji utaboreshwa katika Wilaya ya Newala.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuchangia humu ndani na mkitaka kujua matatizo ya maji Newala, pamoja na kwamba mimi napenda kusema ndio maana sikuchangia Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo ndiko nilikotokea, nilikuwa nasubiri Wizara ya Maji ili niwasilishe kilio cha wananchi wa Wilaya ya Newala. Kwa hiyo, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia, kwanza, nataka nichukue nafasi hii, kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi, kilichonipa bendera yangu nibebe wakati wa kampeni na kushindana na vyama vingine. Pia napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Newala, kwa kunichagua kwa kishindo kwa kura 68,500 kuwa Mbunge wao. Kwa hiyo, ninaposimama hapa, muelewe nyuma kuna kura 68,500. Kwa hiyo, nataka niwashukuru sana wananchi wa Newala, huko mliko nawashukuru, hamkukosea na mimi nawaahidi sitawaangusha, kazi mliyonituma nitaifanya na hapa leo nimeanza kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wote humu ndani tumesoma, Wilaya ya Newala ipo katika *Makonde Plateau; what is plateau*? Wanasema *a rised flat piece of land, plateau* ni eneo ambalo limenyanyuka kule juu, halafu liko *flat*. Hicho ndicho chanzo cha matatizo ya maji katika Wilaya ya Newala, tupo juu. Nimeona wenzangu hapa mnasomewa visima vifupi vilivyochimbwa katika maeneo yenu, ardhi ya Wilaya ya Newala hakuna mahali unapochimba ukakutana na maji kwa sababu *water table is very low*. Kwa hiyo, Newala unapozungumza maji safi na salama, maana yake ni maji ya bomba. Sasa sijui Wabunge wenzangu wangapi hapa, ambao mnaishi katika Wilaya moja, lakini mnapata maji ya kunywa kutoka Wilaya jirani. Hiyo ndio Wilaya ya Newala, tunaishi Newala lakini tunapata maji ya kunywa katika Wilaya jirani ya Masasi, Lindi na Mto Ruvuma. Kwa hiyo, tatizo la maji Newala ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua tatizo la maji, wananchi wa Newala kabla hata ya mkoloni, baada ya kuunda *Newala District Council,* waliunda Kampuni ya Maji inayoitwa *Makonde Water Corporation*. Ikaomba mkopo kutoka Uingereza na ndani ya ule Mradi kulikuwa na *element* ya *cost sharing*, tulikuwa tuna-*share* uendeshaji wa gharama za maji. Tulikuwa tuna uhakika wa kupata maji, kupanua maji, kupeleka maji katika vijiji vipya kila mwaka. Baadaye baada ya Mradi kubinafsishwam nadhani hali ime-*deteriorate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani Mheshimiwa Waziri, ameeleza katika *speech* yake kwamba, Wilaya nyingi hapa nchini, upatikanaji wa maji umefikia asilimia 53.7, Wilaya ya Newala upatikanaji wa maji ni asilimia 22 tu. Kwa hiyo, mnaweza kuona jinsi gani Serikali ya CCM, inahitaji kuweka jitihada za makusudi, kuwanusuru watu wa Newala na Tandahimba ili upatikanaji wa maji nao ufikie angalau asilimia 45, hatuwezi kuwafikia waliofika asilimia 55. Mategemeo yetu 2007, bajeti itaongezwa zaidi ili tuweze kuongeza upatikanaji wa maji ili baada ya miaka mitano hiyo, tufike lengo la asilimia 65. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, aelewe kwamba, katika miaka mitano hii,

Newala wanatakiwa watutoe katika asilimia 22 ya upatikanaji wa maji na kufikia asilimia 65.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini matatizo ya maji Newala? Matatizo ya Mradi wa Maji wa Makonde ni kama ifuatavyo:-

Uchakavu wa mitambo na mabomba. Haya mabomba yaliwekwa enzi ya mkoloni, kabla ya uhuru, enzi ya *Makonde Water Corporation*. Wakati tulipomaliza Bunge nilikwenda kutembelea Mradi wa Maji wa Makondeko na Mkunya, ambako Waziri naye alikwenda, *pump* tatu kwa mpigo zinatakiwa ziwe zinafanya kazi ili ku-*pump* maji kwenda *Makonde Plateau*. Tulikuta ni *pump* moja tu inayofanya kazi, tena *pump* yenyewe imeazimwa Mitema. Tunaomba Wizara, ituongezee *pump* za maji ili maji yanayosukumwa yapate kuwa mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vingi vyenye mabomba hayafiki maji, yaani ukilinganisha na zile enzi za *Makonde Water Corporation,* mimi niliingia darasa la tano *Mnyambe Middle School* mwaka 1959, nafikiri inawezekana wengine walikuwa hawajazaliwa. Pale Mnyambe maji yalikuwa yanatoka tangini kila siku, shuleni kila siku, leo ni miaka arobaini na moja, maji hayatoki Mnyambe, Makukwe na katika Vijiji vingi sana. *Situation* yetu ni mbaya, tunahitaji kutazamwa kwa jicho la huruma. Vijiji vingine mabomba bado hayajafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu umeme. Naishauri Wizara badala ya kuiacha *Newala District Council* iwe inalipa *bill* ya umeme, nadhani Wizara ya Maji na Nishati muwe mnawasiliana wenyewe kwa wenyewe, kwa sababu tatizo mojawapo tunalolipata kule ni kuchelewa kulipwa watu wa umeme na wakati mwingine kusimamisha uzalishaji wa maji. Hili linatuathiri sana, tunaomba ulipaji wa *bill* za umeme ungechukuliwa na Wizara moja kwa moja, badala ya kupitishia Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie *morale* ya watumishi wa Mradi wa Maji wa Makonde. Nimewatembelea *morale* yao ipo chini kabisa, hawajapandishwa vyeo kwa muda mrefu, mmoja kati ya wakubwa pale alipandishwa cheo mara ya mwisho mwaka 1991, *graduate* toka 1991 mpaka leo hajapandishwa cheo *morale down*. Wale waliopandishwa vyeo wengine hata huo mshahara mpya hawajapata, lakini pia zamani Mradi wa Maji wa Makonde ulikuwa unapewa *OC* yake, tukipitisha hapa Bungeni fedha za *OC* za *Makonde Water Corporation* zilikuwa zinapelekwa kwa *Resident Engineer*, sasa hivi hazipelekwi. Kwa hiyo, unakuta kuna kazi kubwa ya yeye kuomba fedha kutoka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nasema, kama fedha imepitishwa za *OC* kwa ajili ya Makondeko, kwa nini isipelekwe katika Mradi ule ili waweze kuzitumia kwa urahisi zaidi. Mazingira duni ya kufanyia kazi ni tatizo mojawapo la Makondeko. Sikugemea *Resident Engineer* wa Mradi mkubwa kama wa Makondeko, awe na ofisi ambayo haijapakwa rangi, anatumia *manual typewriter*, ile kwamba ukitaka kupeleka nakala sita au saba mahali, unapanga *carbon* pale chini. *Engineer, graduate* kweli,

mpaka leo mnamfikisha hatua ya kutumia *typewriter manual,* mazingira ya Mradi wa Makondeko yanahitaji kutazamwa ili ku-*boost morale* yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka kusema kwamba, Newala tunaomba pampu mpya ya maji, tunaomba mitambo ikarabatiwe, tunaomba tupelekewe *OC*, kama ilivyokuwa zamani na maslahi ya watumishi yatazamwe. Lakini jitihada za makusudi zifanyike, ili kuhakikisha tunaongeza upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Newala.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimenong'ona na Mheshimiwa Waziri kwamba, Mradi wa Maji wa Makonde unahudumia Newala, Tandahimba na baadhi ya Vijiji vya Mtwara Vijijini. Kulikuwa na mawazo ya Serikali kwamba, muunde Bodi tatu. Sisi Newala tunasema hatuhitaji Bodi tatu, Newala, Tandahimba, *we have been always one* katika suala la maji. Tangu enzi za *Makonde Water Corporation*, tunaomba tuwe na Bodi moja tuzalishe pamoja, tukae pamoja kugawana maji na hilo litapunguza gharama za Serikali. Nataka nimalizie kwa kuishukuru Wizara, kwa ahadi ambazo zimo katika bajeti, tunashukuru Mradi wetu wa Makonde, utapatiwa fedha. Tumeona na Halmashauri ya Wilaya ina shilingi bilioni 213 wameombewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kukumbusha kuwa, Mheshimiwa Rais, alipokuja kuomba kura Newala katika Mkutano wa hadhara pale Mjini alisema hivi: " Nichagueni mimi Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Rais, mchagueni Capt. George Mkuchika wa CCM kuwa Mbunge, ili mimi na yeye tushirikiane kupunguza tatizo la maji la Mradi wa Makonde." Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ameshakuwa Rais na mimi ninayezungumza hapa, ndiye Mbunge wa Newala. Yale tuliyowaomba watu wa Newala, wameshatekeleza, sasa wanasubiri utekelezaji wa yale tuliyowaahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu siyo utaratibu mzuri kupigiwa kengele mara ya pili, hasa kwa Mbunge mstaarabu kama wa Newala, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kututembelea na kwa mambo mazuri aliyoyaandika ndani ya kitabu cha hotuba yake. Mategemeo yetu ni kwamba, mwaka huu Newala mambo yatakuwa mazuri. Watu wa Newala mliko huko mmenisikia, Mheshimiwa Waziri, nimemshukuru, nimemwomba maji na matatizo yenu nimeyasema. Kazi mliyonituma nimeifanya, huko mliko wazee wa Mkunya, Newala, Chahagara, Kitangari na Mnyambe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kutoa shukrani zangu nyingi kwa kupata nafasi ya kuchangia siku ya leo. Ni kweli nilikuwa sijachangia katika hotuba ya bajeti yoyote. Ni mara ya kwanza kusimama katika uchangiaji wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi zangu kwa Rais na Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi wa Taifa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho

Kikwete. Lakini pia natoa pongezi kwa Makamu Rais, kwa kuchaguliwa kwake na pia natoa pongezi kwa Waziri Mkuu, kwa kuchaguliwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri wa Maji na watendaji wote katika Wizara hii, kwa kuandaa hotuba ya bajeti hii, ambayo sasa tunaenda kuijadili. Pia napenda kutoa shukrani kwa Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kushughulikia tatizo la njaa, ambalo lilikuwa linaikabili Wilaya ya Bukombe, ambapo mara nyingi katika Mkoa wa Shinyanga huwa hatupati shida. Lakini mwaka huu tumepata shida kubwa na pongezi za pekee ziende kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Naibu Katibu Mkuu wake na watendaji wengine, kwa sababu niliwasumbua sana. Hata nikafikiri kwamba, inawezekana inakuwa ni tatizo kwako. Lakini lengo nilitaka tupate chakula na kweli walifanya hivyo na wananchi wa Wilaya ya Bukombe walipata chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa pongezi kwa uongozi wa Wilaya na Mkoa wa Shinyanga hasa *RC, RPC* na *OCD*, kwa matatizo wanayoendelea kuyashughulikia katika Wilaya ya Bukombe. Kwa sababu ni Wilaya ambayo kweli ina matatizo mengi, nafikiri hata nyie mnayasikia mara nyingi kwenye vyombo vya habari. Lakini pia natoa pole kwa wananchi wa Bukombe kwa tatizo ambalo walilipata hapo tarehe 11 Juni, 2006 la kutekwa. Matukio mawili au matatu yalitokea kwa siku moja katika msitu kwenye njia inayotoka Ushirombo kwenda Luzewe katikati kuna Msitu wa Hifadhi ya Taifa, pamoja na Halmashauri. Majambazi yalivamia magari pale mara mbili kwa nyakati tofauti. Lakini natoa pole kwa watu waliojeruhiwa na wenye vyombo vile ambavyo vilipata uharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa wananchi wa Bukombe, kwa kuamini kwamba, mimi ninatosha kabisa kuwawakilisha kuwa Mbunge wao katika Jimbo la Bukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka niende pia kwenye bajeti. Kwa kweli bajeti ni nzuri. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri nilivyoisikiliza na kuiangalia ni nzuri, kama inakwenda kweli kuzingatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ya Chama cha Mapinduzi kwamba, asilimia 90 ya maji safi yatapatikana mijini na asilimia 65 maji safi na salama yatapatikana Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuipongeza Serikali katika bajeti hii, nilikuwa nasikiliza hotuba zilizotangulia na hata nilipitia katika vitabu vya hotuba vingine, nimeona kwamba, kuna Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria ambao unakwenda mpaka Kahama. Nafikiri Serikali wakati inafanya tathmini ya Mradi huu, inawezekana sina uhakika Bukombe ilikuwa bado Kahama. Kwa hali hiyo, nilipojaribu kuangalia mradi huu unakwenda kuishia Wilaya ya Kahama, lakini Bukombe sasa si Wilaya ya Kahama tena ni Wilaya ya Bukombe inayojitegemea. Mimi nilikuwa ninajiuliza, je, Mradi huu kwa sababu pengine wakati tathmini inafanyika, Bukombe ilikuwa sehemu ya Kahama, Mradi huu utaendelea kwenda mpaka Bukombe au Mradi huu utaishia Kahama?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Bukombe mpaka sasa hivi kwa taarifa za tarehe 30 Juni, 2006 ni asilimia 34 tu ya wakazi wa Jimbo la Bukombe, zaidi ya 400,000 ndiyo wanaopata maji safi na salama. Lakini katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 10, amesema wastani wa asilimia 53. Katika hili ina maana ulinganifu wake bado. Mimi nikawa nafikiri asilimia hizi pengine labda wamechukua sehemu ambazo tayari Serikali imekwisha boresha maeneo yale. Bukombe ni eneo ambalo bado linahitaji sana kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba waweze kurekebisha na kuangalia. Kwa sababu Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria, ndiyo mradi pekee ambao unaweza ukatufikisha kwenye asilimia 65 na asilimia 90 katika Wilaya ya Bukombe. Nimejaribu kupitia Bajeti hii, Bukombe haimo. Kibaya sana kilichonisikitisha katika kitabu hiki, mipango ya Serikali ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2005/2010 na kitabu cha Mipango ya Wizara, kilichotolewa kwenye Mkutano Mkuu ukurasa wa 120, nimeona pia Wilaya hii na ndiyo ikaanza kunipa wasiwasi, wamesema kuna kufanya uchunguzi sanifu na kupanua Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria ili kuhudumia Miji ya Igunga na Nzega. Maji yatoke Kahama, yaende Igunga na Nzega, hii ni mipango ya miaka mitano ijayo, kwa maana kwamba Bukombe haimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilifikiri kwa mawazo yangu kwamba, Bukombe ilifanyiwa tathmini wakati ikiwa ndani ya Wilaya ya Kahama. Sasa nilifikiri pengine ndani ya Bajeti ijayo, Bukombe itakuwemo, kumbe tayari Wizara imeshaweka mikakati yake ya miaka mitano ijayo na Bukombe haimo. Umbali wa kilomita kama 100 kutoka Kahama kwenda Bukombe. Ninaomba Wizara ifanye *feasibility study* katika bajeti hii, ili iweze kuona mahitaji ya maji katika Wilaya ya Bukombe jinsi ilivyokuwa kubwa na jinsi tatizo linavyosumbua wananchi wa Wilaya hiyo. Lakini kwa sababu bajeti ya mwaka huu tayari imekwisha kuandaliwa, hatuwezi tukalazimisha kwamba, waandae bajeti upya. Ninachoomba sasa, wanapofanya *feasibility study,* basi mwaka 2007, uwepo mpango huo wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria kutoka Kahama kwenda Bukombe. Ninaamini maji hayo yatanufaisha Mji wa Masumbwe, ambao uko jirani sana na Kahama, maji hayo yatanufaisha Mji wa Ushirombo Makao Makuu ya Wilaya na Mji wa Unyovu. Hilo mimi nilikuwa naliomba hivyo, ikiwa mpango wa muda mrefu hasa kwa kuanzia mwaka 2007. Vinginevyo, Wilaya ya Bukombe suala la MKUKUTA katika Wizara ya Maji, halitakuwa limetusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuomba mapendekezo yangu kwa niaba ya wananchi wa Bukombe, Wizara ijaribu kuyaangalia kwa sababu katika bajeti ya mwaka huu nimeangalia Bukombe hatumo kabisa na matatizo ya maji tunayo makubwa. Tuangalie uwezekano wa kupata fedha za wahisani, zielekezwe katika Wilaya ya Bukombe. Kwa sababu wahisani wapo na nimeona sehemu nyingine wanapelekwa, sasa kwa nini Bukombe wasipelekwe na kwa nini Bukombe isahaulike na kwa nini Bukombe iamue kutengwa? Tunapokuja kujumlisha ule wastani, tunajumulisha kana kwamba, Bukombe imefikia asilimia 53! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara ijaribu kuangalia, tunavyo vituo ambavyo ni *centre* kubwa ambazo zinaweza zikahudumia watu hawa, pengine wakifanya upembuzi yakinifu ili tupate visima virefu katika maeneo hayo hayo ya Masumbwe, kwa

muda fupi huu katika maeneo ya Lubunga, Mbogwe, Lulembela, Ushirombo, Burenga, Unyovu na Mparahara. Hizi sehemu tukipata maji au visima virefu vya maji sasa hivi vinaweza vikasaidia na tukaweka pampu pale tukasambaza maji katika sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia napenda kuuliza na kusaidiwa na Wizara kwamba, kwa sababu MKUKUTA ni Mpango wa Serikali katika nchi yetu na Taifa letu. Wizara ya Maji inanufaisha vipi wananchi wa Wilaya ya Bukombe katika neno la MKUKUTA kama hatupati maji haya na kama visima virefu hatuna, ili tuweze kwenda sambamba na maendeleo ya maeneo haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bukombe ni eneo ambalo bado liko nyuma na kweli sikuchangia katika Wizara nyingine kama Wizara ya Fedha na Hotuba ya Waziri Mkuu, lakini si kwamba, sikuhitaji. Nilitaka nije nichangie kwenye Wizara ya Maji ili niweze kusema. Lakini si kwamba katika Wizara ambazo sitaweza kuchangia, sina shida nazo, kwa sababu kwetu ndiyo Wilaya pekee ambayo bado ina matatizo makubwa mno. Nafikiri katika Mkoa wa Shinyanga, mkiangalia mtaambiwa kwamba, Bukombe ndiyo sehemu yenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sana Wizara ituangalie na ifanye upembuzi yakinifu kwa bajeti hii, ili bajeti ijayo tuweze kupitia na kuona kwamba, Bukombe inapatiwa maji ya Ziwa Victorika kutoka Kahama kwa jirani zetu. Kitakuwa ni kitu cha kushangaza sana, kama maji yatashindwa kuja Bukombe, ambayo ni Wilaya Ndogo ya Kahama, yaende Nzega mpaka Igunga, yanaelekea kuja Dar es Salaam, wakati Kanda ya Ziwa bado hatujapata maji! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa ajili ya bajeti hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Wizara ya Maji ambayo ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, natoa pongezi kubwa kwa Waziri wa Maji, pamoja na Naibu Waziri wake, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na ni ngumu katika Taifa letu, ambacho ndicho kilio kikubwa cha Watanzania. Pili, nawapongeza vilevile wataalam wa Wizara hii, kwa kufanya kazi nzuri kuhusu suala zima la maji na ni kazi ngumu sana.

Mawaziri ambao wamepita katika Wizara hii, Mheshimiwa Edward Lowassa na Mheshimiwa Anthony Diallo katika kipindi kilichopita, tunawashukuru sana kwa kuweka mipango mizuri ambayo kusema kweli inaendelezwa sasa hivi kwa nguvu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie machache kuhusu Wilaya ya Kiteto, ambayo ina matatizo ya maji. Wilaya hii ni ya wakulima na wafugaji, lakini tatizo kubwa ni maji. Waheshimiwa Marais wote, walipokuja kututembelea kipindi kilichopita, wa Awamu ya Tatu na hii Awamu ya Nne, walikuwa wametoa ahadi kubwa

sana. Katika Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Rais, alianzisha Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kusikia kilio cha wafugaji na shida zake ikaundwa Wizara. Ilikuwa ni kumbukumbu tangu enzi ya Awamu ya Kwanza, wafugaji imekuwa ni kilio kwa sababu maeneo yake ni kame na yanaeleweka waziwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu hii ya Nne, Rais alikwenda Kilindi Wilaya ya Handeni. Kutoka Wilaya ya Kilindi sasa hivi kwenda Kiteto, alipofika Kijiji cha Rengatehe, alikumbana na wafugaji pale wakiwa mnadani, wakamlaki, akatoa ahadi akiwa juu ya gari. Aliwaambia wananchi wapumzike na wapige kura vizuri na wasikipigie kura chama chochote cha Upinzani, waipigie kura CCM, atawaletea maji na madawa ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika *record,* wananchi wamekipigia kura Chama cha Mapinduzi, akaja tena pale Kijungu akasimama, walikuwepo watu 2000, 3000, nguo zao nyekundu, kilio, akawaona akawapungia mkono, shida yenu maji, naelewa na madawa ya mifugo. Tupeni kura CCM, wamepigia kura Chama cha Mapinduzi. Sasa leo tunaenda tunazungumza nini? Unaangalia katika ratiba, tunaishukuru kweli Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, imefanya kazi. Nasema hivyo kwa sababu wamechimba visima 18 katika Wilaya ya Kiteto na pote maji yamepatikana na wanaendelea kufanya kazi hiyo nzuri tu. Natoa pongezi kwa kampuni mmoja inaitwa *Maji Take*, katika visima vyote 18, maji yamepatikana isipokuwa visima vinne maji hayatoshelezi. Kwa hiyo, nina hakika Wizara hii ikikazana katika Wilaya ya Kiteto, itaondoa shida ya maji, watafikia lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaombeni sana katika hili, tuna tatizo katika hivi visima 18, kuhusu miundombinu. Kuna makampuni ambayo kwenda kujenga miundombinu ya maji kufika pale, ndiyo wanakwenda kwa ulegevu, wanatengeneza miradi ya maji hawatekelezi. Tangu mwaka 2005 mpaka sasa hivi, tumechimba na wanajaribu sasa hivi kumalizia malizia na tatizo lao ni fedha. Kuna mvutano kati ya Wizara sijui hawatumi fedha huko Wilayani na kadhalika. Msimamie kabisa, leo mmechukua mradi huu katika nchi nzima, kila Wilaya Vijijini 10, licha ya zile Wilaya 40 za majaribio ambazo wamefanya vizuri. Sasa wakienda kwa namna hii, hamtatekeleza hii miradi kabisa. Bora fedha tugawiwe zote zije Wilayani, tuzisimamie kama Miradi mingine. Lakini hili suala la kutuambia *World Bank* na nyie huko katika Wizara, mtakwamisha kabisa Mradi huu usiendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ambao tulikuwa kwenye Wilaya zile 40 za majaribio, tunaombeni sana msimamie na naomba mje Kiteto, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wengine wote.

Suala la pili ni la suala la Bodi ya Maji katika Mji wa Kibaya, mmeongeza Bodi toka 39 mpaka 60 katika kila Wilaya. Kuna tatizo, kwa nini Bodi ya Kibaya haijaundwa? Tumetuma mpaka na majina, watu wamekaa na Mji wa Kibaya una shida ya maji, hakuna hata utaratibu. Mji mzima, nikipita nashindwa kupitia katika mitaa mingine, kwa sababu ya ndoo kulundikana. Kila wakati wa Uchaguzi, watu wa Kibaya wananichagua kwa

imani yao kubwa, wakiteseka na wakinipenda, kwa nini hamji kuwaangalia kujua wana shida gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuwashukuru wananchi wa Kiteto, kwa kunichagua kwa vipindi vinne mfululizo, kwa tabu kama hiyo hiyo, kwa ajili ya mapenzi. Nawaombeni mnisaidie Mji wa Kibaya upate maji. Vijijini sasa hivi, nina uhakika wanaweza wakapata maji, lakini mjini hakuna maji. Ninawashukuruni sana pale Mji Kibaya, wafadhili hawataki Mjini, wanapata Vijijini. Ndiyo tabu tuliyonayo sisi, hakuna mfadhili yeyote anayetaka kuwahudumia watu wa Mjini, ni Dar es Salaam tu na Makao Makuu ya Mikoa. Kule Wilayani wanatuchenga, ndiyo maana tuna matatizo, kule Masasi, kila mahali, mpaka Rais anakwenda kuwaombea fedha Makao Makuu ya Wilaya. Nawaomba sana, muangalie Kiteto. Kwa hiyo, naomba katika suala la Bodi, kazi ifanyike. Kwa hiyo, naomba muangalie suala la Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie kwa kusema kweli ni suala la kushirikiana na Wizara ya Mifugo. Kuna ari sasa, nimeona mabwawa na fedha nyingi za mabwabwa na tuna maeneo. Katika vurugu hii, lakini siyo Kiteto tu, nikizungumzia katika nchi nzima na katika mtazamo mzima wa ufugaji katika nchi hii. Naomba Wizara ya Mifugo na Wizara ya Maji, wakae kweli kikamilifu ili waweze kutenga maeneo mazuri ya kilimo katika maeneo. Kwa sababu haiwezekani kabisa, Kiteto nzima, iwe maeneo yote ni malisho ya mifugo tu, kuna wakulima kule. Tuna maeneo ya wafugaji na tuna maeneo ya wakulima. Sasa tusipotenga huduma za maji katika maeneo ya wafugaji, halafu maeneo ya wakulima, tunakuwa tunawagonganisha watu na tutapata matatizo makubwa, jinsi ya kuongoza watu. Kwa sababu wanachanganyika, hatuwatengei maeneo ya huduma katika sehemu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaombeni sana kwamba, kwa eneo la Kiteto sehemu kama Tarafa ya Makami ni ya wafugaji watupu, tengenezeni mabwawa, malambo na kadhalika. Tarafa ya Kijungu, robo tatu yote ni wafugaji. Sehemu za Mrutangosi zile ni mbuga zote za wafugaji wekeni mabwawa. Sehemu za Matoi na sehemu nyingine ambazo zinalisha Dar es Salaam, kwa ajili ya mahindi na kadhalika, nao wakae wasisumbuliwe na wafugaji ili waweze nao kuzalisha mazao ya kulisha wananchi wengine ambao hawana chakula. Sisi tunataka wote wafugaji na wakulima katika Wilaya ya Kiteto, wakae vizuri na wakae katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hayo yote yanawezekana kabisa, ukinipa mabwawa matano au sita, tumetenga pale. Sasa hivi tuna utaratibu mzuri wa matumizi bora ya ardhi. Kwa hiyo, tunawaombeni sana, kama ikiwezekana Mheshimiwa Waziri wa Maji na vilevile na Waziri wa Mifugo, wafike Kiteto waanze sasa kutenga maeneo hayo na kuweka huduma za maji ambazo zinawezekana kabisa na fedha mlizotutengea ni safi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nitoe pongezi zangu, itakuwa ni vibaya sana kama sitamtaja Mhandisi wa Maji wa Kiteto, kwa kweli *Engineer* wangu,

amefanya kazi nzuri sana na watumishi wake wengine. Kwa hiyo, napenda niwapongeze kabisa na uongozi wote wa Kiteto, waweze kusimamia miradi hii na wakati nitakapokwenda tutasaidiana wote. Nina hakika kwa kipindi hiki, tunaweza kutatua matatizo makubwa ya maji katika Wilaya ya Kiteto. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuzungumzia Wizara hii ya Maji. Pili, napongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri wake na watendaji wake wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa Bajeti hii kwa mwaka huu wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, najielekeza katika upande wa maji kwa ujumla. Maji ndiyo msingi mkubwa wa maendeleo katika maeneo mbalimbali, maji ndiyo msingi mkubwa wa uhai kwa maisha ya binadamu, mimea na vitu mbalimbali hapa duniani na pia maji ndiyo kichocheo kikubwa cha kuweza kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa yote haya niliyoyazungumzia, utaweza kuona kwamba, maji ndiyo kiungo kikubwa katika uhai wa binadamu. Bila maji, tunaweza tukalalamika mara nyingi tuna njaa, bila maji hatuwezi kuishi tunakuwa hatuna uhai. Kwa hiyo, tunachokizungumzia hapa ni kitu muhimu sana katika Serikali yetu hii. Naiomba Serikali, itilie maanani vilio vyote vya Waheshimiwa Wabunge, waliomo humu ndani, wanapolizungumzia suala la maji, isionekane kwamba, kila mtu anavutia upande wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia sehemu moja katika Tanzania yetu hii, nayo ni Wilaya Geita. Wilaya ya Geita ina idadi kubwa sana ya wananchi. Sensa ya mwaka 2002 ilionyesha kwamba, Wilaya ya Geita ina idadi ya watu zaidi 700,000. Katika wakazi 700,000 hao, Mji wa Geita una zaidi ya watu 50,000, kati ya watu hawa wanaopata maji safi na salama ni asilimia tano tu, wengine wote waliobaki hawana maji. Hii asilimia tano imetokana na juhudi ambayo imefanywa na *Plan International*. Napenda niipongeze kabisa *Plan International,* kwa kazi kubwa wanayoifanya, kuweza angalau kuleta huduma ya maji kwa wananchi wa Geita. Wamefanya kazi kubwa, wameweza kutekeleza Mradi huu katika Kata tatu; Kata ya Karangara, Kata ya Kasamwa na Kata ya Ihanamiro. Kata hizo tatu, ndizo zinaweza zikapata maji kutokana na visima. Lakini ukiangalia maji ya Geita, yaliyo mengi yote yamejaa zebaki, kutokana na uchimbaji na kutokuwa na utaalamu wa kutumia hii zebaki. Kwa hiyo, maji mengi yamejaa zebaki, ina maana wananchi wa Geita waliopo, hata kama kuna maji lakini maji yake si salama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara katika mikakati yake, nimeangalia katika kitabu hiki nimeona kama katika ukurasa 22 hivi, wamesema miradi ambayo itatiliwa maanani. Lakini nikikumbuka tangu mwaka 2003, Wizara hii inaniambia kwamba, Wilaya Geita au Mji wa Geita, utapelekewa maji na kila siku wanasema

upembuzi yakinifu, mwaka 2003, mwaka 2004, mwaka 2005. Lakini mwaka huu hata ile fedha ya upembuzi yakinifu haikutengwa.

Sasa naona kwamba huu mradi unaweza ukaanza kusahaulika, ingawa amesema kwamba mradi huu utategemea utafutiwe pesa, sasa tunaingia katika ahadi, hatujui kama zile pesa zitapatikana au hazitaweza kupatikana. Naomba kabisa Wizara ya Maji uiangalie kwa macho mawili Mji wa Geita, upewe maji bila kuangalia nini, kwa sababu ninavyosema kwamba wananchi wa pale Geita wanazidi kupata matatizo kutokana na maji wanayotumia si salama. Wote hapa ni mashahidi, Wilaya ya Geita ina machimbo mengi sana na kupata dhahabu lazima utumie Zebaki na Zebaki inaweza ikapenya ikaingia kwenye visima virefu kwa hiyo, tunajikuta kwamba wananchi wa Geita Mjini na sehemu nyingine tunatumia maji ambayo si salama. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika utaratibu huu naomba hata vile visima vilivyoko pale tuvihesabu kwamba hatuna maji ambayo yanaweza yakawatosheleza wananchi au maji ambayo yako safi. Ombi, naomba kabisa Wizara ifanye mpango madhubuti kama walivyofanya sehemu nyingine. Kwa sababu kuna sehemu ambazo mnasema kwamba kuna Wilaya ambazo zitapelekewa maji lakini Wilaya ya Geita haijapelekewa. Najua ni utaratibu ambao mmeuona kwamba kupeleka maji Wilaya ya Geita gharama yake ni kubwa, basi tulichukulie kama ni janga la Taifa. Pelekeni maji kama tulivyopata njaa, vunjeni miradi mingine lakini angalau Geita tupate maji safi na salama na kuweza kuwanusuru wananchi wa Geita walio wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumengalia sana katika upande wa maji, lakini walipokuwa wanazungumza wamesema kwamba kuna miradi ambayo wanaifufua, miradi ya vijijini. Pili, wamesema kwamba kuna miradi ambayo itaanzishwa kwa vijiji kumi katika Wilaya. Mimi ninachoomba katika Wilaya nyingine hasa Wilaya ya Geita ina miradi iliyokuwepo, ilikuwa imeletwa na Serikali. Miradi ambayo haikuwa shirikishi, sasa hivi tumeamua Serikali yetu iwe shirikishi kwa wananchi. Sasa miradi iliyokuwepo ilikuwa ni ya Serikali ilikuwa haiwashirikishi wananchi. Sasa naomba miradi hiyo ifufuliwe na ikifufuliwa ikabidhiwe kwa wananchi. Kwa sasa ilivyobaki vile haifanyi kazi kabisa. *(Makofi)*

Kwa mfano, kuna miradi mingi si kwa Geita tu, kwa mfano hata Sengerema kuna mradi wa Nyamazugo na Katunguru, kwa Geita kuna mradi wa Nyakagomba, Nyamtukuza, kuna mradi wa Kasamwa, Kalumwa, Nzera na kuna mradi wa Kazirankanda, Ukerewe, hiyo miradi naomba kabisa ifufuliwe kwanza badala ya kuangalia katika vijiji ambavyo tunataka kuvianzisha. Kwa sababu tunaanza upya kitu cha kuanza upya kina gharama kubwa, lakini kuna miundombinu ya maji ambayo iko katika vijiji hivi au katika miji hii. Kwa nini Serikali isitoe pesa, pesa zile zikafufue hii miradi, najua kabisa inaweza ikasaidia wananchi katika eneo lile kwa hali ambayo inaweza ikaridhisha. *(Makofi)*

Kwanza kabisa katika maeneo yale kuna watu wengi wanaishi katika sehemu hizo, kwa mfano Kasamwa. Kasamwa ni *centre* ambayo ni kubwa tu, katika bajeti ya mwaka jana walisema walikuwa wametenga shilingi milioni 30 kwa ajili ya kufufua

mradi wa Kasamwa lakini hadi leo hatujaona fedha hizo zimeenda wapi. Sasa basi naomba miradi hii ambayo ilishaanzishwa lakini utekelezaji wake haukuwa mzuri zaidi, naomba Serikali itilie maanani miradi hiyo badala ya kuanzisha miradi mipya kuliko kuanzisha hiki tunaacha, hiki kinakuja tunaacha, lakini hii tukiiufufua basi wakabidhiwe wananchi. Wananchi wakikabidhiwa watajua nini cha kufanya kama kuna mapato basi wao wenyewe watakusanya kuweza kuiboresha hii miradi ili isiweze kufa tena, wakabidhiwe wananchi katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naliona kwamba inaweza ikasaidia sana kuweza kuboresha maeneo ya maji katika Wilaya yetu ya Geita hasa mradi huu wa Nyamtukuza, umeanza siku nyingi lakini hauendi, mradi wa Nyakagomba nimeuona kwenye bajeti. Nimshukuru tu Naibu Waziri alipokuja Geita wananchi walisikitika kwa kweli, kwa sababu hakukaa kuzungumza na wananchi wa Geita Mjini ili waweze kumwambia tatizo lao la maji nini. Alienda Nyakagomba, aliona ule mradi lakini ule mradi na wenyewe una gharama ambayo kwa kweli ni kubwa. Sasa basi naomba wakati wanatekeleza hiyo mradi wa Nyakagomba basi uende sambamba na miradi ya Nyamtukuza, Kasamwa, Kalumwa na mradi wa Nzera. Miradi yote hii ilikuwepo katika Wilaya yetu. Sasa basi naiomba Wizara itekeleze haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la malambo, nashukuru sana Serikali kwa kubuni utaratibu huu. Utaratibu huu ulikuwepo siku nyingi na wananchi katika maeneo yetu walikuwa wanajua kabisa kwamba mradi wa malambo ndiyo ukombozi wa maji katika maeneo yale. Si kwa ajili ya mifugo tu na pia kwa maji kwa ajili ya binadamu na umwagiliaji wa kilimo. Sasa malambo mengi yaliyochimbwa yalichimbwa kwa mkono na katika Wilaya ya Geita kila Tarafa ina malambo. Sasa tunaposema tukaanzishe malambo mengine katika maeneo ambayo malambo yapo tangu siku nyingi, naiomba Wizara katika eneo kama Geita ipeleke pesa kuweza kuyafufua malambo yaliyokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malambo haya yapo katika kila tarafa mengine yako katika kila Kata. Kwa mfano, lambo la Lwenge liko Kata ya Kamhanga, lile bado linaendelea, lina maji safi. Lakini kuna lambo la Bulela liko Tarafa ya Kasamwa lambo la Kasamwa lenyewe lifufuliwe. Likifufuliwa lile linaweza likawasaidia wananchi wa Kasamwa pale pale lakini kuna vijiji kama sita ambavyo vinaweza vikafaidika na lambo lile. Si hivyo tu, naomba kabisa kwamba malambo haya yatakapofufuliwa najua wakulima na wafugaji watakaa sehemu moja ambayo hawataweza kuwa na mgongano. Kumekuwa na mgongano kati ya wafugaji na wakulima kwa ajili ya maji, maji yamekosekana katika maeneo, wafugaji wanaamua kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kutafuta maji. *(Makofi)*

Sasa yakiboreshwa haya malambo katika maeneo husika najua kabisa wakulima na wafugaji wanaweza wakakaa sehemu moja. Tatizo linalotupata ni moja tu, tunashindwa kuwathamini wafugaji, tunaona kama ni wavamizi, sio wavamizi. Mheshimiwa Waziri wa Maji najua wewe ni mfugaji kwa nini sasa usiboreshe mabwawa haya katika maeneo yale? Maeneo haya yalikuwa na mabwawa, yarekebishwe tu ili kuleta tija katika maeneo husika. Maeneo haya ni mazuri kabisa, Geita yapo mabwawa lakini yamekosa ule ufuatiliaji tu na ninachokiomba kama nilivyosema katika mradi huu

wa maji katika miji basi na mabwawa haya yakabidhiwe wananchi. Wanachi waambiwe hili ni bwawa lenu wamilikishwe kwa hiyo, kikawa ni chanzo cha mapato katika bwawa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanatoka sehemu ya mbali kuja kunywesha mifugo yao basi wataambiwa watoe hata kitu kidogo na mimi najua kabisa kwamba wananchi wanaweza wakafanya vile na kuna maeneo fulani ambayo ninauhakika, kwa mfano lambo la Rwenge wamefanya hivyo. Wananchi wa maeneo yale wanaotunza hilo lambo wamepata chanzo cha mapato na huu ndiyo MKUKUTA. Sasa kwa nini sasa hivi tusi-*invest* hizo pesa za malambo tukafufua malambo yetu ambayo yalikuwa yameachwa sasa tuanze kuyafufua, tuyaweke katika uhai ili kuweza kuleta tija kwa ajili ya wafugaji wetu na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda niunge mkono kwa asilimia mia moja hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watalaam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti. Lakini wanajitahidi kuboresha huduma za maji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze na hili la kuboresha huduma za maji katika miji midogo tisa, Serikali ina mpango mzuri sana wa kuboresha huduma ya maji katika miji midogo tisa na miji hiyo naomba niitaje kwa ruhusa yako, kuna Utete, Ikwiriri, Kibiti, Turiani, Mvomero, Kilosa, Gairo, Kibaigwa na Mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utasaidia sana kuboresha huduma za maji katika miji hii. Lakini kasi ya mradi huu unakwenda taratibu sana, kwa sababu zifuatazo, kwanza ni miji midogo tisa, lakini mkandarasi aliyeteuliwa ni mmoja, kwa hiyo, inakuwa ni vigumu kuweza kukamilisha miradi hii mapema. Na Mheshimiwa Waziri anajua, nilishamweleza Naibu Waziri, na nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri ametembelea Wilaya ya Mpwapwa hivi karibuni, huu mradi utachukua muda kukamilika na mji wa Mpwapwa una matatizo makubwa sana ya maji na wananchi wa mji wa Mpwapwa walikuwa wanategemea mradi ukikamilika basi tuweze kuboresha huduma ya maji katika mji wa Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mji wa Mpwapwa vyanzo vya maji vya mji wa Mpwapwa ni kuanzia Mwaka 19 vingine na tano, baada ya kuanzisha kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, basi ndio tukaanzisha na Wilaya ya Mpwapwa pamoja na vyanzo vya Mayawile na kuchimba visima virefu vitatu. Sasa idadi ya watu wakati huo ilikuwa 3000 kwenye miaka ya 1950 kurudi nyuma walikuwa watu 3000, sasa hivi mji wa Mpwapwa unakadiriwa kuwa na watu zaidi ya 60,000. Lakini vyanzo vya maji bado ni vile vile, kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu tumeshaahidi,

wakati wa kampeni mwaka jana Mheshimiwa Rais alipofika pale wakati wa kampeni aliwaahidi wananchi wa Mpwapwa kwamba tatizo la maji katika mji wa Mpwapwa analifahamu vizuri sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hili la kutuongezea mkandarasi mwingine na tuelezwe kuna matatizo gani? Kwa nini amepewa mkandarasi mmoja miradi yote miji midogo tisa, atakamilisha lini kazi hii? *(Makofi)*

La pili napenda niishukuru na kuipongeza Serikali kwa muda mrefu nimekuwa nimelalamikia huduma ya maji katika vijiji vya Chiseyu, Sazima, Makutupa, Lupeta, Igoji Kusini na Mazae. Lakini hivi sasa niishukuru Serikali kwa awamu ya kwanza ya mradi huu wa Benki ya Dunia kushirikiana na Serikali yetu, awamu ya kwanza vijiji 10 sasa hivi vinapata huduma ya maji katika Wilaya ya Mpwapwa. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali na awamu ya pili vijiji vitano kikiwemo kijiji cha Chiseyu ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri ametembelea pale hivi karibuni. Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwamba imetekeleza lile ombi langu kwamba ni vizuri sasa wananchi wa vijiji hivyo wapate huduma ya maji, maji ndio uhai wetu, maji ndio uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni dawa za kusafishia maji, maji yakichafuliwa na viini vya magonjwa ni hatari kwa binadamu. Labda wataalam watanielewa, tuna njia za kusafisha maji, maji ya chemichemi, haya *gravity scheme*, lakini kwa mfano Mpwapwa, kuna chanzo kimoja cha Mayawile ambacho maji yake ni chemichemi. Sasa kiutaratibu, kiutaalam maji hayawezi kutoka kwenye chemichemi yakaingia moja kwa moja kwenye bomba, lazima yasafishwe na dawa, lazima tujenge Mpwapwa kuna matenki manne yalijengwa kwa ajili ya kusafisha maji. Maji yanapotoka kwenye chemichemi, lazima yanaingia kwenye tenki moja ambayo tunaita *sedimentation tank.* Sasa tenki lile takataka zote zinazama chini, tukitoka hapo tunakwenda kwenye *storage process,* maji meupe pale baadaye tunakwenda tenki la tatu, *filtration tank process* mwisho, baadaye tenki la mwisho *recronation non process*.

Sasa maji kwa mfano yakitoka kwenye chemichemi, yanaingia moja kwa moja kwenye bomba, bila kusafishwa, bila kuwekwa dawa, hii inaweza kusababisha magonjwa ya kuambukiza kama homa ya matumbo *(typhoid fever)*. Kwa sababu maji yanapopita, sehemu nyingi kuna na vinyesi vya wanyama, vinyesi vya binadamu, kwa hiyo, kuna kuwa na *fickle condemnation.* Sasa ile *fickle condemnation* ndio inasababisha magonjwa yanayosababishwa na maji *(water body diseases)*.

Kwa hiyo, ni hatari katika maisha ya binadamu na magonjwa hayo kwa mfano ugonjwa wa homa ya matumbo, unasababishwa pamoja na kwamba ni kula vyakula vichafu vichafu vinavyochafuliwa na viini na lakini vile vile kunywa maji yaliyochafuliwa na viini tunaita *oral fickle transmission*, kwa hiyo, hiyo ni hatari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba vizuri Wizara ya Maji, ni kweli wataalam wote wako Halmashauri za Wilaya, lakini kazi ya Wizara ni sera na kutoa miongozo, mtutafutie dawa kwa ajili ya kusafisha maji. Hii itasaidia kuzuia magonjwa ya mlipuko ya magonjwa kama vile *typhoid,* magonjwa ya kipindupindu na mambo mengi. Kwa hili nilikuwa naishauri Wizara isaidiane na Halamshauri za Wilaya, lakini nichukue nafasi hii

kumpongeza Mhandisi wetu wa maji wa Mkoa, kumpongeza Mhandisi wa maji wa Wilaya na watalam wake wanafanya kazi nzuri, kuna mradi wa *AWAMA British Water Aid,* wanafanya kazi nzuri sana na hivi karibuni Wilaya ya Mpwapwa tunapata maji zaidi ya asilimia 70. *(Makofi)*

Suala la ukame mwenzangu Mheshimiwa Ernest Mabina amelizungumzia, lakini tumeshaishauri Serikali kwamba maeneo ya ukame ambapo hakuna uwezekano wa kuchimba visima virefu au visima vifupi mtuchimbie mabwawa. Mabwawa yatasaidia maji kwa matumizi ya binadamu lakini vile vile na mifugo yetu. Ni kweli tunapata fedha kwa ajili ya kuchimba mabwawa lakini fedha hizo ni kidogo sana pamoja na kwamba kusaidiwa na nguvu za wananchi na nini. Kwa hiyo, naomba zingetengwa fedha za kutosha ili kuhakikisha kwamba tunachimba mabwawa, mabwawa yatasaidia sana matumizi ya maji kwa binadamu pamoja na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali, nilikuwa nasoma kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Maji. Katika mwaka huu wa fedha 2006/2007, nimeona Mkoa wetu wa Dodoma umetengewa karibu shilingi milioni 546 na Wilaya yangu ya Mpwapwa tumetengewa shilingi milioni 84 kwa ajili ya huduma za maji. Kwa hiyo, hii nakushukuru sana na nashukuru Serikali, fedha hizi zitaboresha huduma ya maji katika eneo letu la Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala zima la uvunaji maji. Sasa hivi tuna shule za sekondari kila Kata, kwa hiyo, ninawashauri wataalam wafike katika shule hizo ili kuelimisha wananchi jinsi ya kuvuna maji. Haya maji yatasaidia kwa matumizi ya shule zetu za sekondari ambazo zimeanzishwa hivi karibuni. Tumeshawahamasisha wananchi, Serikali pamoja nguvu za wananchi ili wahakikishe kwamba huduma ya maji inaendelea kutolewa katika maeneo yale ambayo hakuna maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho napenda niwahakikishie wananchi wa vijiji vya Mima, Chunyu, Ihoma na Kimagai kwamba katika mpango huu wa mradi wa maji wa Benki ya Dunia ikishirikiana na Serikali yetu kwamba wamewekwa kwenye mpango huu wa awamu ya tatu. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie mimi kama Mbunge wao kwamba katika mpango wa awamu ya tatu watapata huduma ya maji. Lakini wote tunafahamu sera ya maji ni lazima tuchangie mifuko ya maji na nashukuru hivi sasa ninavyozungumza wameanza kuchangia mifuko ya maji. Kwa hiyo, ninahakika baada ya mwezi wa kumi au kumi na moja tutakuwa tumeshafikisha kiasi kizuri, kwa hiyo, naomba wapate huduma za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru kwa kunipa nafasi na nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na naiunga mkono hoja hii isipokuwa naomba maelezo kwa hili la utekelezaji wa kuboresha maji katika miji midogo tisa, kuteua mkandarasi mmoja, kigezo kilichotumika kuteua mkandarasi mmoja ni kipi na lazima tuwe na *time frame* ni lini mradi huu utakamilika kwa sababu tunahitaji huduma ya maji Mji wa Mpwapwa. Ahsante sana na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu au anayefuata, kama anaweza kuzimudu kuchangia kwa dakika hizo kumi zilizobaki?

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia mchana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Baada ya kusema hivyo naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.49 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mezani ya Mheshimiwa Waziri wa Maji. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri waliyoifanya iliyowezesha kutoa hotuba ya bajeti ambayo inajadiliwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuungana na wasemaji Waheshimiwa Wabunge, waliotangulia kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nitoe maoni yafuatayo katika hoja hii iliyowekwa mezani. Kwanza kabisa naomba nichangie kuhusu mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria. Naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Tatu, kwa sababu za kimsingi zifuatazo, Serikali ya Awamu ya Tatu, iliamua kujenga mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kutokana na fedha za ndani ya nchi yetu. Naipongeza kwa sababu imetupa heshima kubwa Watanzania. Kumbe tukitaka na kuthubutu tunaweza kufanya mambo makubwa kama mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria. Kwa hiyo, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tatu. *(Makofi)*

Vile vile naomba nimpongeze kwa namna ya kipekee kutoka katika sakafu ya moyo wangu, Waziri wa Maji wa awamu ya tatu, kwa sababu wakati wa uamuzi wa kujenga mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, ni kipindi kile kile tulikuwa na majadiliano ya matumizi ya maji ya Mto Nile na nchi 10 za Afrika. Kwa hiyo, ilikuwa ni kipindi tosha kuamua kujenga mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwa fedha za ndani ya nchi. Lakini nampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa jinsi alivyotetea mradi huu kwa busara na hekima kubwa na mpaka sasa mradi huo unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji toka Ziwa Victoria, utakapokamilika vijiji 54 vya Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Mwanza vitapata huduma ya maji safi na salama, ni kitu chema. Lakini naomba Serikali katika awamu inayofuata kuna kata ya Bunambiu Jimbo la Kishapu, Vijiji vya Mwanhiri, Itongwitale na Kijiji cha Bunambui

ambavyo havina chanzo kingine cha maji kilichokaribu na chenye uhakika. Lakini bomba la maji la mradi wa Ziwa Victoria, liko karibu ukilinganisha na chanzo ambacho sasa hivi vijiji hivyo vinapata maji. Kwa hiyo, ni busara tu niombe Serikali kupitia Wizara ya Maji ione umuhimu kuvipatia huduma hivyo vijiji vya Kata ya Bunambiu kutoka katika bomba la maji kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwishahamasisha wananchi katika vijiji hivyo, mimi na Mheshimiwa Diwani Samson, ili tuweze kupata huduma na wananchi wameshakuwa tayari. Kwa hiyo, naomba Serikali iwaunge mkono wananchi na naomba Serikali kupitia Wizara ya Maji, ipeleke wataalam iweze kubaini uwezekano huo wa kupata maji kutoka katika bomba la maji la mradi huo mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie vile vile mradi wa maji safi na usafi wa mazingira. Kama tulivyoeleza katika hotuba ya bajeti, mradi huu kwa sasa utagusa Wilaya zote nchini. Naomba niipongeze Serikali kwa uamuzi huo wa kuamua kwa makusudi kwamba mradi huu sasa uenee katika Wilaya zote nchini. Ni jambo la kuipongeza Wizara. *(Makofi)*

Lakini naomba nizungumzie uzoefu wa awamu iliyopita ya mradi na kuiomba Wizara ifanye jitihada za kurekebisha kasoro hizo. Mradi huu unatekelezwa na Benki ya Dunia. Katika awamu ya kwanza kulikuwa na matatizo makubwa ya kucheleweshwa kwa fedha kufika kwa walengwa wa mradi. Ilikuwa inachukua muda mrefu na wakati mwingine fedha zinafika wakati wananchi wamechoka sana kusubiria. Wananchi wanakuwa wameshahamasishwa lakini kutokana na utaratibu mrefu wa Benki ya Dunia, fedha ilikuwa inachelewa kufika. Utakuta kunaanza na *concept paper* inafuata *mission,* inafuata *design stage,* inafuata *appraisal*, inafuata *back to office report* hivi vitu vinachoshwa wananchi wanataka maji. Hivi ni vizuri kwa nchi zingine zilizoendelea kucheza na hayo maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia makatarasi yanayotumika kwa ajili ya *stage,* gharama yake ni kubwa unaweza ukachimba kisima kikatosha na wananchi kupata huduma ya maji. Kwa hiyo, naiomba Wizara irekebishe utaratibu huo. Fedha zifike kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kishapu tumeshahamsisha vijiji 10, mfano kijiji cha Sakeididi wananchi wamekwisha kuchanga shilingi milioni kumi na moja, wako tayari kabisa wanasubiri mradi ujengwe. Kijiji cha Maganzo ambavyo vile vile ni mji unaokua wako tayari, Kijiji cha Butuyu na wenyewe wako tayari na Munza ambao sasa hivi ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu, sasa hivi wana chanzo kidogo tu lakini wananchi wako tayari mradi wa maji safi na usafi wa mazingira uweze kupanua chanzo hicho na uweze kutosheleza Mji wa Kishapu. Lakini wananchi wa Makipoyo vile vile wako Kiloleni wako tayari, Kiloleni wako tayari, Bulekela wako tayari na Mwamashele wako tayari. Kwa hiyo, naomba Serikali isicheleweshe fedha baada ya utaratibu mzima kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mabadiliko ya hali ya hewa na umuhimu mkubwa wa kuimarisha ofisi za maji za mabonde. Mwaka 1997 nchi zilipokutana Kyoto kuzungumzia Itifaki ya Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa suala la mabadiliko la hali ya hewa lilikuwa ni jambola kutarajiwa kwa muda mrefu. Lakini kwa sasa ni dhahiri Ziwa Victoria, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa joto kuongezeka linakauka pamoja na sababu zingine. Mto Mara unapungua sasa hivi na vyanzo vingine vinapungua. Kwa hiyo, kuna haja ya kuimarisha ofisi za maji za mabonde ambazo zina kazi kubwa ya kufuatilia raslimali ya maji nchini. Tuboreshe vile vile maslahi ya wafanyakazi wa ofisi za maji za mabonde kama tunaona umuhimu wa sekta ya maji. Tuna miradi mikubwa yawezekana baada ya kujenga miradi hii mikubwa, lakini kutokana na kubadilika kwa hali ya hewa na vyanzo vingi kukauka tutakuja kukuta maji hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mfano mzuri wa Ziwa Victoria, tuna mfano mzuri wa Ziwa Chad, tuna mfano mzuri wa Mto Mara na mito mingine ambapo nafikiri Waheshimiwa Wabunge, mahali mlikotoka mnaona mabadiliko makubwa sana. Kwa hiyo, naomba tuimarishe ofisi za maji za mabonde na tuboresha maslahi ya Maafisa wa Maji wa Mabonde ili wafanye kazi ya kufuatilia hali hii kwa karibu zaidi na kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kuhusu ujenzi wa mabwawa katika maeneo kame. Naipongeza Serikali kwa uamuzi wa makusudi wa kujenga mabwawa katika maeneo kame nchini. Wilaya ya Kishapu ni moja ya maeneo kame. Kutoka Novemba, 2005 mpaka mwezi Februari, tumepata mvua kwa muda wa siku 17 tu na ni milimita 233.8 ambazo tumepata. Ni hali ya kuenea kwa jangwa hivyo. Kwa hiyo, nitaona ajabu kwamba katika mabwawa ambayo yamepangwa kujengwa Wilaya ya Kishapu itakosa bwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaona ajabu kwa sababu ni dhahiri Wilaya ya Kishapu na Jimbo la Kishapu linakabiliwa sana na tatizo la ukame na ni mashahidi kwamba nimezungumza hapa kuhusu upungufu ni moja ya matokeo ya ukame. Kwa hiyo, nitaona ajabu Wizara kutoipa umuhimu Wilaya ya Kishapu katika ujenzi wa mabwawa ambayo imepanga kuyajenga. Kwa hiyo, naomba Wizara izingatie hilo suala la ujenzi wa mabwawa katika maeneo kame ninaomba chonde Wilaya ya Kishapu ipewe umuhimu wa kipekee. *(Makofi)*

Mimi nimeanza kuzoea kidogo Bungeni, naomba nisigongewe kengele, lakini la mwisho naipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu, kwa jengo hili zuri, naomba Mungu atuepushe na wale wanaotazama jengo hili kwa jicho la husda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, ili leo na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze pia kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwa kazi nzuri ambayo ameonyesha kuanza kuifanya katika kipindi cha miezi sita iliyopita akishirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wilaya hiyo.

Napenda kuwakumbusha ndugu zangu kwamba Wizara hii, ilikuwa inaongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati huo akiwa Waziri wa Maji, ameacha viwango vya hali ya juu katika Wizara hiyo na kwenu ni kigezo na kipimo. Mnayokazi kubwa ya kujaribu kufikia na kupita viwango vile alivyoviacha. Nawapongeza kwa kupokea kazi hiyo na majukumu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuipongeza Wizara hii kwa mambo mengine makubwa mawili, kwanza ni moja kati ya Wizara ambayo ukiwaandikia barua wanajibu barua, nawapongeza sana. Lakini pamoja na kujibu barua pia ni Wizara ambayo vile vile inafuatilia wanakuja kuwaona wananchi, wanawaona Wabunge katika maeneo yao, wanawaona Halmashauri, wanazungumza na wanafanya mikutano ya hadhara. Kwangu mimi Muheza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri wake amefika kwa siku moja amefanya mikutano mitatu ya hadhara. Kwa hiyo, nampongeza sana, wamezungumza na wananchi wamemwelewe wameelewa matatizo ya Serikali na wana matumaini makubwa kwamba Wizara hii itayaondoa matatizo ya maji katika Mji wa Muheza katika Jimbo la Muheza na katika Wilaya Mpya ya Muheza kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo makubwa ya maji. Lakini watu wengi wanatushangaa kwa nini Muheza tuwe na matatizo makubwa ya maji wakati Muheza tuna vyanzo vikubwa sana vya maji? Chanzo kimoja kikubwa sana cha maji ndiyo chanzo kinachopeleka maji katika Jiji la Tanga. Mto mkubwa umeanzia Muheza asilimia 90 ya mto ule unapita ndani ya Wilaya ya Muheza, hatimaye unaishia Tanga kwa asilimia 10 iliyobaki lakini unapeleka maji katika Jiji la Tanga. Muheza hatuna maji.

Lakini naomba nirudie, nilisema miaka michache iliyopita na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alinisikia na naomba leo nithibitishe kwamba barua uliyoniandikia imefanya kazi na sasa tumefanya utafiti wa namna ya kuwezesha Muheza kupata maji kutoka katika vyanzo vilivyopo ndani ya Muheza, chanzo cha Mto Zigi bila kuvuruga uwezo wa Mto Zigi, kupeleka maji Tanga. Bado tuna chanzo kingine kiko karibu na Mto Zigi, chanzo cha Derema na tathmini zinaonyesha kwamba tunaweza tukapata maji Muheza bila kuathiri upatikanaji wa maji katika Mji wa Tanga kutoka chanzo hiki.

Sasa Wizara imekuja na wamekubali kuisaidia Muheza kupata maji. Siku zote nasema mnapoisadia Muheza kupata maji maana yake mnasaidia kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Muheza kwamba atasaidia Muheza kupata maji. Naomba mradi wa Ubembe Kwemhosi mradi wa maji ambao Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja akazungumza na wananchi na akaahidi kwamba utatekelezwa, utekelezwe. Utatekelezwa kwa kusaidia pia kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wananchi wa Muheza wana imani kubwa kabisa kwamba tatizo la maji katika Mji wa Muheza litaondoka na hatimaye litakwisha kabisa na itabaki historia. Lakini moyo wa maji kwa Jimbo la Muheza na Mji wa Muheza, ni utekelezaji wa mradi huo wa pili unaoitwa *Muheza Main Trunk* ambao umefanyiwa utafiti na kuonyesha kwamba maji yanaweza kupatikana kutoka chanzo cha Mto Derema. Huo ndiyo moyo, mradi wa Ubembe Kwemhosi utatupunguzia matatizo ya maji kwa muda. Tunaupokea kwa sababu kwa uhakika utatupunguzia matatizo ya maji kwa muda na utaweza kutoa huduma kwa zaidi ya kata sita. Hilo ni jambo jema na Mji wa Muheza tatizo hili litapungua. *(Makofi)*

Lakini kwa mtazamo wa mbali *solution* ya matatizo ya maji Muheza ni *Main Trunk* hiyo ya Muheza. Mradi ambao umekadiriwa kufikia shilingi bilioni 3.2. Lakini naomba sasa watalaam wasipate *pressure* kama mradi wa Ubembe Kwemhosi utakuwa umetekelezwa maana yake mradi huu mkubwa wa *Muheza Main* sasa gharama yake itapungua kwa sababu mradi wa Ubembe Kwemhosi utakuwa pia umehudumia sehemu kubwa ambayo ilikuwa ndani ya mradi huu mkubwa wa *Muheza Main Trunk*. Kwa hiyo, badala ya shilingi bilioni tatu sasa hivi makadirio yangu yanaonyesha itashuka kwa zaidi ya shilingi milioni 500 na pengine itakuwa chini ya shilingi bilioni 2.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muheza ni kubwa, tunazo kata 23 ni moja kati ya majimbo ambayo yana kata nyingi. Lakini sehemu kubwa ya maeneo hayo ina matatizo ya maji licha ya mji wa Muheza na maeneo haya ambayo mradi huu wa Ubembe Kwemhosi umelenga. Lipo tatizo moja kubwa sana katika eneo la kata inayoitwa Kata ya Ngomeni. Kata ya Ngomeni ndio kipo Chuo cha Kilimo cha Mlingano. Katika chuo kile hakuna maji. Kuna matatizo makubwa ya maji. Jitihada zote zimefanywa ndani ya Kata ya Ngomeni kutafuta maji. Tumepata wahisani wametusaidia kuchimba visima viwili virefu na visima vingine viwili vifupi katika visima vyote vinne hivi maji yamepatikana lakini maji hayo hayafai kwa matumizi ya binadamu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika kata hii nzima ambayo kipo hiki chuo na pia kuna Kiwanda cha Kamba Ngomeni, kiutaalam hakuna maji, yatakayoweza kutumika kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Sasa tutafanya nini? Hata mradi huu wa Ubembe Kwemhosi utakapokuwa umekamilika itakuwa vigumu sana maji kuweza kufika katika Kata ya Ngomeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yetu tuliyowahi kuyatoa tumejadiliana sana na wenzetu wa Jiji la Tanga, kama itawezekana hili narudia tena jitihada zimekwishafanywa ili kusaidia Chuo cha Mlingano kupata maji na wahisani wamekwishakujitokeza wametoa fedha kupitia Wizara ya Kilimo zaidi ya shilingi milioni 100 kusaidia Chuo cha Mlingano kuweza kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watapata wapi kama ardhini hakuna maji? Eneo lote maji hayafai. Njia pekee ya kukisaidia Chuo na Kata hiyo kupata ni kuomba hisani kutoka Jiji la Tanga kwa muda wakati Muheza ikiendelea kusubiri utekelezaji wa miradi mingine mikubwa ili tuweze kupata maji. Ili Tanga waweze ku-*supply* maji yale maskini ya Mwenyezi Mungu yanatoka Muheza tu lakini kuyarudisha angalau mpaka kwenye

Chuo cha Kilimo cha Mlingano, kwa muda tu wapate maji pale wako tayari mita iwekwe na watalipa kama wakazi wa Jiji la Tanga wanavyolipa. Sasa wataalam tumezungumza nao kiutendaji hili linawezekana ma-*engineer* wamekaa wameona hili linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kisiasa na kiuongozi linahitaji maamuzi kutoka juu kwa sababu Jiji la Tanga lina utaratibu wake wa kuhudumia Jiji la Tanga na si Wilaya ya Muheza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa tatizo hili nasimama leo katika Bunge hili na naomba viongozi wote mtusaidie kwa vyovyote itakavyowezekana Mlingano na Kata ya Ngomeni wapate maji kutoka Tanga, kwa utaratibu ambao Tanga itaupendekeza na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza itautekeleza. Ninapozungumza ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Muheza tayari imekwishaandika barua Jiji la Tanga kuomba hilo. Kwa hiyo, ninaomba sana mtusaidie hili liweze kutekelezwa. Fedha za kutekeleza mradi ule hazitatoka Wizarani wala Halmashauri, wahisani wamekwishapatikana, fedha zipo tayari mradi huo utatekelezwa. Naomba ridhaa yenu leo ndani ya Bunge hili kupitia Wizara inayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nizungumzie sehemu ya pili, ambayo Mheshimiwa Rais, alitoa ahadi ni mradi wa maji kwa ajili ya Kata ya Kigombe. Kata ya Kigombe iko katikati ya Mji wa Tanga na Pangani. Lakini eneo hilo lililopo ni Wilaya ya Muheza. Mheshimiwa Rais alipofika pale wakati anakwenda Pangani alisimama pale akazungumza na wananchi na aliwaahidi wananchi pale watapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi niseme kwamba katika eneo lile Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Waziri wa Maji, alitenga fedha na kikachimbwa kisima kirefu kipo na kina maji mengi na ya kutosha kabisa. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi hizo ambazo amekuwa akizifanya. Tatizo lililopo ni kukamilisha kazi hiyo. Tutajitahidi kuingiza mpango huo kwenye programu ya *TASAF* katika mpango huu unaokuja ili vile vile kumsaidia Mheshimiwa Rais, katika utekelezaji wa ahadi yake, wananchi wako tayari kuchangia nguvu kazi, wafanyekazi ili mradi ule uweze kutekelezwa na uweze kukamilika na ndugu zangu wa Kigombe waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho naomba nikumbushie kwamba Wizara ijitahidi sana kuhakikisha kwamba vyanzo vyote vya maji katika nchi hii vinapimwa na muwe na *data* za uhakika ya vyanzo vyote na si kupima tu na kuweka *beacons* na hati zipatikane. Sasa mtaamua kwamba hati hizi zitakuwa katika majina ya Halmashauri au katika Serikali za Vijiji vinavyohusika. Msaidiane na Halmashauri kwa sababu wengi wakiagizwa kufanya kazi hiyo, kwa sababu ya matatizo ya fedha kazi hizo zinaweza zikachelewa au zisifanyike kabisa. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Maji yenyewe kama mhimili isaidie katika hili kwa kushirikisha Wizara zinazohusika kama Wizara ya Ardhi na sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nashukuru kwamba nimewakilisha mawazo ya wananchi wa Jimbo la Muheza na Wilaya mpya ya

Muheza na ninaamini kabisa yale tuliyosema na tunayokusudia yatatekelezwa na matatizo ya maji katika Jimbo la Muheza yatakwisha. Nawatakia kila la heri Mwenyezi Mungu awabariki wote. Nashukuru na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na nikuombe radhi ukiona sauti inapanda kidogo maana yake ni matatizo tu ya maji kwenye Jimbo la Babati Mjini, lakini nadhani utanivumilia kwa sababu matatizo ya maji ya Babati Mjini, yanafanana na yale ya Jimbo la Peramiho ambalo mimi niliwahi kulitembelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nitumie nafasi hii, kwa kweli kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu wake pamoja na watendaji wake kwa sababu hotuba iliyoandikwa hapa kwa kweli imejaa takwimu na imegusa kila mahali. Kwa kweli nampa hongera sana ni kati ya hotuba ambazo zimeandaliwa vizuri sana. Kwa ajili hiyo, sauti haitapanda nitakuwa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kwa kusema kwamba matatizo ya maji ya Halmashauri ya Mji wa Babati, yalianza kupata ufumbuzi baada ya Bodi ya Maji, kuteuliwa bodi hiyo inaitwa *BAWASA* na bodi iliteuliwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, wakati ule akiwa Waziri wa Maji. Tunamshukuru sana nataka nimhakikishie kwamba Bodi ile inaendelea vizuri na inachapa kazi na kazi yake ni nzuri na mimi nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu kwamba Mji wa Babati ni mji unaokua kwa haraka na kwa sababu umepata hadhi ya kuwa Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Manyara basi ni kama mtoto aliyezaliwa upya. Mahitaji ya mtoto mdogo wote tunayafahamu. Mtoto mdogo akizaliwa anahitaji mambo mengi sana, anahitaji maziwa, sukari, chakula mambo mengine mengi kuliko pengine hata mahitaji mtu mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mji wa Babati umekuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara, ndiyo Mkoa ambao kwa kweli ni mpya na kwa hiyo, mahitaji ya Mji wa Babati ni makubwa na idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa sana.

Kwa hiyo, kwa kweli miundombinu yake ya maji imejengwa tangu enzi ya ukoloni. Kwa hiyo, ni ya muda mrefu sana. Sasa Mji wa Babati unategemea vyanzo vichache sana. Moja ni chanzo cha Mrara kutoka kwenye mlima unaoitwa Kwaraa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo hiki kimejengwa zamani, sasa kinahitaji sasa ukarabati wa hali ya juu. Mabomba yaliyowekwa enzi zile kwa kweli yalikidhi mahitaji ya watu wachache. Vile vile eneo hili linahitaji vile vile mtambo wa kuchuja maji na vile vile inahitaji sasa maji yasambazwe vizuri kwenye mji wa Babati. Sasa chanzo hicho kwa kweli kinatoka mlimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Babati lina maji mengi chini ya ardhi, yako maji mengi chini ya ardhi. Tunachohitaji ni kuchimbiwa visima virefu, hiyo ndiyo

itakuwa kwa kweli utatuzi wa tatizo hilo la maji kwenye mji wa Babati. Utafiti wa maji kwenye bonde linaloitwa Bonde la Maisaka. Kwenye bonde hilo limetengwa eneo na wapo wananchi kwenye eneo lile. Nilikuwa naiomba Wizara kwamba kwa muda mrefu sasa wananchi wamekuwa wakisubiri eneo lililotengwa na wale ambao wapo eneo lile hatima yao ni nini? Nina hakika kwamba fidia itataka fedha nyingi sana. Kwa sababu matatizo ya ardhi, kwenye Wilaya ya Babati ni matatizo ambayo kwa kweli ni makubwa sana. Kesi za ardhi kwa Wilaya ya Babati mara nyingi zinakwenda mpaka kwenye Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nisingependa Wizara ya Maji ikaanza kuingia kwenye matatizo na waanchi kwa sababu tu pengine aidha ya kuchelewesha fidia kwa eneo ambalo wanadhani kwamba litakuwa na maji ya kutosha au kama fidia haiwezekani basi ni vizuri Wizara izungumze na wale wananchi walio katika eneo lile wale walio karibu namna ya kuweza kuishi katika eneo lile. Lakini wakiachwa kwa muda mrefu kwa kweli linawaletea kwanza matatizo hawajui hatima yao na hilo ndiyo bonde ambalo wanalitumia kwa ajili ya mazao ya chakula ni bonde linatoa kweli mazao mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile yako mawazo kwamba pengine eneo lililotengwa ni kubwa sana kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri ufanyike utafiti wa kina na vipimo virudie pale ambapo kwa kweli ndipo panapostahili ili baadaye hata kama kuna mtu anasema kwamba eneo lile siyo eneo lenye maji basi idhihirike kwamba ni eneo ambalo kuna maji. Kwa hiyo, kwa sasa pengine niishie hapo kwa kusema ni vizuri Wizara ikaliangalia jambo hilo vizuri, kwa kina kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuna maeneo mengine Ziwa Babati ni Ziwa lenye maji ya baridi. Ni Ziwa lenye maji mazuri, lakini pengine ubora wake na usalama wake kwa ajili ya maji ya binadamu unahitaji kuangaliwa sana. Kwa hiyo, nadhani kwamba ni vizuri vile vile eneo hilo la Ziwa, Ziwa lifanyiwe vile vile utafiti ili kuona ni namna gani vile vile maji ya ziwa lile yanaweza yakatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo yanaonekana kwamba yana maji ni eneo la Singe. Kata ya Singe iliwahi kufanyiwa majaribio na raia mmoja ambaye kwa kweli aliwahi kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Marehemu George Neema na maji yalitoka kwa wingi sana kwa bahati mbaya ule mradi kwa kweli hakuweza kuukamilisha. Sasa eneo hili kwa kweli linahitaji kufanyiwa utafiti na kisima kiliwahi kutoa maji kisima kirefu. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Mheshimiwa Waziri eneo hili likaangaliwe mapema. Ni eneo ambalo lina maji mengi na yakichimbwa kwa kweli kwa kisima kirefu na likawekwa tenki kubwa likawekwa kwenye mlima unaolimwa Nyawali upo pembeni mimi nadhani kwa kweli wananchi wanaweza wakapata maji ya kutosha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kijiji cha Nakwa, yapo maji ya kutosha chini ya ardhi na utafiti umekwishakufanyika. Kwa hiyo, kinachohitajika kwenye maeneo haya kwa kweli ni kuchimba tu visima virefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kwanza niseme hayo maeneo lakini la pili nirudi kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 32. Mheshimiwa

Waziri amekubali kwa kweli Mji wa Babati bado uko kwenye daraja la (c). Kwa hiyo, tunakushukuru kwa kuendelea kulea Bodi ya Maji na kama nilivyosema kwa sababu ya uchanga umelielezea vizuri pale na kwamba tunashukuru Serikali kuendelea kulipa watumishi wale wa Bodi, *DAWASA* na kwa ajili ya kulipia umeme na kuendesha mitambo ya mashine ya kusukuma maji. Kwa kweli tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hilo.

Vile vile nitumie nafasi hii kuishukuru Wizara kwamba kwenye ukurasa huo kwenye sentensi ambayo kwa ruksa yako inasema Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itagharamia kazi za dharura ambazo ni ukarabati wa mfumo wa maji safi katika Mji wa Babati. Kwa kweli tunakushukuru kwa hilo na vile vile nishukuru kwamba mfumo wa maji safi na ujenzi wa mifumo ya uondoaji wa maji taka umetuweka kwenye kundi hilo ambalo katika kipindi hiki cha Bajeti ya mwaka 2006/2007 mji wa Babati umewekwa. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo moja kwenye Halmashauri ya Mji wa Babati. Mheshimiwa Waziri hapa amesema ili kutekeleza mradi ule ambao unafadhiliwa na Benki Dunia unahitajika Mhandisi mwenye taaluma inayotakiwa na Mheshimiwa Waziri ameeleza kuna upungufu wa Wahandisi 52 kwenye hotuba yake. Nataka kumweleza kwamba Mji wa Babati hauna Mhandisi wa Maji, sasa sijui tatizo ni nini. Sina hakika kama Utumishi wamekwishakubali kutoa kibali au Halmashauri ndiyo yenyewe bado haifanyi utaratibu wa kutangaza nafasi hiyo sina hakika. Lakini nadhani tutawasiliana na wahusika wote Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na Utumishi yuko hapa. Tunataka jambo hilo kwa kweli lifanyike kwa haraka kama ambavyo Mheshimiwa Waziri mwenyewe amesema kwamba hili kwa kweli lifanyike haraka kama ambavyo Mheshimiwa Waziri mwenyewe amesema kwamba hili lipewe kipaumbele cha kuwa na Wahandisi wa Maji kwenye kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 36 Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala hili utekelezaji wa mpango huu wa Benki ya Dunia na kwamba katika ukurasa wa 26 kwamba vijiji 10 kwa kila Halmashauri ya Wilaya, nadhani maana yake vile vile ni Halmashauri za Wilaya kwamba vijiji 1,075 vitahusika.

Sasa nilikuwa naomba kwamba katika mradi huo wa Benki ya Dunia ambao kwa sehemu nyingi unaonekana unasuasua kidogo, tunaomba utekelezaji wa kila mwaka utolewe taarifa ili tujue katika miaka hii mitano vijiji hivi vitakuwa vimesaidiwa kiasi gani miradi gani kwa kweli itakuwa imekamilika. Ningeshauri vile vile hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu basi walau zipungue kidogo. Zifanyike kama inavyotakiwa lakini basi muda upunguzwe ili miradi ianze kwa ukamilifu. Wananci wako tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia, wananchi wa Babati vile vile katika maeneo mengine kwenye Kata ya Sigino, Kata ya Isaka, vijiji vya Malangi pamoja na Kiongozi kuna matatizo makubwa ya maji. Kata zingine ni Kata ya Bonga, Kata ya Himiti, Kata ya Nangara, Kata ya Mtuka, huko nako kuna matatizo makubwa ya maji. Kwa hiyo, ningeomba vile vile ningeomba katika maeneo haya ya miradi basi vijiji

hivi vifikiriwe kwa kweli. Kwa kweli ili tuweze kuwaondolea wananchi matatizo haya ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo na mimi naomba niishie hapa kwa kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri na nikushukuru kwa kunipa nafasi hii tena. Naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Makadirio na Matumizi ya bajeti hii ya Wizara ya Maji na napenda tu kuwapongeza watu wa Wizara ya Maji wakiongozwa na Waziri wa Maji Mheshimiwa Stephen Wasira pamoja Naibu wake Mheshimiwa Mama Shamsa Mwangunga, kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika na wanaonekana wakifanya kazi, wamekuwa wakitembea katika Wilaya mbalimbali na tunawaona, vyombo vya habari vinawaripoti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni mwanzo mzuri wa kuweza kutekeleza majukumu ya Wizara yao na kwa kweli sitakuwa nimetenda haki kama sitatoa kwanza pongezi zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Bwana Patrick Rutabanzibwa, kwa uteuzi wake. Lakini pia namfahamu Rutabanzibwa, toka alipokuwa Wizara ya Nishati na kuna kipindi tulimwandalia mdahalo pale Chuo Kikuu wakati nikiwa Kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi na uwezo wake wa kujieleza na kujenga hoja ni mzuri na ninaamini kabisa kwamba atahamishia huo uwezo wake katika Wizara ya Maji ili aweze kutekeleza majukumu yake jinsi ambavyo inapaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache tu. Nina jumla ya mambo matatu tu ya kuzungumzia. Suala la kwanza ambalo ni dogo ni suala hili la mradi huu wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)* na toka Bunge hili limeanza imekuwa ni kawaida ya Mawaziri kuelezea mpango wa fedha za *MCC* na tayari niliongelea katika hotuba ya Wizara ya Miundombinu kwamba inavyofahamika *MCC* bado haijakubalika bado mazungumzo ndiyo kwanza yapo awamu ya pili, hatujafikia mahali ambapo tunaweza kusema kwamba mradi huu utafadhiliwa na *MCC* ndiyo kwanza tumeteua sekta muhimu ambazo fedha hizi toka Marekani zitatusaidia ambazo ni miundombinu, maji na nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa Mawaziri wanapokuja na kuanza kuweka *commitments* ya kwamba mradi huu Wilaya fulani, kwa kweli sidhani kwamba ni sahihi kwa sababu bado mradi huu utapaswa uletwe Bungeni, Wabunge waujadili, waupitie na kuweza kuamua ni maeneo gani ambayo fedha zitaenda. Sasa katika Wizara hii ya Maji Waziri anamezungumzia kwamba *MCC* itafadhili Wilaya ya Misungwi. Nilikuwa naomba tu Waziri kwa kweli angeweza kusema kwa kweli Serikali inaendelea na mazungumzo tofauti na kutaja *specifici* Wilaya ambayo mradi wa MCC utaweza kufadhili kwa sababu hatua bado ziko za chini sana na tunaweza tukajikuta tunajenga matumaini ya wananchi na mambo haya yasiweze kuwatokea kama jinsi ambavyo yanatakiwa.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu na nitoe rai kwa Mawaziri wengine watakaokuja kwa sababu hata Waziri wa Mipango aliitaja MCC kama kuitaja hakuweka *commitment.*

Nilikuwa naomba na Mawaziri wengine wasifurahie tu kutaja na kuridhisha Wabunge kwamba mradi utafadhili mahali fulani. Wajaribu kutulia kwa sababu *MCC* itakuja kwenye bajeti ijayo. Wasubiri wataweza kutaja hayo maeneo ambayo yatahusika. Hilo ni eneo la kwanza ambalo ni dogo ambalo ningependa kulizungumzia kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Stephen Wasira ili aweze kuliona na asitaje *specific* baadaye tutajikuja kwamba anaingia kwenye matatizo ambayo hayana msingi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala hili la *EU Water Facility* nilizungumza na Mheshimiwa Waziri na ninashukuru kwamba alinisikiliza vizuri na baadhi ya mapendekezo yangu yakawa ameyachukua na kitu ambacho napenda kusisitiza katika hii *EU Water Facility.* Tuna tatizo la taarifa na kwa mwaka ni mara ya pili, Jumuiya ya Ulaya inatoa fedha kwa ajili ya miradi ya maji, kwa nchi za *African Carribian* na *Pacific* na nchi yetu ni moja ya nchi ambazo hazifaidiki na miradi hii kwa sababu taarifa hazitoki. Taarifa hazifikii watu mbalimbali ambao wanahusuka na masuala ya maji.

Sasa nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba *EU* wanapotangaza hii miradi wataalam wake wafanye kazi ya kuwasiliana na Wilaya na kuzisaidia Wilaya kutengeneza miradi hii ya maji kwa sababu miradi ya *EU* ni migumu sana. Kwa hiyo, ni vigumu sana Halmashauri za Wilaya zenyewe kuandika na kuweza kupata fedha. Kwa mfano mwaka jana ni *NGO* 10 tu ambazo zilipata pesa kutoka *EU Water Facility* na hapakuwa na Halmashauri ya Wilaya hata moja ambayo ilipata pesa kutoka *EU Water Facility.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba na hili watendaji wa Wizara ya Maji ikibidi Waziri ateue mtu maalum kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miradi hii kutoka *European Union* kwa sababu vina pesa nyingi sana. Wilaya moja inaweza ikapewa takriban *Euro* milioni 5 kwa ajili ya maji. Kwa hiyo, inaweza kuifanya Serikali ika-*reallocate* fedha zake kwa ajili ya maeneo mengine. Tatizo tulilo nalo ni kwamba ni taarifa, hatuko *pre-active* nchi za Magharibi ndiyo zinakula pesa za *European Union* kwa sababu hii iko *open* kwa kila nchi nchi ya *European* kwa hiyo, nilikuwa namwomba Waziri aweze kuliona na bahati nzuri watendaji wake wanasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hii *EU Water Facility* ya sasa hivi ambayo Waziri ameizungumzia katika hotuba yake, amezungumzia kwamba mji wa Kigoma ni moja ya maeneo ambayo yatafaidika kwa upande wa maji safi na maji taka. Lakini tayari mji wa Kigoma tayari tuna mradi ambao uko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusiana na majitaka kutoka *NODIC Fund* wa takriban shilingi bilioni 2.9.

Sasa kuna maeneo ya Wilaya ya Kigoma, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, ambayo hali ya maji ni mbaya sana na kwa sababu tayari nimeongea na Waziri kuhusiana na suala la *EU Water Facility* na nikampa ushauri na akakubali ushauri wangu, nilikuwa naomba fedha za mwaka huu za *EU Water Facility* ambayo tayari Tanzania inapata kwa Mkoa wa Kigoma ziende Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Isiwe kuwa wanatoa ushauri wengine, wanaenda kufaidika wengine. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili Waziri aweze kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, programu ya maji vijijini. Programu hii inatarajia kufikia vijiji 1,075. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba programu hii itawezesha kufikia malengo ya MKUKUTA na kwa kweli ningependa kuungana mkono na msemaji wa Kambi ya Upinzani. MKUKUTA ndiyo ulioanza, Ilani ikafuata. Tunapofikia malengo, tunafikia malengo ya MKUKUTA, hatufikii malengo ya chama cha siasa. Naomba hii tujaribu kuweka haya mambo, kwa sababu MKUKUTA ndiyo ulioanza kabla ya Ilani, Uchaguzi umefanyika Desemba, 2005 Ilani zimetengenezwa mwezi Agosti, 2005 MKUKUTA tumeupitisha mwezi Mei, 2005.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba haya mambo yaweze kuwa *clear.* MKUKUTA unasema tunataka vijijini watu wafikiwe na maji asilimia 65 ya *house holds* na ndani ya dakika 30 kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, alivyozungumza. Waziri anasema mradi wa maji vijijini utatusaidia kuweza kufikia malengo ya MKUKUTA. Lakini malengo ya MKUKUTA ni ya miaka mitano. Ni lazima na hii kwa Mawaziri wote, nawapa ushauri na ni ushauri wa bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufikie wakati tuseme katika mwaka wa fedha 2006/2007 tutafikia lengo kiasi hiki ili tuweze kuwapima. Mkisema tu tutafikia malengo, tutawapimaje mwakani. Ni lazima muweke vitu ambavyo vitatufanya sisi tuweze kuwapima. Naomba hili na Waziri utakapokuja utuambie na uwaulize watendaji wako watuambie kwamba mwaka huu tutafikia lengo la MKUKUTA kwa kiwango gani ili mwakani tuweze kuona matokeo yake tuweze kujua kwamba yakifikia mwaka 2010 tutakuwa tumefikia hayo malengo ya MKUKUTA.

Sasa katika hili la programu ya maji vijijini, nilikuwa nataka nizungumzie kitu kimoja, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kama ilivyokuwa Halmashauri zingine vijiji 10 vitaweza kupata fedha kutoka katika mpango huu. Vijiji sasa vinatoka katika Jimbo la Kigoma Kusini, vijiji vitatu katika Jimbo la Kigoma Kaskazini. Sina tatizo na hili hata kidogo. Kwa sababu mimi ninachokitaka ni maendeleo ya wananchi kwa ujumla wake. Kwa hiyo, sina tatizo na mgawanyo huo wa vijiji, sina tatizo nao hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu ni kwamba kuna *lack of co-ordination,* vijiji ambavyo Serikali imevipanga kwa ajili ya mradi ya maji vijijini, kwa Wilaya ya Kigoma kuna vijiji viwili ambavyo tayari vina mradi wa maji kutoka Shirika la Kihispaniola *(ISF)* ambavyo ni kijiji cha Mahembe na kijiji cha Kahalu. Sasa unajua hapa mna-*reallocate* fedha sehemu ambayo tayari kuna mradi ambao unaendelea na mradi huu unaendelea kwa sababu unagusa vijiji vya Mtakwimba, Mahembe, Msimba, Kamala mpaka upande wa Kusini kijiji cha Simbe.

Mimi nilikuwa nashauri kwamba napongeza kwamba kijiji cha Kalinzi ni miongoni mwa hivyo vijiji kwa sababu kwanza ni mji mdogo, ni mji ambao unazalisha kahawa, unahitaji maji ya kutosha una tatizo la maji. Kwa hiyo ni eneo zuri. Lakini nilikuwa naomba mahala ambapo kijiji cha Kamala kinatajwa na naomba Mkurugenzi wa Maji Vijijini na Wizara ya Maji, Bwana Sayi, alisikie hili ili akalibadilishe kwamba eneo la Kamala kwa sababu *already* kuna mradi mwingine, lichukuliwe na Kijiji cha Nyarubanda kwa sababu Nyarubanda ni moja ya vijiji ambavyo vinazalisha kahawa na vinahitaji maji na kina tatizo kubwa la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kijiji cha Mahembe kwa sababu kina mradi mwingine wa *ISF* ambao unatokana na fedha za Jumuiya ya fedha za Ulaya. Naomba kichukuliwe na kijiji cha Mwandiga ambayo pia ni mji mdogo, ni mji wa muda mrefu, una watu wengi na kwa kweli kuna tatizo kubwa sana la maji. Kwa hiyo, nilikuwa naomba watendaji wa Idara ya Maji, kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, waweze kuchukua hayo marekebisho, wawasiliane na Mhandisi wa Wilaya ili kuweza kuweka hayo marekebisho kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Nyarubanda na Mwandiga inakuwa ni sehemu ya vijiji ambavyo vitaguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la bajeti ya Wizara ya Maji. Kwanza mimi nataka kupingana na kauli ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwamba Bajeti ya Wizara ya Maji ni ndogo. Si ndogo. Wizara ya Maji mwaka huu imetengewa asilimia 8.4 ya bajeti mzima. Hii nchi haiwezi kuwa ni ya maji. Hii ina nchi ina sekta nyingi. Kuna Kilimo, kuna Afya, kuna Elimu na kadhalika. Asimilia 8.4 ya bajeti inatosha. Cha msingi ni Watendaji kutekeleza. Kwa hiyo, hili nilikuwa nataka kidogo nilielezee. Lakini kuna tatizo moja, ni tatizo la mgao wa fedha za Bajeti kiwilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani hapa leo asubuhi amezungumza. Ametaja Wilaya ambazo zina matatizo ya kero kubwa ya maji. Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali hii hapa *Human and Development Report* ambayo kila Mbunge aligawiwa na Wilaya ambazo ziko chini kabisa, katika suala zima la maji, ukurasa wa 75, ni Sikonge, Mkuranga na Igunga, miongoni mwa hizo Wilaya kuna Wilaya ya Urambo ndani ya Wilaya 10 bahati mbaya Mheshimiwa Spika hapa hayupo. Ndani ya Wilaya hizo 10 ambazo zina matatizo makubwa sana ya maji ambazo chini ya watu 20 wanapata maji katika jumla ya watu 100. Lakini sasa nikaja kuangalia katika hotuba ya Waziri, amegawaje rasilimali zinatokana na maji. Nikawa *soft* kidogo, mimi najiona kwamba ni Mtaifa na nisingependa kutoa lugha ambazo zinaweza kutugawa. Lakini Wilaya ambazo zinaongoza kwa kugawiwa fedha nyingi kwanza Kinondoni, haimo katika Wilaya zenye matatizo. *(Makofi)*

Pili, Bunda na tatu Nzega. Nadhani hivi vitu lazima tuweze kuviangalia, Bunda haimo katika kumi bora yaani zile kumi zenye matatizo zaidi. Lakini Bunda peke yake imepewa fedha zaidi ya fedha ambazo Mkoa wa Kigoma umepewa. Bunda imepewa shilingi milioni 278. Kigoma kwa ujumla wake shilingi milioni 206, Singida kwa ujumla wake shilingi milioni 248, Manyara kwa ujumla wake kwa Mheshimiwa Omar Kwaangw' shilingi milioni 286. Sasa hii ni lazima tuweze kuangalia tunagawanye rasilimali zetu.

Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo nimekuwa naomba tuweze kuyaangalia na kwa mikoa, mkoa ambao unaoongoza ni Mara, mkoa wa pili ni Pwani, Wilaya ya Bagamoyo ndiyo Wilaya ambayo inaongoza katika baadhi ya Wilaya ambazo zimetengewa fedha nyingi zaidi. Kwa hiyo, inabidi tuweze kuangalia, tugawe rasilimali zetu na mimi nilitarajia kwamba Wilaya ya Igunga ingepata fedha nyingi zaidi. Wilaya ya Mkuranga ingepata fedha nyingi zaidi, sawa ni Wilaya zenye matatizo, zingepata fedha nyingi kuliko jimbo langu kwa sababu hizi zina matatizo kwa vile Watanzania ni lazima wakati mwingine tuwazungumzie Watanzaia wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Sikonge, imepata fedha nyingi zaidi. Wilaya ya Urambo imepewa shilingi milioni 71. Ina matatizo watu 17 tu ndiyo wana uwezo wa kupata maji kati ya watu 100. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri aweze kuyaangalia haya, ili aweze kuyarekebisha kwa sababu yanaweza yakatuletea matatizo. Mliona kinyang'anyiro kilichotokea hapa katika Wizara ya Miundombinu. Watu wanaangalia kutokana na Waziri anatoka wapi. Makosa haya haya yanakuja kurudiwa tena katika mgao mzima wa maji.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba inawezekana kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu tunamfahamu Mheshimiwa Stephen Wasira, ni mzalendo, anapenda nchi yake. Kwa hiyo, naamini kwamba hakufanya makusudi, maana yake hata Kongwa imepewa hela nyingi zaidi, kuliko Wilaya zingine za Dodoma. *(Makofi)*

Kwa hiyo, haya mambo inabidi kuyaangalia ili tuweze kutatua matatizo mbalimbali. Mimi nimemaliza hoja zangu nashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Maji. Nianze kwa kumpongeza yeye Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri walioiwasilisha hapa ina mpangilio nzuri, ameisoma kwa ufasaha, mambo yamekaa vizuri nawapongezi sana kwa kazi nzuri kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja wa Kamati iliyoshughulikia hotuba hii. Mengi tumechangia kama alivyowasilisha Mwenyekiti wangu,, ameiwasilisha vizuri, inanifanya mimi niunge mkono asilimia mia moja bila kusita katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri Mkuu tulichangia mambo mengi, tuligusia ujenzi, tuligusia kilimo na tuligusia maji. Wakati anajibu Mheshimiwa Waziri, Waziri Mkuu hakupata nafasi ya kujibu hoja mbalimbali kutokana na ufinyu wa muda. Lakini aliagiza Wizara basi ziweze kuyachukua hayo matatizo na baadaye waweze kutujibu wananchi waliotutuma waweze kupata taarifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Waziri Mkuu kama jinsi Wabunge wengine wakati wa hotuba yake walivyoweza kumpongeza kwa uwepesi wa kuchukua maamuzi fulani fulani kadri jinsi Wabunge wanavyochangia hapa Bungeni, hayupo kwa ajili ya kukaa tu hapa, anaratibu mambo na mengine anayachukulia hatua hapo hapo. *(Makofi)*

La kwanza , ambalo utekelezaji wake umeonekana ni lile barabara ya kutoka Usagara kwenda Geita kupitia Sengerema. Alichukua *action* mara moja na kuitekeleza. Tunampongeza sana Waziri Mkuu kwa hatua hizo. Kwa hiyo, Waziri Mkuu kuwepo hapa anaratibu shughuli za Serikali Bungeni, ndiyo kazi yake hasa. Kwa hiyo, picha hiyo, imetupa matumaini ya hali ya juu sana, si tunapopiga kelele hapa, bali ni misingi ya haki tumetumwa na wananchi ili tuweze kufikisha hapa na baadaye tupate majibu kutoka kwenye Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zangu nyingi niligusia sana kwenye tatizo la maji. Nilizungumzia maji, nikaelezea katika mji wetu wa Misungwi. Nilieleza matatizo yaliyoko pale, matatizo yaliyoko ni makubwa sana ningependa niyagusie tu kidogo kwa leo lakini baadaye nategemea majibu mazuri kutoka kwa Waziri. *(Makofi)*

Kwanza nikiri kwamba Bunge ni mahali patakatifu, unapaswa, unaseme maneno ambayo kwa kweli yana utafiti wa kutosha. Tarehe 4 Aprili, 2006 kwenye Mkutano wa Tatu wa Bunge,niliuliza swali linalohusiana na suala la maji Misungwi. Nilijibiwa vizuri sana na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 33 amegusia lakini inatofautiana na jibu nililopewa kwenye swali langu tarehe 23 Aprili, 2006, tofauti kabisa.

Naomba ninukuu kidogo tu kwenye jibu sehemu ya (b). Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kwamba awamu ya kwanza itahusu utekelezaji wa hatua za muda mfupi, usanifu na mifumo ya maji safi na maji taka. Utayarishaji wa vitabu vya zabuni, ukarabati na kuanza ujenzi wa mifumo mipya ya maji safi. Awamu ya pili, itahusu kukamilisha ujenzi wa mifumo mipya ya maji na uondoaji wa maji taka." Lakini akaendelea Mheshimiwa Naibu Waziri, akasema sehemu inayofuata, sahamani Mheshimiwa Mwenyekiti, akasema: "Mheshimiwa Spika, mfadhili aliyefanya upembuzi yakinifu, kwa sasa ana uwezo wa kugharamia utekelezaji wa hatua za muda mfupi tu katika miji ya Bukoba, Musoma na Misungwi, kwa kiwango cha shilingi bilioni 9.6." Ametaja ikiwemo Misungwi.

Nikija kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kwa kupitia Shirika la Maendeleo la *AFB* lilishakamilisha upembuzi yakinifu katika miradi ya maji safi na maji taka katika miji ya Bukoba, Misungwi kwa kubaini kuwa gharama za utekelezaji miradi hiyo ni shilingi bilioni 93.5 katika mgawanyo ufuatao, Bukoba shilingi bilioni 31.7, Musoma shilingi bilioni 48.8 na Misungwi shilingi bilioni 15.0 katika mwaka 2006/2007.

Lakini akaendelea kusema kwamba *AFD* imekubali kuchangia kiasi cha shilingi bilioni 9.6 kwa ajili ya kutekeleza kazi ya dharura katika miji ya Bukoba na Musoma tu. Sasa kipindi kilichopita ilihusishwa mpaka Misungwi lakini leo hii kwenye hotuba ya Waziri amesema kwamba kuna dharura, ilitoka wapi? Sasa hapo nataka tuelewe kwamba ni Waziri yeye au watendaji wake ndio waliomletea taarifa hizi za uongo, imefika mahala sasa wananchi wanakuwa na wasiwasi na Bunge lao, nimeuliza hapa nimejibiwa vizuri, wamekuwa na matumaini ya hali ya juu, leo hii katika hali ya dharura Misungwi haimo, tena yenyewe ni shilingi bilioni 15 wakati Musoma shilingi bilioni 31.7, Bukoba 48.8 wamegawanywa zile shilingi bilioni 9.6 wao. Huyu mdogo ameachwa aendelee kuumia tu, tunaendeshaje Bunge sasa namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapoteremka kwenye vifungu utuwie radhi, imefika mahala sasa tuwabane, mtuachie tuwabane ni tatizo kubwa sana hili, upendeleo pendeleo unaanza kuonekana, tunaanza kubanwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana hapo uwaachie nafasi, mimi kwa kweli baada ya kubanwa juzi juzi imefika mahala, nilikuwa nimeanza kufikiria ujumbe wa kwenda kumuona Rais, niende na mapendekezo moja kwa

moja kabisa, mimi nadhani sitawahusisha sana Mawaziri, nitahangahika na watendaji, Mawaziri ni juzi juzi wameingia tu hapa wana miezi minne, watendaji wako miaka yote ile wanajua matatizo ya Misungwi, hata juzi wakati anajibu Waziri wa Kilimo hapa, kila anapokwama majibu yalikuwa yanatoka kwa watendaji hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wenye kuwabana zaidi ni watendaji, kama ni kuteremshwa vyeo wateremshwe, ikibidi kufukuzwa wafukuzwe waingie wengine pale wafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niliseme katika hali hiyo kwa sababu imefika mahala wana Misungwi hawanielewi kabisa, juzi wamenipigia simu wakipongeza, lakini leo hii ni tofauti na hotuba hii wakisikia mbele ya safari tuachie tushirikiane na Wabunge wenzetu tuweze kufanya kazi ili Serikali ije katika utaratibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwenye upande mwingine, kwenye maji, maji ni ya muhimu sana, ukihitaji dhahabu kuisafisha utumie maji, ukihitaji kupanda mazao vizuri utumie maji, niendelee kumpongeza Waziri Mkuu katika mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama ameusimamia kwa karibu sana na Mawaziri waliopo na wenyewe wanaendelea kuusimamia sana kazi aliyoifanya ni ya hali ya juu, amewakumbuka wananchi wake lakini cha ajabu Mheshimiwa Waziri Mkuu alikumbuka na mifugo. Kila patakapopatikana kituo cha maji, lazima pajengwe kwa kukumbuka mifugo, mifugo ni ya muhimu sana jamani na nikuombe Mheshimiwa Waziri katika mipango yako yote unapogusa tu mahala fulani pana mradi wa maji, lazima ukumbuke mifugo kwenye eneo hilo itahitaji kunywa maji kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kengele imelia niendelee kuwa nagusa gusa pole pole hivyo, nitoe tahadhari kwenye hali ya Ziwa Victoria, hali ya Ziwa Victoria bado maji yanazidi kupungua, mfano halisi unaonekana kwenye mradi wa maji kule Mbalikwa, tunahitajika kuongeza mabomba zaidi ya matano kuyafuata maji ziwani. Ukija Sumbugu, tatizo ni hilo hilo magati mengi sasa hivi yanazidi kubaki pembeni baada ya maji kuzidi kupungua, sasa Serikali ianze kuliona hilo ili angalau tuanze kujiandaa kujenga mabwawa makubwa, tuweze kukinga maji kwa ajili ya tahadhari katika mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie uhaba wa watumishi kwenye Halmashauri zetu hasa sekta ya maji, tunao vijana wetu wanamaliza chuo, kwenye Chuo chetu cha Maji pale Rwegarula, wanamaliza, lakini cha ajabu, ajira hawapati, hebu Waziri jaribu kufanya utaratibu wa hali ya juu, vijana wanapomaliza pale watafutiwe kazi moja kwa moja waende kwenye Halmashauri zetu wawasaidie huko. Tuna matatizo ya wataalam wa maji kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze ndugu yangu Mkurugenzi wa Maji vijijini Ndugu Sayi, kazi hiyo kwa kweli anaiweza kabisa, anagawanya katika utaratibu wa hali ya juu vijiji vyote vinavyohusika na yeye anajaribu kufika kuona na kusaidia, wananchi wa Masasi wanakupongeza sana kwa mradi wako ambao umetekeleza pale unaenda vizuri, wanaomba tu ukipata nafasi uwaongezee pesa kwa ajili ya ujenzi wa tenki ili waweze ku-*reserve* maji mengi na baadaye waendelee kutumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze *JICA* wameshafanya upembuzi katika vijiji 16 kwenye Wilaya ya Misungwi, lakini uwezo wa pesa zao ni vijiji viwili tu, kijiji cha Busongo na Ngaya kule Bugisha. Sehemu nyingine vijiji 14 vilivyobaki havina kabisa mfadhili mwingine baada ya yeye kumaliza kazi ya upembuzi yakinifu. Sasa tunaiomba Serikali basi kwa sababu wameshapembua, ninyi kazi yenu sasa ni kutafuta fedha zingine ili tuweza kukamilisha suala hilo.

Lakini nimalizie kwenye maji safi na mazingira, tumeshaainisha vijiji kumi tayari tangu mwaka jana, utekelezaji hamna. Juzi juzi nilikuwa kwa mwenzangu pale Sikonge, nao wanasema ni hivi hivi tu hatujaona lolote, hivi Waziri huu mradi utaanza lini sasa ili angalau wananchi watokana na matatizo ya maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi nimshukuru tena Waziri pamoja na Naibu Waziri wanajituma sana hasa mama anajaribu kuzunguka kila sehemu amefika pale Usagara, amefanya mkutano wa hadhara, Usagara ndio iliyokuwemo kwenye orodha ya vijiji 16 imeshafanyiwa upembuzi yakinifu, lakini cha ajabu haikupata pesa. Nimuombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri, uliwaona wananchi wangu wa Usagara walivyokuwa wanakulilia, wako tayari kuchangia, watafutie fedha ili angalau waondokane na matatizo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nirudie tena kuunga mkona hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuichangia kidogo Wizara hii. Kwanza naomba nitoe pongezi zangu za dhati kabisa na pongezi za wananchi wa Masasi kwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali kwa kweli nilipokuwa natoa hotuba yangu ilikuwa kwa kasi ndio lakini ilikuwa na maudhi kidogo, lakini leo nakuhakikishia ndugu Waziri, nazungumza nawe nikiwa na furaha kabisa. Nasema hivi kwa sababu umekwishaanza kuonyesha, toka uchukue nafasi hii ya Uwaziri pamoja na Naibu wako kwa kweli vijiji mlivyopita katika nchi hii haijapata kutokea. Tunawashukuru mwende na kasi hiyo, Mungu atawabariki na nyayo zenu zitafuatwa na wengine wanaowafuateni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi hizi sasa nizungumze mambo matatu, hasa zaidi yanayohusu Wilaya yangu na hasa hasa katika jimbo langu. Katika ukurasa wa 21 Mheshimiwa Waziri umesema kutokana na ufinyu wa bajeti na kiasi kikubwa cha fedha kinachohitajika kukamilisha miradi ya uchunguzi na hatimaye ujenzi wa miradi ya maji ya chemichemi ya Bwinji kwa ajili ya mji wa Masasi na Nachingwea, inaonyesha kwamba ndio ipo lakini ipo katika kusuasua.

Sasa ningeomba nikueleze Mheshimiwa Waziri kupitia kwa Mwenyekiti, kwamba mradi huu ni wa siku nyingi na kwa bahati nzuri mradi huu ulifanyiwa kazi na mambo yale masuala ya upembuzi yakinifu na nini yamekamilika, kazi kubwa sana sana

ilifanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa sasa Mheshimiwa Edward Lowassa, ambaye nampongeza sana, yeye pamoja na mimi atakumbuka kwamba Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu alikuwa amekwishapata fedha kwa ajili ya utekelezaji ya mradi huu na fedha zilikuwa zitoke China na tuliambiwa wakati ule kwamba zilikuwa zimepatikana kama shilingi bilioni tano, sasa kama angekuwepo bado madarakani tungemuuliza mzee mambo yakoje? Kulikoni? Lakini leo hayupo, lakini Waziri Mkuu anasikia, hivi fedha zile zimekwenda wapi? Fedha zile alizokwenda Mheshimiwa Benjamin Mkapa kuziomba China pamoja na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, wakarudi wakatuambia, mimi naondoka kwenye kiti hiki lakini nawaachieni maji Masasi, ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, hii naiuliza Serikali sio hasa wewe Mheshimiwa Waziri lakini wewe unaweza kutusaidia utakavyokuwa una-*summarize* kusema fedha zile jamani zilikuwa hewani tu ama kweli zilipatikana na kama zimepatikana nani aliyezichukua hapo akapeleka katika mradi mwingine? Watu wa Masasi walisikia kauli hii na kwa kupitia kinywa changu mimi nauliza kwa niaba yao, ili Serikali ituambie jamani zile fedha jamani ziliota miguu. Sasa kama ziliota miguu basi tuambiwe, kuna shida kubwa sana katika mji wetu wa Masasi na ndio maana hata Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu alijitahidi sana kutafuta fedha hizo. Sasa kama zimekwenda sehemu nyingine tuelekezeni kwa sababu nchi hii ni moja na tunajua matatizo yetu. Mradi huu wa Bwinji, Masasi pamoja na Nachingwea unahitaji kiasi kama cha shilingi bilioni, leo hii Waziri Mkuu nashukuru sana, ametueleza asubuhi kwamba hali ya Mapato imeongezeka yaani kwa mwezi tunapata karibu shilingi bilioni 220 hili ni jambo kubwa sana na la pongezi. *(Makofi)*

Sasa Waziri Mkuu kuchukua shilingi bilioni 10 katika shilingi bilioni 200 za mwezi mmoja si zinatosha pale Masasi kukamilisha mradi huo? Jamani chonde, hebu angalieni jambo hilo. Kama fedha hizi zimeongezeka kwa nini tuwe tunangoja na hapa tunaambiwa miradi inayotafutiwa fedha, inayotafutiwa fedha, Masasi mradi huu hela yake ipo na mapato hayo yameongezeka, tupeni fedha hizo tumalize kiu ya Masasi tafadhali. Nafikiri jambo hili Serikali imeshalisikia barabara, kwa hiyo, naamini tutakuwa na ufumbuzi wa suala hili. *(Makofi)*

La pili, katika hilo hilo nashukuru kwamba Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete, mara baada ya kuchaguliwa alipokwenda Sudan, akazungumza na wenzetu wa *BADEA* na *BADEA* wakaonyesha *interest* kwamba wataweza kusaidia maji Masasi.

Mimi namshukuru sana Rais kwenda tu safari ya kwanza anaikumbuka Masasi, kwa kweli hili ni jambo kubwa, sisi watu wa Masasi tunamshukuru sana. Sasa lakini hata safari iliyopita nilitahadharisha kwamba fedha zinatafutwa, baada ya kutafutwa, wanachangamkia wengine, sasa hili ndio baya hili, sasa watu wasije wakachangamkia suala hili la fedha za *BADEA* maana nimesikia asubuhi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano kwamba sasa hivi anavyozungumza wamepanda ndege kwenda Mwanza sijui kwenda kuangalia kiwanja na nini, huko hela zitakwenda. *BADEA* sijui watakwenda wapi na wapi, hivi Masasi hawawezi kwenda? Mbona hakuna mpango wowote hatujasikia kwamba *BADEA* nao sasa hivi wanakwenda ili kwenda kuona jinsi wananchi wa Masasi wanavyopata shida ya maji ili walau waone huruma ya kuwapatia fedha hizo

za maji kwa nini? Kama mna uhakika fedha hizi zitapatikana mimi sina maneno. Kwa bahati nzuri nilipita Mkoani Mtwara, ofisi ya maji wakaniambia kwamba upembuzi yakinifu na mambo yote yanayohusika nayo yalikuwa yamekamilika, kinachosubiriwa ni fedha tu kupata mkandarasi kujenga mradi huu. *(Makofi)*

Sasa tafadhalini, kama ndio hivyo tafuteni mahala popote, pamoja na fedha za ndani kusudi tuweze kufanya kazi hii na nitashukuru kwamba wakati bomba hili linavyokwenda Masasi kutoka Bwinji, naomba vijiji vifuatavyo vipate maji hayo. Cha kwanza kijiji cha Nango yenyewe, ukitoka Nango kijiji cha Liputu nacho kipate maji, ukitoka Liputu baadhi ya sehemu za Mwena na Chikundi nazo zipate maji, ukitoka hapo Chigugu ipate maji, Chigugu ikishapata maji maji nayo Chikukwe ipate maji, ukitoka Chikukwe na Makongwa ipate maji, ukitoka Chikukwe Namakongwa ipate maji, ukitoka Namakongwa ipate maji, Mirambo ipate maji, mwisho na Masasi yenyewe yabubujike kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pia nikitaka kuchangia kwamba katika suala la matatizo ya maji katika jimbo letu, upande wa Magharibi ambao ndio unapakana na Wilaya ya Nachingwea, kuanzia sehemu za Namajani, ukienda Namatutwe, ukifika Chikoweti, ukifika Chiwale, ukifika Mpanyani, Lukuledi na kadhalika. Sehemu hizi zote zina matatizo ya maji, kulikuwa na mpango hapo zamani wa kujenga bwawa katika mto wa Lukuledi, sasa mpango huu sijui umefifia namna gani, mpango huu ungeweza kuleta maji kwa upande wa Masasi Magharibi na hapo hapo kuleta maji upande wa Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba ninyi wapya, Waziri pamoja na Naibu Waziri hebu angalieni kwenye *archive* zenu muone jinsi gani mpango huu unavyoweza kufufuliwa, tuondoe masizi yaliyoota katika mradi wenyewe ili uwe juu, uweze kupatiwa fedha na uweze kutekelezwa. Kulikuwa na ahadi kwamba *JICA* pamoja Japan wangeweza kutekeleza mradi huu lakini baada ya hapo kumekuwa kimya moja kwa moja. Kwa hiyo, naomba sana bwawa la Lukuledi liweze kuwa *revisited* ili maeneo haya niliyoyataja nayo yaweze kupata maji.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka Mashariki, Masasi nayo ina matatizo makubwa na kwa bahati nzuri kuna chemichemi nyingi, kuna chemichemi ya Nahinga, ambayo chemichemi hii ingeweza kutoa maji kwa vijiji vya Nanganga, ikaweza kutoa maji kwa vijiji vya Mumbulu, ikiweza kutoa maji pia katika vijiji vya Mkwera na kadhalika. Sasa yale ni maji ya Mungu, ni kama unayafungulia kwenye bomba, yapo yanatoka yanabubujika, upembuzi yakinifu umekamilika, kilichobaki pesa. Jamani kama nilivyosema mwanzoni, fedha hizi za mapato zinazoongezeka za ziada, hebu jaribuni kutafuta tafuta kidogo kusudi wananchi hawa waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii inawezekana kabisa, inawezekana kwa sababu Mwenyezi Mungu katika ukanda ule wa Makongo wa upande wa Wilaya ya Masasi kuna chemichemi nyingi sana, ukitoka Nahinga hapo kuna chemichemi nyingi, Nango, Liputu, Ndanda, Mwena na Mwiti, yaani zimejaa chemichemi na hizi zote zina maji safi ambayo yanaweza kuchukuliwa, wananchi wakayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili suala la fedha, fedha jamani hebu tafadhali tuwe na *master plan* inayoeleweka, *master plan* itakayowapa wananchi vijijini maji salama na ya uhakika ya bila wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba sana kuiunga mkono hotuba ya Waziri wa Maji na kusema kwamba ametoa matumaini, tuna matumaini makubwa kwake, naamini kabisa kama ameanza hivi basi wale askari wa miavuli wanaoning'inia wataendelea kuning'inia huko juu lakini hawa watakuwa wameshuka chini barabara na kutuletea maendeleo ya dhati hasa katika sekta hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hotuba hii ya Wizara ya Maji, pia ningependa kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kama nilivyofanya huko nyuma ya kumpongeza Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi, chama dume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama chetu, Mheshimiwa Yusuf Makamba, namfahamu sana yeye hakudandia uongozi katika nchi hii, ameanzia chini, kwa hiyo, anauzoefu mkubwa kwa hiyo, tunaimani naye kwamba sasa tumempata Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuwapongeza wenzetu ambao wamepewa Idara katika Chama cha Mapinduzi wote nawafahamu, ni wachapakazi, ni wazalendo watakijenga chama chetu wakishirikiana na wanachama wengine. *(Makofi)*

Pia ningependa kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa uhodari wake wa uchapaji kazi, namfahamu tangu tuko CCM pale Makao Makuu na hata hapa alipokuwa anazungumza Mheshimiwa Raynald Mrope, alikuwa anakubaliana na maneno yale maana nilikuwa namwona anachekacheka, anafurahia furahia kuonyesha kwamba ni kweli yale ambayo alikuwa anayazungumza anayafahamu fika katika suala zima la mradi wa maji wa Bwinji, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ningependa kuchangia kidogo. Kwanza ningependa kuanza katika vyanzo vya maji. Pamoja na yote haya ambayo tunayazungumza ya kutaka kueneza maji katika nchi yetu hii ya Tanzania ambayo ni kubwa sana, lakini kama hatukuwa makini katika kulinda vyanzo vya maji katika nchi yetu itakuwa ni kazi bure. Viko vyanzo vingi sana vya maji, kama alivyoeleza hapa kaka yangu Mheshimiwa Raynald Mrope, ambavyo kama tunavilinda tutapunguza tatizo kubwa la maji katika nchi yetu.

Mimi natoa ushauri kwa Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ya *brother* wangu Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kaeni pamoja mtunge sheria kali, ileteni hapa Bungeni ili tuweze kulinda vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakuwa na huruma katika hili ipo siku tutakuja kujuta sisi wenyewe na vijukuu vyetu vinavyokuja vitatuona hatuna maana hata kidogo, hatukuweza kuilinda nchi yetu. Kwa hiyo, naomba sana Wizara hizi mbili tungeni sheria nzuri tu, leteni Bungeni tutaipitisha ili vyanzo vya maji hivi tuvitunze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu pamoja na maelezo yaliyotolewa na Serikali katika kulinda vyanzo vya maji bado wengine wanakuwa wabishi hawataki kusikia, wanakwambia mimi nimekaa hapa tangu enzi za mababu zangu unanifukuza hapa unanipeleka wapi na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa njia pekee ya kumaliza haya ni kuwa na sheria kali ya kutunza vyanzo vya maji. Kuna mengine hatuna haja ya kuyaonea huruma, ni kwa ajili yetu sisi wenyewe na vizazi vyetu na kwa uhai wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka katika Jimbo la Lulindi. Jimbo la Lulindi kuna vyanzo vya maji, viko vingine ambavyo Serikali wamevifanyia kazi vinatoa maji kwa mfano pale Chiwambo, Lulindi maji yanatoka. Lakini maeneo mengine hayajafanyiwa kazi na wakati mwingine inaonekana kana kwamba suala hili la maji si la muhimu kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kuna chanzo pale Mkululu, pamoja na kwamba ni kijijini kwangu mimi mwenyewe lakini nazungumza kwa maana ya maji. Ni chemichemi nzuri tu, maji safi kabisa paliwekwa mashine pale ya ku-*pump* maji, akaja mjanja mmoja akasema mimi nimetoka Wizarani sijui, nimekuja kuchukua hii nikatazame tazame kidogo, nitarudisha, mpaka leo hii ile mashine haijarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake wanavijiji wa maeneo yale ambao walikuwa wanafaidika na mashine ile wanapata taabu ya kuyafuata maji haya. Mkululu yenyewe, Mkonde, Mbalichila, Chinolo, Mnolela, Mpulima, Majembe Ndago na kadhalika inawabidi waamke asubuhi na mapema saa kumi alfajiri wayafuate maji haya kwa sababu ile mashine haijarudi mpaka leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kaka yangu Mheshimiwa Stephen Wasira na tulizungumza akakubali kwamba atafanya ziara ya kuja katika eneo langu hili, naomba ahadi yake hiyo asiiche. Aje pale aone na mwenyewe atafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hii amezungumzia kuanzishwa kwa Bodi ya Mto Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefurahi sana, nimefurahi kwa sababu ni jambo la kusikitisha sana ule Mto ni mkubwa, una vijiji vingi, Manyuli, Mnavira na vijiji

vingine lakini wanapata matatizo ya maji. Wanatembea maelfu kwa kilometa kufuata maji, matokeo yake wengine wanaumwa na mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nina mfano, mpiga kura wangu mmoja alikwenda Mto Ruvuma, alikoswakoswa na mamba katika paja nikatoa gari yangu nikampeleka zahanati ya Makong'ondo wakasema hapa hatuwezi tukamtibu tumpele Newala, maskini ya Mungu yule mtu alifariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kwa kuwa Bodi hii imeshaanzishwa, basi na ifanye kazi kweli. Wakati mwingine miradi hii sio mikubwa kiasi hicho cha kuhitaji fedha, wafadhili ni hela kidogo sana mamilioni tu. Leo Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ametutangazia mwezi huu Shilingi bilioni 220 zimepatikana. Hivi kweli miradi hii midogo midogo ya kuwanusuru watu wetu tutashindwa kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu wake waje kutembelea kando kando ya mto Ruvuma, wataona wao wenyewe kwamba kwa kweli hakuna haja ya kuchelewesha kuleta mradi wa maji katika maeneo haya ili wananchi wale na wao wajione wako katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni muhimu sana kwa sababu ndio uhai kwa binadamu. Kila unapokwenda, wimbo unakuwa ni huo, maji, maji na hasa nawaonea huruma akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kwa mila za Kiafrika unapozungumzia matatizo ya maji, maana yake ni kwamba unamwambia mama aamke asubuhi, wewe baba uvute shuka yako uendelee kulala, yeye aende akangojee maji na asipofanya hivyo akirudi nyumbani kwa wengine ambao mikono yao ni mirefu, ni makofi mtindo mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kule kwetu haya ndio yanayotokea. Akina mama wanasumbuka sana kutembea maelfu kwa maelfu kilomita kufuata maji alfajiri kwa ndoo moja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuja haraka haraka kule kwetu ingawa hakuja katika Jimbo langu, lakini alikaribiakaribia.

Pia, napenda nimpongeze kwa kutupangia kiasi hiki cha Shilingi milioni 151 katika Wilaya ya Masasi, lakini pamoja na hayo, namwomba sana afanye ziara aje Wilaya ya Masasi, Jimbo la Lulindi, afike katika maeneo haya ambayo mimi ninayaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, sina tatizo hata kidogo na hotuba hii ya Mheshimiwa Wassira, ni nzuri, inaleta matumaini na kama ataendelea hivi, basi anaweza kuwa Waziri wa Maji wa Kudumu katika nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kumchaya na hasa kwa dua zako. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Laizer, Mheshimiwa Felix Kijiko ajiandae na Mheshimiwa Balozi Kagasheki naye ajiandae.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hotuba ya Waziri wa Maji. Napenda kusema kwamba, naunga mkono hotuba ya Waziri kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la MKUKUTA. Nimesikia sana eti MKUKUTA sio mpango wala Ilani ya Chama cha Mapinduzi, nasikitika kabisa. Nakumbuka mikakati yote iliyowekwa tangu Vyama vingi vianze mwaka 1995 mpaka sasa hatuna Ilani ya Chama kingine chochote tunayoitekeleza.

Kwa hiyo, Awamu ya Tatu ndio imebuni na imeweka MKUKUTA na Rais wa Awamu ya Nne alisema mipango yote ya Awamu ya Tatu ataitekeleza yote ambapo ni pamoja na MKUKUTA. Hivi tunaweza kusema kwamba kila jambo zuri ambalo limefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi sio la kwake? Napenda kusema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haikatai mazuri inayoshauriwa na mtu yeyote na Chama chochote. Kama kuna mazuri leteni tutatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya maji. Nampongeza sana Waziri wa Maji, pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wake wote. Nadhani kila Bajeti ya Maji mimi huwa nampongeza Bwana Sai, anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia Mradi wa Maji Vijijini. Jimbo langu ni Jimbo la Vijijini ambalo ni kame sana. Nikisikiliza hotuba za Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sidhani kama kuna Jimbo ambalo ni kame zaidi ya Jimbo la Longido. Katika Jimbo la Longido akina mama wanakwenda kuchota maji kilometa 20. Nashukuru sana Mradi wa *ADB* ndio ukombozi kwa baadhi ya Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni visima virefu. Katika Jimbo langu hakuna maji ya *gravity.* Maji tunayotegemea, ni maji ya visima virefu. Naomba Serikali ipime maeneo yote ambapo yanapatikana maji ya visima virefu ili wakati wowote fedha zitakapopatikana ijulikane kwamba eneo fulani lina maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 Mheshimiwa Waziri Mkuu alitupa fedha kwa ajili ya visima viwili na nashukuru Waziri wa Maji amevitaja katika hotuba yake. Hivyo visima viwili vimechimbwa, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Yaani, walimaliza kuchimba, vikaachwa na katika maeneo hayo wananchi wana shida sana ya maji. Mpaka sasa mradi huo haujaanza na mbaya zaidi wananchi wameona kwamba kuna maji mengi sana pale, lakini bado wanateseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri ameitaja na ninaiomba Serikali katika Bajeti hii, tukiwa katika Bunge, hili ipeleke fedha kule na ifuatilie kwa sababu kuna matatizo sana katika Halmashauri ya Monduli na fedha zikienda, lazima

zikae miezi mitatu. Kuna Shilingi milioni ishirini zilipelekwa mpaka sasa hazijafanya kazi na hasa Mhandisi wa Maji.

Mheshimiwa Waziri unakumbuka ulipokuja Jimboni kwangu sikupata taarifa kabisa kama unakuja, wananchi wananiambia kuna Waziri amepita kwenda Namanga, mimi niko Longido sikuelezwa kabisa kwamba unakuja. Hivi jamani, ni haki?!

**WABUNGE FULANI:** Sio haki.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Kuna Watendaji wengine hawataki Wabunge wawepo katika msafara wa Mawaziri kwa sababu ya madhambi yao. Wanajua tutasema madhambi yao. Kwa hiyo, ni afadhali nimkimbize Waziri bila kumtaarifu Mbunge. Nilisikitika sana! Mimi nakuja kuambiwa Waziri yuko Namanga! Kwa hasira na mimi nikaondoka nikaenda maeneo mengine, sikwenda Namanga! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba miradi ya Jimbo la Longido itekelezwe hasa baada ya kuona kwamba sasa Longido imekuwa Wilaya. Nilikuwa namwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Waziri wa Maji: "Mheshimiwa Waziri, naomba upeleke fedha Wilaya ya Monduli." Kila siku ananiambia, bwana naogopa kupeleka fedha kwa sababu sitaki nionekane napendelea Monduli. Sasa nakuja kushangaa kuna wengine ambao wanathubutu kupeleka! Wao hawaoni kwamba ni aibu?! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kila siku nalalamika kwa sababu ya vipaumbele mnavyopanga. Serikali inapanga vipaumbele kwa upendeleo mkubwa. Majimbo mengine yana maji, mengine hayana maji, lakini fedha zinapelekwa huko huko kwenye maji. Barabara nyingine ni nzuri, sisi wengine kilomita 30 tunakwenda kwa muda wa masaa mawili, lakini hatupati fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, ningependa nitoe mfano kidogo. Mkoa wa Arusha una Wilaya tano, wamepewa Shilingi milioni 270; Dodoma ina Wilaya tano, wamepewa Shilingi milioni 546; Mara ina Wilaya tano, wamepewa Shilingi milioni 749. Sasa Wilaya ya Longido na Wilaya ya Ngorongoro kwa sababu tunapakana, naifahamu ni Wilaya kame, zina matatizo makubwa sana, lakini Wilaya ya Monduli imepewa Shilingi milioni 40 na Wilaya ya Ngorongoro Shilingi milioni 40. Hivi ni sababu zipi zimefanya mpaka sisi tukapata Shilingi milioni 40, wengine wanapata Shilingi milioni 240? Lakini sisi ndio tuna matatizo ya maji zaidi! Sielewi! Bado tutapiga kelele kwamba hamtendi haki katika mgao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la mabwawa. Maeneo mengine wanadhani kwamba maji ya mabwawa yanatumiwa na wanyama tu. Kwetu mabwawa ndio maji yanayotumiwa na binadamu, mifugo pamoja na wanyamapori. Ukiangalia maji hayo, ndio wengine mnasema kwamba ni maji machafu. Lakini ndio sisi tunaomba mabwawa kwa ajili ya matumizi ya wanyama pamoja na binadamu. Unakuta maji yamekaa kwenye bwawa miezi tisa, lakini bado wananchi

wanatumia, yamebadilika rangi, lakini bado wananchi wanatumia, lakini hata hayo mabwawa hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wizara mbili ambazo zinashughulikia suala la mabwawa, nazo ni Wizara ya Mifugo na Wizara ya Maji. Naomba fedha zote za mabwawa ziunganishwe na zipangwe katika utaratibu wa kuwasaidia wananchi pamoja na mifugo. Naomba sana Serikali itusaidie katika suala la mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kuhamahama, tatizo ni kwamba, baadhi yenu sio wafugaji mnadhani kwamba wafugaji wanahama tu kwa kupenda, hapana. Hawana mabwawa, lazima wahame! Bwawa likiisha, lazima utahama, kwa sababu huna maji mengine ya kutumia. Lazima utahama na tutakapohamia ni maeneo yale yale mnayopeleka hizi fedha, mnayopeleka maji. Kama mnataka tusihame, basi mpeleke mabwawa katika maeneo hayo ya wafugaji kwa sababu tukipata maji, hatutahama. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea tu nitapewa kuchangia Wizara ya Mifugo. Kwa hiyo, niishie hapo, mengine nitayasema katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hotuba hii. *(Makofi)*

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilianza kushawishika kwamba labda makosa yanayoandikwa kwenye hivi vitabu tunavyopewa vya kusoma wakati tunazungumzia Bajeti za Wizara mbalimbali, kwamba ni makosa ya Mawaziri, lakini nadhani tuwasamehe kwa sababu kwanza ni wapya, Uwaziri wa miezi sita na sisi Wabunge wa miezi sita tukiwasema, tutakuwa tunawaonea. Mimi nadhani watu wa kulaumiwa ni hao Watendaji wa Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Watendaji kwa sababu ni kama wanawategeshea Waheshimiwa Mawaziri wasome makosa matupu. Mwanzoni hiki kitabu nilikuwa nafikiria kwamba kilikuwa na *typing error* kwenye *figures* za pesa, kumbe Watendaji wa Wizara walioandaa, wamempatia Waziri mzima aje atusomee sisi. Mimi nawapeni pole sana Waheshimiwa Mawaziri, mnategeshewa sana na hawa watu, wafukuzeni kazi, msiwaonee aibu. Vinginevyo, mtajikuta ninyi mnalaumiwa, inakuwa ni malumbano kuwasema Mawaziri wakati makosa sio ya kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza, ninazungumza kwa niaba ya wananchi wa Kibondo yenye Majimbo mawili, Jimbo la Muhambwe na Buyungu. Kule tuna matatizo makubwa sana ya maji na nilitegemea kabisa baada ya kuipata hotuba ya Wizara ya Maji, Wilaya hii ingekuwa imefikiriwa sana. Lakini baada ya kugundua hayo makosa na kuwasikia Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nimefarijika wanaposema

Mawaziri wamewatembelea kule kwao, ndio wamepata fedha kidogo ambazo wametengewa humu ndani zinaridhisha.

Naomba Waheshimiwa Mawaziri wafike kule Kibondo wakaone jinsi watu tunavyoishi kwa taabu. Wilaya haina barabara, haina maji, wananchi wanahangaika! Wananchi wanaishi kwa kutegemea wakimbizi! Wakimbizi wakiondoka mwananchi wa Kibondo amekwisha, hatapata maji! Wenye magari hawatapata mahali pa kuyapitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makusudi mazima, naomba Waheshimiwa Mawaziri msione sehemu nyingine ni mbali, fikeni mjionee wenyewe. Mimi nawakaribisha Kibondo. Nikisikia Waziri anakwenda na mimi nitakwenda ili nimpokee nimpitishe kwenye barabara hizo, nimpeleke mahali ambapo wananchi hawapati maji, njia hazipitiki ili Bajeti ya mwakani labda Kibondo itakumbukwa kwamba kuna Mtanzania anaishi kule. Lakini naomba mchukulie Kibondo kwamba ni sehemu ya Tanzania kama sehemu nyingine zilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kibondo Mjini kuna watu 12,800. Sasa inavyosikitisha, Makao Makuu ya Wilaya kama hapawezi kuwa na maji, ni aibu kubwa mno! Kama tatizo liko Makao Makuu ya Wilaya, basi kule Vijijini ndio usiseme tena. Ukienda Vijijini, utashangaa. Utaona akina mama wanavyohangaika kuchota maji! Mimi nadhani itafika wakati sasa na wanaume tusaidie kuchota maji. *(Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwasakazie akina mama tu na wanaume itabidi tuwasaidie hawa akina mama, kwa sababu wanapata shida sana. Mama anaondoka kufuata maji kilometa kumi, akina baba tunasubiri maji tuoge twende kutembea. Tuwasaidie! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu ya Wilaya ya Kibondo ina mtambo wa kusukuma maji. Mtambo huu ni mbovu kwa miaka mingi. Kila wakijaribu kuwasha mtambo huo, maji hayaendi, wale wachache ambao ni watu 430 wameweza kubahatika kuunganishiwa maji nao wameshindwa kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji tunayotegemea Makao Makuu ya Wilaya ni maji tunayosaidiwa ya *TCRS* Maendeleo Shirika linalohudumia wakimbizi ndio wanatembeza maji kwa kutumia *bulldozer* kubwa sana. Sasa kweli hii Wizara ya Maji inashindwa kutuma mtaalam kwenda kuangalia mpaka wananchi wale wanaumia kiasi hicho na leo tunapewa Shilingi milioni 80 ambapo ukipiga mahesabu utakuta kwamba hizo fedha hazitoshi kununua dizeli ambayo inaweza kutosheleza mahitaji ya kusukuma maji kwa muda wa mwezi mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa pale Kibondo Mjini nikipata milioni 176 nitamaliza mwaka bila kuwa na tatizo la maji kwa sababu nitanunua dizeli. Nazungumza hivi kwa takwimu ambazo ni sahihi. Sasa nashangaa ninapoona kuna sehemu zinapata milioni 300, 400 ambayo nilifikiria kwamba ni makosa ya *typing,* lakini ukweli ni

makusudi mazima! Naomba Waziri wa Maji aangalie suala hili kwa Kibondo. Tatizo, hela iliyotolewa ni kidogo sana, wananchi wataendelea kuumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia pale Kibondo Mjini, lakini tuna watoto wanasoma Shule za Sekondari. Wale watoto wanapata taabu, hawana maji, mtoto anakwenda Shuleni kuanzia saa 1.00 mpaka saa 12.00 na kushinda bila kunywa maji. Lakini kinachosikitisha, hata wataalam walioondoka kwenda kufanya utifiti wa kuchimba visima, hawakuweza kufika Kibondo, badala yake waliishia Kigoma, mahali ambapo ndege inatua. Kule Kibondo wanapaona mbali sana. Hawa watoto wa Shule tunawasaidia namna gani? Kama mabomba hayawezi kufika, basi Wizara itumie wataalam wake, wanafunzi wachimbiwe visima vya maji, wasome kwa raha. Hawa wanafunzi ndio Wabunge wa mwaka kesho ndani ya Bunge, sisi tutakuwa tumeshang'atuka, lazima tujali uhai wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo tatizo kubwa sana la mabomba ya kutoka kwenye *intank* kufikisha kwa watumiaji ambao ni Makao Makuu ya Wilaya iliyoko kilometa nne. Mabomba yaliyopo, yamechoka! Bomba la inchi tatu linasukuma maji kutoka kwenye *intank,* eti hilo bomba ndio litoe maji ya kuwatosheleza watu 12,800 na uwezo wa bomba hilo ni mdogo. Kwa maana hiyo, Idara ya Maji imeamua kuweka mgao wa maji mara moja kwa wiki na ni kwa watu wachache sana. Lakini tunasema tuna Hospitali yenye wagonjwa wanapelekewa maji na *bulldozer* la wakimbizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nikifiria hili suala la maji, nakosa amani. Mimi juzi nilizungumza nilipochangia hotuba ya Waziri Mkuu. Nilizungumza sana na sikuwa na sababu ya kutokuyapongeza haya mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yamejitolea mhanga kumsaidia mwana- Kibondo kwa tatizo hilo la maji.

Napenda nilipongeze Shirika la *TWESA* ambalo linachimba visima, *TCRS* Maendeleo na *TCRS* Wakimbizi, hawa ndio watu ambao kwa kweli ni tegemeo la mwananchi wa kule Kibondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo naona linajitokeza kadri tunavyoendelea kujadili Bajeti za Wizara mbalimbali ni wataalam kupotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kabisa Mawaziri wana moyo wa kusaidia Wabunge wenzao tuliomo humu ndani, lakini wataalam walionao, ama hawatembei, wanafanyia kazi Mezani, ama wanafanya makusudi ili kuwaangusha Mawaziri wetu. Naomba wasifanye hivyo. Mawaziri hawa kwa kweli mimi nadhani kwa kazi ambazo kwa miezi sita wamefanya chini ya uongozi wa Waziri Mkuu, hawalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema Waheshimiwa Mawaziri na hasa akina mama, hata *saloon* hawaendi, hawana muda. Mimi naungana naye na hata wale Mawaziri wanaume nadhani tukiwaangalia na wao kuna kitu kinahalalisha kwamba hawalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani watalaam hao wanaotumika ama waliopo kwenye Wizara mbalimbali ni vizuri waangaliwe kwa zile Wizara ambazo hazijaleta hotuba zao za Bajeti. Hivyo viini macho ambavyo wanawategeshea Mawaziri. Waache!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa mara nyingine tena kwamba, Waheshimiwa Mawaziri, naomba Kibondo muione kwamba ni sehemu ya Tanzania, sio sehemu ya Burundi, fikeni kule Kibondo muangalie wananchi wanavyoteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nilishazungumza kwa uchungu mkubwa sana kuhusu hilo tatizo la maji kwa wananchi wa Kibondo ambao hadi hivi sasa ninavyoongea wana wiki ya pili hawapati maji. Hata hayo maji ya mgao wa mara moja kwa wiki hawapati kwa sababu hawana fedha ya kununulia mafuta. Naomba Wizara yenye dhamana ya maji, kwa kweli itembelee Wilaya zote za Kigoma. Ni matatizo matupu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI KHAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Awali ya yote, naomba nimpongeze Waziri wa Maji kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa leo asubuhi kwa Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka huu ambao tunaujadili hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli yamesemwa mengi na kuna uchungu mwingi kama Wawakilishi wa Wananchi, unaona katika kila suala linalokuja tunakuwa na mengi ya kusema. Leo ni maji, miundombinu, afya itakuja, kilimo na kadhalika, maana ni masuala ambayo yanagusa watu wetu na ni masuala ambayo tuna haki ya kuyasemea hapa Bungeni na tuna haki ya kuyatetea kwa sababu ndio kazi tunayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba niseme tu kwamba tuwe *realistic* kidogo, maana tunaweza tukaitazama Serikali lakini pia ule mgao ni mgao ambao kwa kweli upo, lakini matatizo ni mengi na pesa yetu ni kidogo. Kwa hiyo, inabidi tutazame ni mgao gani tutakaofanya na suala ambalo Wabunge wenzangu wanasema kwamba haki itendeke katika *fomular* hizi za mgao. Hilo nafikiri ni muhimu.

Lakini naomba kwa kuwa tunatuzungumzia suala la maji, niseme tu kwamba, nilikuwa napitia *article* moja ya *Financial Times,* Gazeti la Uingereza la Agosti, 2005 . *Actually* mwaka jana sio mbali sana. Hili gazeti lilikuwa linazungumzia suala la utumiaji wa maji ya *Ziwa Victoria,* kama *source* ya *Mto Nile* na wakawa wanazungumzia juu ya *treat* ya mwaka 1929 ambayo Uingereza ilisaini huo Mkataba kwa niaba yetu sisi tukiwa kama Makoloni yake na Wamisri na ikimpa Misri Veto kwamba unapokuja katika suala la utumiaji wa maji ya *Ziwa Victoria,* basi kauli ya mwisho wanayo Wamisri.

Sasa mimi naona ni vizuri tuyaseme na nimeona nichukue hii *article* niweze kuinukuu kwa kuwa tunazungumzia maji na kuna mradi mkubwa wa maji kutoka *Ziwa*

*Victoria* kuhusu maeneo ya Shinyanga na kadhalika. Kwa kweli mimi nimefurahi na ninafurahi kuona hili sio Gazeti la Tanzania, ni Gazeti la Uingereza, *it is Financial Times* ambalo ni gazeti moja linaheshimiwa sana. Hili gazeti linasema na ninapenda ninukuu: *"Edward Lowassa Minister of Water and Livestock Development says the Governments View the Nile treat is an invalid Colonial Treat" (Makofi)*

Halafu anaendelea anasema, wanam-*quote* Mheshimiwa Waziri kwamba: *"How can we deny our people the right to have water just to keep people happy Abroad?"*

Wanaendelea kumnukuu na mimi nitamnukuu hapa, wanasema: *"They are travelling ten kilometres to 15 kilometres to fetch water!" (Makofi)*

Wanaendelea, wanasema: *"Mr. Lowassa says the Government will seek to expand the pipe line if it gets more funds, adding that financing is the biggest stumbling block to development of water sector."*

Sasa kwa kweli nataka kusema kwamba kama tunajadili hotuba hii ya Wizara ya Maji aliyoitoa Waziri wetu wa Maji leo asubuhi, ni kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amejenga misingi mizuri na ni dhahiri kabisa kwamba amewaachia misingi mizuri katika Wizara hiyo na matokeo yake ni kwamba tunayo Bajeti hii na tunayo mapendekezo ambayo wameyatoa katika mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Kwa hiyo, tunafurahi na tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba ametoka hapo ameshika nafasi kubwa sasa na inampa nafasi ya kutazama maeneo yote ingawa kweli eneo la maji lina Waziri wake, lakini yeye kama *Head Prefect* pale juu, basi atazidi kulitazama zaidi na atazidi kutusaidia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, suala la maji kwa mfano Bukoba ninakotoka mimi, naomba nipasemee sana na ninashukuru kwamba Waziri wa Maji ameliweka katika mpango wake wa Bajeti na ni suala ambalo nimekuwa namsumbua sana tangu mwezi Januari, 2006, nimekutana naye na pia mwezi Februari na Machi na kilio changu na kimeendelea kuwa kilio changu kwamba, tatizo la maji katika Mkoa wa Kagera na hususani katika Jimbo la Bukoba Mjini, ni tatizo kubwa sana. Mitambo ya maji ambayo imekuwa pale ina zaidi ya miaka 50 na tunazungumza wakati ambapo *population* ya pale Mjini ilikuwa sio watu zaidi ya 15,000, lakini sasa hivi unazungumzia watu ambao wanakwenda karibu 400,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa hizo mashine ambazo zina zaidi ya miaka 50, kusema kwamba zinaweza zikamudu kutoa *service* za maji katika Mji ambao umepanuka kiasi hicho na *population* imeongezeka, watu wamejenga zaidi, matumizi ya maji yamekuwa ni mengi zaidi, kwa kweli ni kitu ambacho hakiwezekani na ni kitu ambacho nimekuwa nakipigia kelele. Ninashukuru kuona kwamba Waziri wa Maji amekiweka katika hotuba yake, lakini kubwa itakuwa ni kutazama ni vipi ambavyo litaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitazama hotuba ya Waziri wa Maji katika ukurasa wa 33 na ukurasa wa 34, amezungumzia miradi miwili ambayo ita-*finance project* za

maji katika Jimbo la Bukoba Mjini. Mradi wa kwanza ni ule ambao utakuwa *financed* na Wafaransa. Sasa mimi ningeomba kabisa kwa sababu katika kitabu kuna mahali ambapo Waziri anasema kwamba, zile Halmashauri ambazo zitakuwa hazina wataalam na Wahandisi wa kuweza kuyasimamia haya hazitapata pesa.

Sasa suala la utaalamu ni suala ambalo tumekuwanalo katika nchi hii tangu tumepata uhuru. Maana kila mwaka tunazungumzia *training people,* nafikiri ningeomba Serikali ifikie mahali kwa sababu suala la *training* tunaweza tuka- *train* katika maeneo ambayo ni *new areas of technology* ambazo zinakuja na ni kweli, lakini kuna mambo mengine ambayo ni *so basic and so fundamental.* Sasa unapozungumzia *training* ya watu kama hao wataalam wa maji ni kitu ambacho tumekuwa nacho *for so many years*.

Kwa kweli naomba kwamba Serikali, maana wanaposema sasa na hii ni kama kinga wanajiwekea, wanasema pesa zitaweza kutolewa lakini pia pesa hazitatolewa iwapo kutakuwa katika Halmashauri hiyo ama katika maeneo hayo hakuna wataalam au watu ambao wana utalaam katika maeneo hayo. Sasa hatujui vipi litakwenda kwanza na hatujui hilo tutalifuatilia vipi ama tutalitazama vipi. Kwa hiyo, naomba tusinyimwe hii fursa ya kupata msaada kwa sababu eti hakuna wataalam, lakini naomba hii iwe ni *package* kwa sababu muweze kutusaidia tuweze kupata hizo pesa, lakini pia tuweze kupata wataalam wa kuweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ninaongelea hili, naona kuna mradi wa pili ambao ameuzungumzia Mheshimiwa Waziri na huo ni mradi ambao unakuwa *financed* na Shirika la Umoja wa Mataifa la *Habitat*. Sasa naona hapa wanazungumzia katika utekelezaji huu kuna ununuzi wa pampu nne za kupampu maji kutoka katika Ziwa Victoria, lakini pia wanazungumzia juu ya kuweka *viosk* 25 kwenye maeneo mbalimbali ya Mji wa Bukoba. Kwa hili ningeomwomba Mheshimiwa Waziri kupitia kwako kwamba zipo Kata, maana Jimbo la Bukoba Mjini lina Kata 14, lakini zipo Kata ambazo zina matatizo makubwa sana ya maji na akina mama wanakwenda mwendo mrefu sana kutafuta hayo maji na hili ndiyo limekuwa linasemwa na wananchi. Ningeomba hizo Kata kwa kweli zipewe kipaumbele katika kutengeneza hizi *viosk* ambavyo wanazungumzia hapa.

Hizo Kata naomba nizitaje ili Mheshimiwa Waziri aweze kuziweka katika kumbukumbu yake na itakapokuja katika utekelezaji azitazame kwani ni muhimu sana. Kata hizo ni Kata ya Kahololo, Kata ya Buhembe, Kata ya Nyanga, Kata ya Kagondo, Kata ya Ijuganyondo, Kata ya Kibeta na Kata ya Kitendagulo. Hizi ni Kata ambazo naomba kabisa Mheshimiwa Waziri wakati anazungumzia utekelezaji wa *Program* hii ambayo ameiweka katika hotuba yake ni Kata ambazo ningeomba azitazame sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yetu yatazidi kuwa mengi na Serikali yetu itabidi tuzidi kuihimiza ifanye inavyoweza kufanya, lakini ningeomba tu niseme kwamba sasa hivi *population* ya Tanzania kama nchi, nafikiri kwa sensa zilizopita tupo watu milioni 36, lakini inasemekana kwa *projections* ambazo nimeweza kuziona ni kwamba katika miaka 19 itakapofika mwaka 2025 *population* ya Tanzania itakuwa watu milioni

60. Kwa hiyo, tunazungumza katika miaka 19 ijayo *population* yetu itakua *almost* ime-*double*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa itabidi Serikali ifanye maandalizi mazuri nasisi kama Viongozi, Muhimili mwingine wa Bunge tuone kama ni vipi tutasaidiana na Serikali kwa sababu tunatazama ni *projection* ya mbele sasa hivi watu wanazidi kukua, *resources* zetu zinakuwa *limited,* lakini ni vipi tunaweza tukazitumia na ku-*expand* hizi *resources* tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *resources* zipo, lakini ni vipi sisi tumejiweka sawa kuzitumia hizo *resources* katika kuleta maendeleo ya nchi yetu? Ziko nchi hapa duniani, *a country like Singapore* haina chochote, *Singapore has no resource* yoyote ambayo unasema kwamba inakuwa *produced* pale. Lakini unapozungumzia katika nchi ambazo zimeendelea leo, ingawaje wanasema ni *part* ya *developing country,* lakini *statistically* ukitazama katika *area* zote, *in fact* wanazidi hata nchi ambazo ni *developed.* Lakini ni kwa sababu wamekuwa na uwezo wa kuweka mambo yao katika *priorities* nzuri na wameweza ku-*focus* katika *education*.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningependa kusema bila kupoteza muda na ninaona nipo katika *time* ni kwamba zile *factors of production* ambazo zimekuwa zinakuwa *insisted* katika watalaam wa uchumi zamani wakisema ili muweze kuendelea, *you need capital, land* na *labour the three basic factors of production*, lakini sasa hivi wanasema *they become almost absolutely* ama siyo kama ni *factors* kubwa isipokuwa *the biggest factors* sasa hivi wanazungumzia *it is a knowledge based economy,* maana yake ni *economy* ambayo inakwenda *on the basis* ya watu *knowledge* yao na *priorities* zao na mtazamo wao ukoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kushukuru na ninaomba kupitia kwako nimwombe Waziri wa Maji, mambo ambayo ameyazungumza katika Bajeti hii ili tutakapokutana Mungu akitujalia katika Bajeti ijayo mwaka 2007 atuambie kwamba haya alayoyazungumzia katika Jimbo la Bukoba Mjini yatakuwa yametekelezeka.

Baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Kagasheki, naomba nimwite Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Laus Omar Mhina ajiandae na Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye ajiendae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Maji ambayo imewasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake na Wataalam wote waliomsaidia kuweza kuandaa Bajeti nzuri na kuwasilisha hapa Bungeni.

Aidha, nampongeza Waziri wa Maji na Naibu Wake kwa jinsi wanavyoendesha Wizara hii kwa umahiri. Ninafurahi kwa jinsi ambavyo wanatembelea maeneo mbalimbali kuona hali halisi ya matatizo ya wananchi na hivyo hata wakiandaa mikakati wanaandaa kitu ambacho tayari wanakifahamu kwa kuwa wamekiona *physically.* Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu ambao ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la usambazai wa maji Vijijini. Pamoja na juhudi kubwa na mikakati mizuri iliyoandikwa kwenye Bajeti hii ya kusambaza maji Vijijini, bado tatizo la maji Vijijini ni kubwa na maeneo mengine kabisa hayajawahi kupata maji safi miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wilaya ya Urambo kwa kweli hii inatia huruma. Ni Wilaya ambayo ina Kata 11, zaidi ya Vijiji 60, lakini hawana maji safi. Maji yanayotumika kule yanasikitisha! Ukiletewa maji mezani, yana rangi kama ya *juice* ya *passion* ambayo ni nzito, unashindwa kuelewa, haya ni maji au ni chakula! Inatia huruma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina Mama wanatia huruma! Wanaamka asubuhi badala ya kwenda mashambani kujitafutia riziki na kwenda kwenye kilimo na shughuli nyingine za biashara, wanaamkia kwenda kwenye maji. Akitoka huko ni saa nne na bado maji anayoyaleta yanatia huruma kwa sababu maji wanayotumia kule, ni maji ya visima vifupi ambayo yanapatikana sana sana wakati wa mvua. Wakati wa ukame ndiyo usiseme, tatizo ni kubwa sana. Ninamwomba sana Waziri aliangalie suala la Urambo kwa jicho la huruma. Wanawake wa Urambo kwa kweli wana matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wananchi wa Urambo wapatiwe maji japo hata Kata chache tu angalau wakipatiwa kwa kuanzia na Kata chache wale wa jirani wata-*share* wakati taratibu nyingine zinaendelea, lakini Kata zote zina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Urambo ni kubwa. Ninaomba sana pamoja na kuwa kwenye mipango inatamkwa kwamba mikakati inaandaliwa, lakini kwa kweli ichukuliwe juhudi za haraka za kuweza kusaidia wananchi wa Urambo waweze kupatiwa maji kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la vyanzo vya maji. Matatizo makubwa ambayo tunayo sasa hivi hapa Tanzania yakiwemo ya ukame, matatizo ya kukosa nishati ya umeme ya kutosha, hali iliyopelekea nishati hii ya umeme kupanda bei kwa hali ya ajabu, matatizo ya chakula na mengine mengi, chanzo chake ni uharibifu wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vyanzo vya maji inabidi kuwepo msisitizo wa hali ya juu na hili lisiwe ni suala la Wizara ya Maji peke yake, liwe ni suala la Wizara zote kwa sababu kila Mwananchi, kila Wizara inaguswa na suala la maji. Maji ni uhai, hakuna asiyefahamu. Bila uhai, hakuna kazi inayokwenda, wala hakuna maisha yenye uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara hii iangalie, mwananchi yeyote yule ambaye anahusika kutumia raslimali hii ya maji, Mashirika, viwanda na yeyote yule pamoja na kuwa wana hati za kutumia maji, lakini waandae mikakati mahiri ya kuhakikisha ni jinsi gani wanavyotumia raslimali hii ya maji. Kila kiwanda, kila Shirika viandae mkakati unaoeleweka na ikiwezekana uwasilishwe hata Wabunge wajue kabisa kila Shirika limeandaa mkakati gani kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji.

Sasa hivi tuna tatizo kubwa la umeme, imefikia hatua Bwawa la Mtera ambalo tunaitegemea limeelekea kukauka, kina kimepungua kiasi kwamba sasa hivi imebidi kisitumike tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama suala la Mtera maji kupungua limetokea siku moja, ni suala ambalo limetokea muda mrefu. Swali ninalouliza ni kwamba, Je, *TANESCO* ilikuwa haifuatilii hili suala? Kama ilikuwa inafuatilia, *TANESCO* ilikuwa inafuatilije kujua kwamba kwa kuwa maji ndiyo chanzo kikubwa cha kuwepo kwa umeme, *TANESCO* ilikuwa inakikisha kwamba ule mtiririko wa maji upo? Ili isije ikakutana na hali ambayo imefikia sasa hivi na kulazimu bwawa lifungwe, lisitumike. Wananchi wanateseka kupata umeme, kisa ni kwamba maji yamepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa kwamba kama kungekuwepo na mikakati ya kutosha tangu mwanzoni, *TANESCO* ingejua mapema kwamba kina kimeanza kupungua, maji yamekuwa machache na hivyo kuchukua juhudi za tahadhari za mapema kulikoni kusubiri mpaka matatizo yatokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la maji safi na maji taka. Kuna juhudi nzuri kabisa na mikakati mizuri na mahiri imeandaliwa na Wizara ya Maji, lakini ninazungumzia zaidi kwa yale maeneo ambayo wananchi walijenga bila kuwepo na mpango maalum na hasa maeneo ya Miji mikubwa kama ya Dar es Salaam, Mwanza na mingine ambapo wananchi walianza kujenga bila ya kuwepo Mipango Miji na hakuna kabisa mfumo wa maji taka ambao umewekwa.

Ninaiomba Wizara, kwa kuwa Serikali imekiri kabisa kwamba kwa wananchi wale waliojenga kiholela ni kwa sababu Mipango Miji ilichelewa, na wananchi wakawa wameshajenga na sasa hivi haiwezekani tena kuwabomolea, wala kuwahamisha na kwa kuwa tayari Serikali imelikubali hilo na imeamua kwa moyo kabisa kuwaandika kuwepo uhalali wa maeneo hayo. Ninaiomba Wizara iangalie maeneo haya, yanatia huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetembelea *Kinondoni B* utasikitika! *Sewerage System* hakuna. Maji yanayotumika nyumbani, maji yanayotoka mabafuni na kadhalika,

yote yapita kwenye mtaro halafu yamesimama wala hayatembei. Sasa ninajiuliza maswali, wanaoishi pale, usalama wa maisha yao uko wapi? Utakuta watoto wanacheza jirani na ile mifereji kwa kweli napata uchungu! Najaribu kuangalia kwamba tutawezaje kudhibiti magonjwa kwa hali hii? Hata kama mzazi akiwa makini kiasi gani, mazingira yanayokuzunguka kama yana hali ile huwezi kuepuka kuwepo na mlipuko wa magonjwa.

Ninaiomba Wizara, maeneo ambayo yamejengwa bila mpango, ambapo hakuna *Sewerage System* wachukue juhudi na tahadhari za dhati kuweka *Sewage System* ili wananchi wanaoishi maeneo yale waweze kunusurika na magonjwa mbalimbali ya mlipuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la uvunaji wa maji ya mvua. Suala la Uvunaji wa maji ya Tanzania bado hatujalipa msisitizo wa kutosha. Maji tunayopoteza kipindi cha mvua za masika na kipindi cha mvua za vuli ni mengi kabisa kiasi kwamba kama yangevunwa kwa utaratibu, kilio cha maji katika maeneo mengi kingepungua. Pia, wananchi wangekuwa wanapata maji safi, tofauti na sasa hivi ambapo wanapata shida ya maji na pia maeneo mengine hata maji wanayotumia siyo maji safi.

Kwenye Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, hapa amesema kwamba, kwa mwaka mzima mwaka 2005/2006 ni sehemu moja tu, eneo la Chunya ndipo walipoweza kusaidiwa hii teknolojia ya kuvuna maji ya mvua na mpango uliopo wa mwaka 2006/2007 ni kusaidia sehemu mbili tu ambazo ni Wilaya ya Lindi na Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maji ya mvua yapo Mikoa yote na Serikali wakati inachukua mwaka mzima kuhangaikia Wilaya mbili, kwa nini hiyo elimu ya kuvuna maji ya mvua isipelekwe maeneo mbalimbali kwa wakati huu? Kwa nini tusubiri mwaka mmoja tushughulikie Wilaya mbili wakati hiyo elimu tungeweza tukasambaza, wataalam wakaendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali ianze kutumika haraka tukijua hasa Tanzania kwa jinsi gani tunavyokabiliwa na hali ya ukame hasa baada ya misitu yetu kuharibiwa kwa kiasi kikubwa?

Kwa hiyo, ninaishauri Wizara kwamba, badala ya ku-*concentrate* kwenye Wilaya mbili, ipange mpango maalum wa kuhakikisha angalau kwa mwaka mmoja inaelimisha Wilaya 20. Serikali iwasaidia wananchi ili wapate elimu na zaidi kuwasaidia pale inapowezekana *financially* waweze kujenga hayo mabwawa ya kuvunia maji ya mvua ili tuweze kupambana na suala la upungufu wa maji mkubwa tulio nao hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi nasema kwamba Tanzania kwa kweli tuna bahati. Tuna bahati sana! Tunachokosa ni mipango na jinsi gani ya kuweza kupanga shughuli zetu kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba tukae chini tupange na tuweke mikakati ambayo itatusaidia kuweza kutumia rasilimali tulizonazo zote. Tatizo ni

kuweza kupanga vizuri mipango yetu ili tuhakikishe kwamba rasilimali tulizonazo zinatusaidia kwa ajili ya kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi, nasema ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Magdalena. Sasa Mheshimiwa Mhina karibu. Ah! Naona Mheshimiwa Mhina hayupo, basi nimwite Mheshimiwa Kabuye na kama muda wetu utaturuhusu tutaendelea na Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Zambi. Mheshimiwa Kabuye, tafadhali.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Naomba niseme kidogo, kwa Kagera mara nyingi huwa tunasema: *How CCM Government Underdeveloped Kagera?* Hii inaweza ikathibitishwa. Leo hii kuna mipango inayopangika, kuna utafiti wa maji chini ya ardhi, Kagera *zero*, kuna visima vilivyochimbwa na Makampuni binafsi lakini Kagera *zero*, kuna visima vilivyochimbwa na mawakala, lakini Kagera *zero*. Kagera ina matatizo gani?

Nilizungumza juzi kwamba ukiangalia Kagera, hakuna Wilaya iliyo na hospitali ya Serikali, kila mara tunagongwa kwenye hospitali za *Mission. What is wrong with Kagera*? Ukienda upande wa elimu, ni Shule zilizoachwa na Mkoloni na hizo nyingine hazijui hata kukarabatiwa. Nini? *Why are you underdeveloping our Region! You CCM Government*! Huo ulikuwa ni utangulizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wakati wananchi wa Kagera watafikia mahali watasema afadhali Mkoloni. Hawatafika huko, lakini wanaweza wakafikishwa kwa shida. Halafu nawaombeni, mimi ni Mwalimu, hivi unaposema kwamba unaunga mkono kwa asilimia mia moja, maana yake ni *excellent!* Yaani vyema sana! Kweli?! *Excellent*! ni kweli kabisa asilimia mia moja, hakuna makosa. Hivi mnatania au mnafahamu maana ya asilimia mia moja? *(Kicheko/Makofi)*

Mkoloni alijua huko akatutengenezea visima vya pete *(ring wells)* kwenye matatizo, hivyo visima vingine vimeshafutika, katengeneza malambo, malambo mengine yamejaa mchanga na udongo umejaa. Mkoloni ajitahidi kutangeneza mifereji, yaani akatengeneza hata visima virefu vya *wind mill,* leo hii hakuna. Sasa naomba sana tuangalie tusije tukawafikisha wananchi kuwa kama wana wa Israel. Walifika mahali wakambana Musa kwamba, Bwana, afadhali ungetuachia Misri, tunateseka lakini tulikuwa tunakunywa maji, leo umetuleta jangwani tufe! Wananchi tusiwafikishe hapo, fanyeni kazi kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunasemaje? Naishukuru hotuba …

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, kanuni ya ngapi Mheshimiwa Mongella, tafadhali.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Kanuni ya 42. Mheshimiwa Phares Kabuye ni msemaji mzuri sana na anatusaidia sana kwenye Bunge la Afrika, lakini hii sidhani kama iko kwenye utaratibu katika kipindi hiki tulichofikia cha ukombozi wa Bara la Afrika, tukisikika tunamsifu Mkoloni, mimi nafikiria na heshima nilizonazo kwa Mheshimiwa Kabuye hii ni nje ya utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni hiyo imesomwa na mimi naomba nitumie Kanuni namba 55, kifungu cha pili kwamba Spika anaweza akatoa uamuzi hapo hapo juu ya jambo lolote lililosemwa ama baada ya muda. Kwa hiyo, kwa kufuatana na muda tulionao, ninaomba jambo hili nilitolee utaratibu baadaye. Lakini kwa sasa tuendelee na hotuba ya Mheshimiwa Kabuye na baadaye nitatoa utaratibu.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwetu kuna hadithi moja inayosema: "Nyani alikaa juu ya jiwe akatoa ushuzi unaonuka, lile jiwe halikujitikisa, lakini nyani akasema pamoja na kutojitikisa, wewe jiwe umekisia." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna anayemsifu Mkoloni, nimesema tunaweza tukafikishwa hapo kwa sababu waliotumikiwa na Mkoloni hawajafa, wengine ni akina sisi, wanalinganisha na Mkoloni, sio simba!

**MBUNGE FULANI:** Ni mtu!

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Ni mtu na watu tunachokitaka ni huduma, hata kama inaletwa na shetani, kwangu shetani akileta maji nitayapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biharamulo tumepewa Shilingi milioni themanini kwa ajili ya maji. Katika Mkoa wa Kagera, Biharamulo ni Wilaya kubwa. Ninaposema Biharamulo ni pamoja na Biharamulo Mashariki kwa sababu ile Wilaya bado hatujafanya taratibu za kujitenga na katika Mkoa wa Kagera. Biharamulo ni kame kuliko Wilaya nyingine, lakini tumepewa Shilingi milioni themanini ambayo ni sawa na visima viwili au ni miradi ya *gravity* miwili.

Ndugu yangu Waziri wa Maji, nilikuwa nimemwandikia barua ya kuomba, tuna mpango tunatengeneza maji ya bubujiko yenye gharama ya Sh. 61,000, kwa Shilingi milioni 80 tutatengeneza *gravity* ngapi? Kwahiyo, naomba sana, Biharamulo tuna shida ya maji hasa katika Tarafa za Lusahunga na Lunazi, kuna Vijiji vyenye shida ya maji. Mtu anakwenda na ndoo au debe anaona havitoshi, mpaka anabeba kibuyu mgongoni kama anayebeba mtoto ili angalau aweze kuleta maji ya kutosha. Kama ana mtoto, atabeba mtoto mgongoni, kibuyu mbele na mtungi kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mtusaidie. Sisi hatuna ugomvi, tunalolitaka ni huduma. Tunaomba haya malambo ambayo mmesema nimemsifia Mkoloni, malambo ya Nyabugombe, Nyakahura, Kalenge, Lukora na Kabimbi yote yameharibika. Tunaomba yote hayo yafufuliwe ili wananchi wapate maji. Yote hayo yamechimbwa na Mkoloni na wananchi wanaona. Wananchi wana matumaini na Serikali yao mpaka sasa, sijasema kwamba wameshakata tamaa, lakini wanaweza wakakata tamaa. Tunaomba maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna miradi ya zamani. Tulikuwa tumevuta maji kutoka Ziwa Victoria kuja mpaka kwenye Vijiji vya Kachwamba. Leo hii mradi huu umekufa. Maji yanatoka Ziwa Victoria, nadhani yanakwenda Shinyanga na Kahama, hayawezi kwenda hata kilometa ishirini kando kando ya ziwa. Hatuna maji! Mimi sisemi mje mwangalie, maana kama ni kutembea, Mtanzania aliyezaliwa hapa na mtu amejifunza jiografia anafahamu hata bila kwenda Biharamulo. Waziri Mkuu, ndugu yangu Waziri wa Maji anajua kabisa ni wapi kuna maji na wapi hakuna.

Kwa hiyo, sisi tunaomba tusaidieni sana kuleta maji. Kuna Mto Kagera, unaweza kuvuta maji na tukapata maji. Kuna Mto Rusumo, tunaweza kupata maji. Lakini la ajabu kabisa, mimi katika Kijiji ninachozaliwa huko Nhongola, unapopika chai, huna haja ya kuweka maziwa. Maji yenyewe yanafanana na maziwa, labda ile ladha ndio kasoro. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yenyewe ni meupe, yaani utafikiri maziwa na hayo ndio tunayokunywa na yenyewe unakwenda kusubiria. Mnaposema akinamama wanabakwa, wanawasubiri kwenye mto usiku, wanawabaka. Usiku wanaamka na kama akinamama sio waaminifu, ndio njia ya kusema nakwenda kuchota maji, saa kumi na mbili! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika mahali ambapo sipajui. Yote haya nayasema tu, sio kwa sababu ya kufurahisha, nawaombeni sana. Sisi Serikali yetu tunaipenda. Mimi nilikuwa mtu mzima wakati tukitafuta uhuru na wananchi tukiwaahidi mambo mengi sana. Sasa tunataka hayo yatimizwe moja baada ya lingine, hatuna ugomvi na mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda Afrika ya Kusini, Wakoloni wamechelewa kuondoka, hali yao ni nzuri. Ndio! Nikawauliza ninyi mnafanya hivi, wanasema sisi dhahabu yetu tumeiweka hapa na ya Tanzania tunazidi kuleta, kwa hiyo sisi tutang'aa. Sasa ndugu zetu na maji nayo jamani! Nawaombeni, Mji wa Biharamulo kama walivyosema Kibondo kwa kweli unakua kwa haraka sana, lakini tunapata maji kwa mgao, kwa wiki mara mbili. Mabomba mengine ni ya chuma, yaliachwa zamani kabisa, maji yanapotoka yanakuwa mekundu kama viti vyetu, kwa sababu ya kutu. Kwa hiyo, nawaomba sana mtusaidie, msifanye mzaha. Kama wenzangu walivyosema, maji ndio kitu kikubwa sana. Mwili wa binadamu asilimia zaidi ya sabini na tano ni maji. Kama hakuna maji, ni matatizo makubwa sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujitahidi, tugawe pesa zetu hizi bila ya upendeleo. Tusije tukawa kama misahafu kwamba aliyenacho ataongezewa na yule ambaye hana, hata kile alichonako atanyang'anywa. Hapana, tusifanye hivyo. Yale yalifanyika wakati ule na yalipendeza, lakini kwa leo ukifanya hivyo, pale kwenye maji ndipo upeleke maji, pasipo na maji hata vile visima vikikauka sio hoja, hayo hayapendezi. Ndugu yangu, aah, wakati mwingine inakuwa kama unamsuta ndugu yako na yeye ana nyundo ya kutengeneza pesa, lakini baba kwa mtoto hakuna kusema sina chakula. Wewe umeshajiita baba, lazima utimize kila kitu. Kama baba ni Serikali, sasa tumwambie nani? Wa kumwambia ni Serikali! Hakuna kwingine pa kwenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutawasema na kumsema mtu sio kwamba unamchukia. Sisi ni wazazi, mtoto unaweza ukampiga mikwaju, sio kwamba unamchukia, hapana. Ni mtoto wako. Kwa hiyo, tunaposema sana, mara tuna-*refer* Wakoloni, tunataka mwone kwamba sisi tuna uchungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafurahi sana kama kweli angalau haya yaliyokusudiwa yamefanyika na yafanyike. Niliwaambia juzi kwamba watu wanatufahamu, wanangojea sasa fulani tunavyomfahamu na uzembe tuone atafanya nini. Fulani tunavyomfahamu ni mchapa kazi: Je, katika Serikali hii atalegea?! Tusaidieni tupate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi nawashukuru na namshukuru kwa kunipa nafasi hii kwa sababu inawezekana katika Wizara zilizobaki nisiweze kuchangia kwa sababu ninashtakiwa kwamba niliiba Ubunge. Kwa hiyo, nakwenda kwenye kesi, kuanzia wiki ijayo sitakuwepo. Kwa hiyo nashukuru kwamba nimesema haya, naomba visima vyetu vifufuliwe, malambo niliyoyataja yafufuliwe na naomba hizo Tarafa za Lusahunga, Nyarubungo, Kata ya Nyabusozi na Kata ya Lunazi zipate maji ili wananchi waisifu Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tunayoyasema mnaweza mkasema, ohoo, unausifu ukoloni, lakini siku moja watatukimbiza. Acha ya kumsifu Mkoloni, watatukimbiza kabisa na watatupiga. Kwa hiyo, ni afadhali tuanze kutukanana sisi wenyewe, tuanze kulaumiana kabla hatujalaumiwa na hao watu wanaotuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama ninavyosema sina shida na Serikali, tumpe nafasi mwenzetu. Ukisema kwamba ameanza, hakuanza, ameshakuwa Waziri zaidi ya mara moja, uzoefu anao. Akishindwa si kwa sababu ya kuanza, hapana. Wizara ya Maji inafanana na Wizara zote zile alizowahi kuongoza. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwa uzoefu wake alioupata na uzoefu ilionao Serikali yetu, watatusaidia na hasa kwenye janga hili, tuanze angalau na maji basi, hata kama mengine yatakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nawatakia kila la kheri na naunga mkono hoja, sio kwa asilimia mia moja. Hakuna *absolute* hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa taarifa niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba, wanapochangia hoja, Kanuni Na.50 Kifungu cha

(8)(ii) kinasema: “Jaribu unapozungumza Bungeni usitumie maneno yanayoudhi wenzako.”

Kwa hiyo, naomba kutoa hilo angalizo na naomba sana Waheshimiwa Wabunge tujali sana hilo, kutotumia maneno ambayo yanaweza kumuudhi mtu yeyote yule ndani ya Bunge ama nje ya Bunge. *(Makofi)*

Kulingana na muda tulionao, tumebakiwa na dakika chache sana na haziwezi kutosha kwa mchangiaji yeyote kuchangia kwa kuzingatia kwamba kila mtu anataka achangie kwa muda aliopangiwa. Kwa maana hiyo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.36 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 11 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*